
MASOMO YA BIBLIA YA SHULE SABATO

Watu wazima



# Tazama Naja Upesi

Vol. 93 No. 3
Julai – Septemba, 2017

# YALIYOMO

1. Utukufu, Furaha–Tumaini lenye Baraka/ 5
2. Dalili za kurudi Kwa kristo/10
3. Ujumbe wa Onyo kwa Ajili ya Siku zetu./15
4. Imani potofu katik siku za mwisho/20
5. Hakika Yesu anakuja tena./25
6. Akija Kwa Nguvu nyingi na Utukufu Mkuu/ 31
7. Kukesha na Kungoja./36
8. Uhusiano wa Pekee pamoja na Kristo./41
9. Jiweke Tayari/46
10. Kufanya kazi kwa ajili ya Bwana./52
11. Busara za Mipango ya Mungu./57
12. Kuenea kwa kilio kikuu./62
13. Usiku wa Manane hadi Mapambazuko./67
14. Matokeo ya Mwisho / 72

**Masomo ya Biblia ya shule Sabato** ni utaratibu wa mafundisho ya kila siku, ni msingi pekee juu ya Biblia na Roho ya Unabii, pasipo maelezo ya nyongeza.

Nukuu itolewe kwa ufupi sana kama ikiwezekana, kwa ajili ya kuelekeza ufahamu. Mabano huwekwa baadhi ya sehemu ili kusaidia kuelewa maana ya jambo kwa usahihi na kwa ulaini, Jifunze zaidi katika chanzo kilichopendekezwa.

# UTANGULIZI

Swala la kuja kwa Yesu Mara ya pili – ambalo limetajwa katika Biblia mara mamia, limekuwa tumaini lenye Baraka kwa Kanisa katika vizazi vyote. Ni msingi wa ujumbe wa mwisho- ukweli wa leo-kutolewa ulimwenguni.

Ufahamu wa tumaini la kuja kwake Yesu mara ya pili ni msingi ambao hufungua historia yote ambayo hufuatiwa na maelezo yote ya masomo ya baada au yajayo - Uinjilisti Ukr. 220.

Kadri watu ambao hutangaza kwa shauku ya kungoja kwa ajili ya ujio wa Yesu Kristo, tungeangalia kila dalili inayoelekeza katika tukio hili. Hili litakuwa tukio kuu katika historia ya dunia. Ingawa hatuwezi kujaribu kuweka au kupanga tarehe ama siku kwa ajili ya kurudi kwa Bwana wetu, tunaambiwa kuwa, kwa kuziangalia sana dalili na Ishara zilizotolewa na Manabii, Mitume na hata Yesu mwenyewe (Hasa katika Mathayo. 24), tunatambua ya kwamba tukio la kuja kwa Yesu liko karibu sana- Tena mlangoni katika siku hizi.

Kulingana na Mtume Petro, hatutazamii tu, bali pia"kuhimiza" ujio wa Bwana (2 Petro. 3.12). Tunaweza hakika kuhimiza kuja kwake na kujiandaa kujitayarisha kukutana naye (Luka. 12.36 -38, Matendo 3.19-20, 2 Petro 3.14) na kwa kuifanya kazi ambayo ametukabidhi kuifanya (Luka. 19:12, 13, 15: 14.23, Mathayo. 24.14). Kama tunapuuza kufanya hivyo, tutakuwa tumeshikilia dhamana"Kucheleweshа" kuja kwa Bwana. Wakati tunapojifunza masomo haya, wanafunzi wote wa shule sabato watapata fursa nzuri ya kujichunguza wao wenyewe binafsi katika nuru ya maswali haya. Je, kwa maisha yangu nimekuwa"nikiharisha" au"kuchelewesha" kuja kwa Bwana? Kama unayosababu ya kweli kwa kuamini kwamba nimechelesha kuja kwake, nitawezaje kufanya badiliko katika maisha yangu na kuanza kutenda kwa moyo wote, je, Bwana anataka nimfanyie nini? Majibu ya wazi juu ya maswali haya yatapatikana katika masomo haya.

Haitoshi kuamini kwetu katika kuja kwa Yesu upesi kwa kufahamu kila kitu kilichoandikwa kuhusu hilo, na kulihubiri kwa wengine. Kuna waumini wengi sana waliokiri ujumbe wa Malaika watatu ambao wako kwenye"njia pana" wakati wanasafiri katika njia nyembamba wanajidanganya wao wenyewe na wengine pia. Kutobadirika kwao huwaongoza wenye dhambi kuwa na mioyo migumu na udhuru."Hakuna utofauti kati yetu. Tunafanana, tunavaa, tunaongea, na kutenda hakuna tofauti" – (Shuhuda ya 1 Uk. 128). Hivyo itakuwa"kupimwa katika mizani na kuonekana kupungua" (Maandiko ya awali Ukr. 37) somo hili linatuonyesha namna ya kunavyoweza kuepuka aina hii ya Roho yenye mwamba.

Masomo haya tuweze kujifunza yaweze kutongoza kwenye kina cha wakfu kadri tunavyokuja karibu na Kristo na kumkaribia kila mmoja wetu. Hebu tuungane wote katika kufanya maombi kwa ajili ya kudhihirishwa kwa Roho Mtakatifu, kwa ajili ya kuifungua kazi, kwa hiyo tuweze kujiandaa katika matarajio yenye shauku, kama ilivyokuwa kwa watu wa Mungu wa kweli mnamo mwaka 1884.

*Idara ya shule ya Sabato Bara kuu (GC)*

*SABATO YA TAREHE 01 JULAI, 2017.*

## Sadaka za sabato ya kwanza Ni kwa ajili ya Kanisa dogo lililoko Washington DC nchini Marekani.




Ndugu wapendwa, Dada, na marafiki duniani kote.

Kadri watu wanavyojiandaa kwa ajili ya kuja kwa Yesu tena mara ya pili, tunadaiwa deni la shukrani kwa baba zetu waliotanguliza, ambapo chini ya majaaliwa ya Mungu ilianzishwa nchi ambayo humudu uhuru wa dini kwa watu wote mmoja mmoja. Taifa la Marekani ni nchi ya tatu duniani yenye wakazi wengi zaidi ina wakazi milioni mia tatu na ishirini na nne na laki mbili za ishirini na saba elfu. [324, 227, 000] Mji mkuu wa Taifa upo Washington DC (District of Columbia) na imeungana na Tawala za Virginia na Marylandi kwa maili 64 za mduara wa barabara. Kuwa nyumba za makazi ya watu zipatazo laki sita na hamsini (650, 000) ikijumulishwa na nyumba za watumishi wa serikali, wanadiplomasia wa nchi za kigeni na familia zao, kwa wiki zaidi ya watu miloni moja husafiri kwa kubadilishana kutoka miji ya Virjinia na vitongoji vya Merylandi, Washington DC ni jiji la 24 kwa wakazi wengi zaidi ndani ya Marekani, na la 7 katika ukubwa wa majiji. Jiji hili kubwa lenye uchumi wake, kisiasa na utamaduni wa kibiashara ni nchi yenye rutuba kwa ajili ya kueneza Injili.

Kazi ya mtangenezo ilianza katika eneo la Washington DC katika miaka ya 1970 na washiriki wachache sana. Mnamo mwaka 1980 nyumba ndogo ilinunuliwa katika milima ya Hekalu (Tempo) katika vitongoji vya Wilaya ya Meryland na ikapendekezwa nyumba hiyo iwe Kanisa. Hili Kanisa dogo limekuwa Alama ya Nuru katika eneo hili kubwa. Ndugu wengi wamekuwa wakija kupitia Milima ya Hekalu na wanasaidia kujenga huduma katika eneo hili. Kanisa dogo ambalo limekuwa likitumika miaka mingi na lina uwezo wa kubeba Takribani watu 30, limekuwa dogo sana katika kuabudia kwetu. Pamoja na kuongezeka kwa washiriki na kuhudhuria kwa wageni wa kawaida, tuko kwenye hitaji la jengo kubwa. Baada ya kuomba sana na kufunga, maamuzi yalifanyika kununua eneo kubwa kwa urahisi. Mikakati iliwekwa katika jiji hili la Metropolis, inaturuhusu sisi kutimiza agizo bora la Bwana wetu kwamba"Enendeni na kuyafundisha mataifa yote". (Mathayo. 28:19, kuweka mkazo au nguvu) kutangazwa kwa Injili lazima isambazwe kwa kila Taifa, lugha, jamaa na watu kwa ajili ya ushindi wa nafsi kwa Bwana.

Tunaomba kwa wanafunzi wote wa shule ya Sabato watusaidie kuinua swala hili katika Alama mpya ya Nuru katika Mji Mkuu nchini Marekani. Mungu akuzawadie utajiri utoe ukarimu kwa ajili yake. Tunawashukuru kwa ajili ya kuendeleza ukarimu wenu kwa kuchangia mpango huu wa thamani.

*Ni ndugu na Dada zenu kutoka katika milima ya Hekalu (Marekani)*

# Utukufu, Furaha – Tumaini lenye Baraka

**Tazama Bwana alikuja na watakatifu wake Maelfu Maelfu (Yuda. 1.14 mwishoni).**

"Kwa wasafiri, wwatu wa Mungu, muda kitambo uliosalia wa kukaa katika"Mamlaka uvuvi wa mauti". Tumaini la thamani na shangwe kuu limetolewa katika ahadi ya marejeo ya kuonekana kwake, yeye amabye ni"Ufunuo na uzima" kuwarejesha tena watu wake waliofukuzwa nyumbani" – *Pambano* kuu ukr. 299.

**Imependekezwa kujifunza: Pambano kuu Ukr. 299-303.**

## *Jumapili* *Tarehe 25 Juni*

### 1. ALITIWA MOYO KWA AHADI ZA MUNGU

**a. Katika historia ya mapema kabisa, Nani alikuwa mzee wa saba kutoka kwa Adamu kuonyeshwa katika maono- kwa jinsi gani lilimchochea katika njia njema? Yuda. 1:14-15.**

"Katika Roho ya Unabii (Mungu) alimuchukua (Henoka) hadi katika vizazi vitakavyoishi baada ya gharika, na alimwonyesha matukio yaliyounganika pamoja kuja kwa Yesu mara ya pili na mwisho wa dunia. . . "

"Katika maono ya kiunabii alionyeshwa na kuelekezwa kuhusiana na kifo cha Yesu na kuja kwake katika utukufu, akija pamoja na malaika watakatifu kuja kuwakomboa watu wake kutoka kaburini. Pia aliona hali ya machafuko ya ulimwengu wakati Kristo atakapotokea mara ya pili- kwamba kutakuwepo na majigambo, majivuno, ufedhuri na kiburi, kizazi chenye kutenda wapendavyo wenyewe, wakimkana Mungu pekee na Bwana Yesu Kristo na kuikanyaga sheria huku wakidharau upatanisho. Aliona wenye haki wakivikwa taji pamoja na utukufu na kutukuzwa. Waovu walichomwa mbele za Mungu na kuteketezwa kwa moto. "

"Enoka alikuwa Mhubiri wa haki, akiufahamisha ulimwengu kile Mungu alichokuwa amemfunulia"- Wazee na Manabii Ukr. 85, 86

## 2. KUJIAMINI KWA FURAHA.

**a. Elezea njia ya watu wa Mungu katika Agano la kale kipindi walipoonyesha matumaini yao katika kuja kwa Yesu mara ya pili. Zaburi. 50:1- 4, 96:11-13.**

---

"Kuja kwa Kristo ili kupokea utawala wa haki kumevuviwa maneno ya waandishi watakatifu kwa utukufu Mkuu na kwa hamasa kubwa. Washairi na Manabii wa Biblia wameshughulikia kwa maneno yawakayo moto wa kimbingu" –34

**b. Pamoja na lugha adhimu aliyotumia, Nabii Habakuki alielezeaje kurudi kwa Yesu? Habakuki. 3:3-6.**

---

**c. Ni faraja iliyoje, Ahadi ya kutia moyo inarudiwa kwa waumini wa agano jipya, na kwa jinsi gani mvuto huu ungetuvutia sisi katika njia kuu. Matendo. 1:10-11.**

---

---

"Ahadi ya mwokozi ya kuagana pale Mlima wa Mizeituni, kwamba angekuja tena iliangaza juu ya mtazamo kwa wanafunzi wake, fikra zao, mioyo yao ilijaa furaha na matumaini, ambapo (huzuni/ masikitiko) na majaribu yasingeweza kuhafifisha wala kuwazimisha" – Ibid Ukr. 302.

"(Matendo 1.11 imenukuliwa) ya thamani kweli, hii ilikuwa ahadi kwao wanafunzi wenye huzuni. Kwamba wangemwona Yesu tena ambaye alikuwa mpendwa wao Mkuu. Pia ahadi hii ya thamani ni kwa kila mfuasi wa kweli wa Kristo. Hakuna hata mmoja, anaye mpenda Yesu kiukweli atakayesikitika kwa kuja kwake tena mara ya pili. Kadri wanapotazama ukaribu wa kuja kwake mwana wa Adamu, wapenzi wa kweli wa Yesu watatazama mbele kwa matumaini yenye furaha na watatafuta kujiweka tayari kwa kumtazama yeye ambaye nafsi zao humpenda ambaye alikufa ili kuwakomboa wao"

"Yesu anakuja, lakini mwanadamu hasikii ole, mwenye dhambi hasikii kutubu dhambi zake wala kuomba msamaha kwake, kwa maana kila kosa la kila kitu mtu wakati huo litakuwa limeamuliwa kwa uzima au kifo. Wale ambao wameishi katika dhambi watabakia kuwa wadhambi daima, wale ambao wametubu dhambi zao kwa Yesu katika Hema ya patakatifu, wamemfanya yeye kuwa rafiki yao na kupenda kuonekana kwake, wameandikiwa msamaha kwa ajili ya dhambi zao, na wamejitakasa nafsi zao"katika kuutii ukweli" watabakia kuwa safi na watakatifu milele zote" – The Yourth's Instructor, April 1, 1854.

## 3. THAMANI YETU YA KUJIWEKA TAYARI KIKAMI LIFU.

**a. Tunawezaje kupata ujasiri kutoka kwenye tumaini lililoelezewa na Paulo? Tito 2:11-13.**

---

---

"Sisi ni wasafiri, wageni ambao tunasubiria tumaini na kuomba kwa ajili ya tumaini lenye Baraka, na kutokea kwa Bwana wetu na mwokozi Yesu Kristo kwa utukufu. Kama tunaliamini hili na kulileta kwenye maisha ya matendo. Ni juhudi ya matendo gani hii ingekuwa imani na tumaini lenye Baraka ni hamasa kiasi gani ya upendo mmoja kwa ajili ya mwingine, umakini mtakatifu ulio hai kiasi gani kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Na katika heshima yetu kwa ajili ya thawabu, ni msitari gani wa utengano ungekuwa ukishuhudiwa kati yetu na ulimwengu" – Uinjilisti Ukr. 220.

"Mungu hukusaidia kuwa watu wake wakaze macho yao kuelekea mbinguni waangalie ujio wa Bwana wetu na mwokozi Yesu Kristo kwa Utukufu, wakati huo usikivu wa watu wa ulimwengu ukigeukia kwenye makampuni ya biashara mbalimbali, ya kwetu yangekuwa ni ya kimbingu. Imani yetu ingefika mbele zaidi na zaidi katika sura ya mionzi ya Nuru ya uungu kutoka katika Hema ya mbinguni na kuiangazia mioyo yetu, kama vile ilivyoangaza juu ya uso wa Yesu..."Makusudi na nia ya Bwana wetu ni kwamba tungekuwa na mkesha, kwamba wakati ajapo na wakati abishapo tuweze kumfungulia haraka iwezekanavyo" – *Shuhuda ya* 2 Ukr. 194, 195.

**b. Yesu atatokea kwa namna gani kwa wale ambao wanangojea kwa shauku marejeo yake? Ebrania 9:28 (mwishoni).**

---

---

"Kristo kwenye kuifunga kazi yake kama mpatanishi" Atatokea pasipo dhambi kwenye ukombozi na kuwabariki watu wake wanaongojea uzima wa milele" – Pambano kuu Ukr. 485.

"Yesu anakuja kama alivyopaa kwenda mbinguni, pamoja na nyongeza ya mng'ao wa pekee anakuja pamoja na utukufu wa Baba yake na Malaika wote watakatifu wa mbinguni wakimsindikiza katika njia yake. Badala ya taji ya kikatiri ya miiba ya kutoboa Hekalu lake takatifu, ni taji la mng'ao wa utukufu wa kusitaajabisha akiwa na uso wa utukufu wa kivita. Hataonekana tena mtu wa masikitiko na huzuni bali uso wake utang'aa mng'aro wa ajabu kuliko jula la adhuhuri. Hatavalia kanzu ya kufumwa, bali vazi jeupe kuliko theruji- lenye mwangaza wa kustaajabu" – *The yourth's Instructor*, April 1, 1854.

## 4. TAMANI MAREJEO YAKE.

**a. Ni ujumbe gani katika mahubiri ya Luther yaliyovuma na fundisho la Paul kuhusiana na saa ya hukumu ya mwisho? Ebrania. 9:27.**

"Luther alitangaza,"Nashaurika mimi mwenyewe kwa hakika, kwamba siku ya hukumu haitakosekana katika utimizo wa miaka mia tatu. Mungu hataweza, na hawezi kuuvumilia ulimwengu huu mwovu zaidi. " Siku kuu ya kutisha inakaribia ambapo ufalme muovu utapinduliwa na utaangamizwa – *Pambano kuu* Ukr. 303.

**b. Wanamatengenezo walikuwa na uthibitisho gani wa hatia, vilevile nini kingekuwa kipaumbele chetu kikuu siku hizi? Ufunuo. 16:15.**

---

---

"Ulimwengu huu kongwe hauko mbali kufika mwisho wake" Alisema milanchothon. " Calvia huwaagiza wakristo" wasiwe wa kusitasita". Kuitamani na kuikumbatia siku ya kuja kwa Kristo kama matukio yote ya heri zaidi hutangaza kuwa"familia nzima yenye uaminifu wataiihifadhi na kuitunza mandhari ya siku ile. Lazima tuwe na shauku na Kristo, lazima tumtafute, tutafakari, anasema, (alfajiri)pambazuko ya ile siku kuu Bwana wetu atadhihirisha ukamilifu wa utukufu wa ufalme wake. "

"Si Bwana Yesu aliyeinua juu utu wetu mbinguni? Mwana matengenezo wa nchini Usikochi alisema"Hatakuja? Tunajua ya kwamba atarudi pamoja na ile Parapanda" Ridiley na Latima ambao waliyaongoza maisha yao yawe ya hali ya chini tena ya duni kwa ajili ya ukweli, walio na Imani ktk ujio wa Bwana. Ridiley aliandika, ulimwengu pasipo shaka- Hili inanifanya kuamini, na ndiyo maana nauambia, huvutwa- kwenda mwisho. Hebu tuwe pamoja na Yohana mtumishi wa Mungu, kilio ndani ya mioyo yetu kiende kwa mwokozi wetu Yesu Kristo, Njoo, Bwana Yesu Njoo -" Idib. "

"Kurudi kwa Yesu katika ulimwengu huu hakutachukua muda mrefu, hebu hili liwe wazo la msingi la kila ujumbe"

"Tumaini lenye Baraka la kuonekana tena mara ya pili kwa Yesu, ni hali halisi yake ya dhati, huhitaji mara kwa mara kujitoa kwa watu. Kutazama upesi kutokea kwake Bwana wetu itatuongoza sisi kuhusiana na mambo ya ulimwengu kuwa si kitu wala si chochote. . . "

Kwa sasa haiwezekani kusema kwa watumishi wa Bwana, kama ilivyokuwa kwa Nabii Daniel" Wakati ulioamriwa ulikuwa mrefu" (Dan 10:1). Ni sasa lakini wakati ni mfupi hadi hapo mashahidi wa Mungu watakapokamilisha kazi yao katika kuitayarisha njia ya Bwana" – *Shuhuda ya 6* Ukr. 406.

## Alhamisi — *Tarehe 29, Juni*

### 5. SUBIRI KWA UKAMILIFU SIKU YA AHADI.

**a. Elezea wajibu wa wale wote ambao wanakutana kikamilifu na Mkuu wa Amani wakati arudipo. Amos 4:12 (Mwishoni) Zefania. 2:3.**

---

---

"Kristo husema"Nayajua matendo yako (Ufunuo. 2.2) Hukufahamu pengine unayoishi maisha ya utimilifu na kama unampenda kwa kuongea na kumwaza yeye, . Je, tunatarajia kuipata mbingu na kujiunga angalau na kwaya ya mbinguni? Kama vile tunavyoingia ndani ya kaburi tutainuliwa juu kama tabia ni njema... Huu wakati wa sasa ni kwa ajili ya kufua na kunyoonsha ni wakati wa kufua joho zetu na kuzifanya ziwe nyeupe kwa damu ya mwanakondoo.

"Wakati mwanasheria alipomwendea Yesu Kristo na kumuuliza"Nifanye nini ili kuurithi uzima wa milele?"Jibu lilikuwa"Tunza Amri" Hili swali lilikuwa la kinyume lililoulizwa na mwanasheria na alipokea jibu la kinyume kama alivyouliza kinyume" – *Manuscript Releases* Vol. 9, Ukr 262.

**b. Kutakuwa na kina cha hisia kiasi gani kwa wale wote ambao kwa moyo wote wameipokea na kuikumbatia ahadi ya Kristo kwamba atarudi upesi? Ufunuo. 22:20.**

---

"Ninatamani kumtukuza Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, nahitaji sauti yangu iwe mwangwi na kujirudiarudia katika mahakama za mbinguni. Utakuwepo pale? Kisha inakulazimu kuiongoza sauti yako kumsifu na kumtukuza yeye duniani. Ndipo utakavyoweza kujiunga na kwaya ya mbinguni na kuimba wimbo wa Musa na Mwana kondoo. Mungu anatusaidia sisi, na kutujaza utimilifu wote na nguvu ndipo tunaweza kujaribu furaha ya ulimwengu ije" – *The Ellen G. White 1888 Materials* Ukr. 128.

## Ijumaa — *Tarehe 30 Juni*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI.

1. **Ningezingatia nini kuhusu matamanio yangu ya kina kwa ajili ya kurudi kwa Yesu?**
2. **Kwa nini Ahadi zinazohusu kurudi kwa Yesu zimetolewa kwetu moja kwa 1?**
3. **Kwa nini ni muhimu kuchimba uhakika wa tumaini kwa kushiriki ukweli huu pamoja na wengine?**
4. **Katika karne ya 16 kwa jinsi gani wanamatengenezo walitia mkazo Imani ya kurudi kwa Yesu?**
5. **Tunaokolewa kwa njia ya Imani, kwa hiyo ni sharti gani hufunua Imani yetu halisi?**

# Dalili za kurudi Kwa kristo.

**Nanyi kadhalika, mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu. Luke 21.31.**

"Kristo aliwataka watu wake wakeshe kwa ajili ya dalili za kuja kwake na kushangilia kwa kadri ambvyo wangetazama na kuziona dalili za kuja mfalme wao- Pambano kuu ukrs 308.

**Imependekezwa kujifunza: Pambano kuu ukr 31- 38, 304-316, 333-334.**

## *Jumapili* *Tarehe 02 julai*

### 1. KUYAONA MATUKIO YAJAO

**a. Ni utabiri gani aliofanya Mwana wa Adamu kuhusiana na Uwepo wa Hekalu kuu katika siku zake - Tukio ambalo wasingeweza kulidhania mitume? Mathayo 24:1-2**

Kadri Utumishi wa Yesu ulivyovutia kwenye Hekalu lenye uzuri na fahari. Jambo gani limeshakuwa wazo lisilosemaka Kwa hao waliokataliwa! Mtazamo wake ulikuwa mzuri mno, Lakini Kwa masikitiko alisema. Ninayaona haya yote, Majengo yaliyojengwa kwa maajabu hasa mnaona kuta hizi zinaonekana kama hawezi kupatwa na uharibifu lakini sikilizeni maneno yangu. Siku inakuja ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe jingine ambalo hatabomoshwa -" *Tumaini la viazi vyote* ukr 627

**b. Maswali gani ya mitume yenye kuvutia, Na kwa Jinsi hili liliingiliana na unabii wa Yesu kuhusiana na mwisho wa dunia? Mathayo 24:3**

"Wanafunzi walihusisha maangamizi ya Yerusalem pamoja na matukio ya kuja binafsi kwa kristo katika utukufu wa kidunia kuchukua kiti cha Enzi cha ufalme wa kidunia, kuwadhibu wayahudi wenye moyo mgumu wa kutotubu, na kuvunjika mbali nira ya utawala wa Rumi. Bwana alikuwa amesha waambia kwamba angerudi tena mara ya pili. Hivyo katika kutaja Hukumu za juu ya Yerusalemu, akili zao zilirejeshwa kwenye ujio huo. *Pambano kuu* ukr 25

## 2. UNABII ULIOTIMIA BAADA YAKUPAA KWA KRISTO

**a. Ni onyo gani tungelishikiria kutoka kwenye dokezo la kiroho la kuangamizwa kwa hekalu mnamo mwaka wa 70 A. D kama vile Yesu alivyokuwa ametabiri ? Isaya 30:12- 13**

"Upofu Sugu na Ukaidi wa viongozi wa Wayahudi, na uharifu wa makosa ya kuchukiza uliokuwa ukifanyika ndani ya Mji uliozingarwa ulisisimua hasira ya Warumi. …. katika ghadhabu yao maaskari walirusha na kuvurumisha ndimi za moto na mishare kwenye kona za Hekalu, na kwa mapanga yao waliwachinja kwa wingi wale ambao walikuwa wakitafuta mahitaji huko nje . Damu ilitiririka chini ya hakalu kama maji. Maelfu juu ya maelfu ya Wayahudi waliangamia, sauti ya kivita ilisikika ikisema -"Ikabodi, utukufu umejitenga umeondoka" - *Pambano kuu* ukr 33

"Mji wote pamoja na Hekalu zilizochomwa hadi kwenye misingi yake na juu ya ardhi iliyokuwa ikisimama nyumba takatifu- ililimwa kama shamba" - [Yer 26:18] Ibid, ukr 35

**b. Baadhi ya majina yenye umuhimu wa kuvutia tunaweza kubarikiwa tokea kwenye namna tu ya wale amabo waliyatunza na kuyashika maneno ya Yesu aliyoyatumia. Luka 21:22.**

" Kwa muda wa miaka saba mtu mwanaume aliendelea kupanda na kushuka katika mitaa ya yerusalemu, akitangaza ole ambao ulikuwa una kuja juu ya mji. Cha ajabu alifungwa gerezani na kuchapwa viboko . Lakini hakulalamika midomo yake. Kwa matusi na kubezwa alijibu, ole ole kwa Yerusalemu, Ole, ole kwa wakazi wake kilio cha onyo lake hakikukoma hadi hapo alipochinjwa kwa kuzingirwa, yeye alikuwa ametabiri.

"Hakuna hata mkristo mmoja aliyeangamia ndani ya angamizo la yerusalemu. Kristo alikuwa amekwisha kuwaonya mitume wake na wote ambao waliamini maneno yake walikesha kwa ajili ya dalil zilizioahidiwa" [Luka 21. 2 -22 imenukuliwa ] - Ibid ukr 30.

"Luka 21.20-22 imenukuliwa, hili ni Onyo lilitolewa litunzwe baada ya miaka Arobaini, hadi angamizo la Yerusalemu.

Ombeni kwamba kukimbia kwenu kusiwe siku za baridi, wala siku za baridi, wala siku ya sabato kristo alisema [Mathayo 24:20] Miaka Arobaini baada ya ufufuo wake [ sabato] takatifu bado ilitunzwa. Kwa miaka Arobaini Mitume waliomba kwamba kukimbia kwao kusingekuwa siku ya sabato" - *Tumaini la vizazi vyote* ukr 630.

## 3. WAKATI WA KIPINDI CHA UNABII - GIZA LA VIZAZI

**a. Tukio gani lingekuja juu ya waumini baada ya mauwaji ya haraiki ya mji wa Yerusalemu mwaka wa 70 A. D ?**

"Kutoka kwenye tukio la uharibifu wa maamuzi ya Yerusaemu, Kristo alipitisha na kuunganisha kwa haraka habari na mlolongo wa historia ya mwisho wa dunia - na kuja kwake mwana wa Mungu katika nguvu kuu na utukufu . Katika matukio haya mawili, kuliweka wazi maono ya kristo ya Giza la kristo la karne nyingi kwa ajili ya kanisa lake, kukumbwa na umwagai wa damu huzuni machozi na maumivu makali . - *Tumaini la vizazi vyote* ukrs 630 630, 631 .

**b. Ilikuwaje kipindi hicho cha kihistoria cha dhiki iliyoonyeshwa katika unabii wa kitabu cha ufunuo ? Ufunuo 11: 2, 3:13.5**

**c. Maandiko gani matakatifu hutuongoza kuhusu muda wa unabii a kufahamu jinsi ya kupiga mahesabu ya urefu wa kipindi hiki, kutunza katika akili kwamba unabii unahesabika katika siku 30 za mwezi na siku 360 kila mwaka? Hesabu 14:34, Ezekiel 4:6.**

"Ukandamizaji wa maandiko matakatifu chini ya utawala wa Rumi, Matokeo ya kutisha ya ukandamizaji huo, mwishowe umetukuza neno la Mungu kwa uwazi kabisa kupitia kalamu ya kinabii. Yohana akiwa uhamishoni katika visiwa vya upweke vya Patmo alipewa maono ya miaka 1260 kipindi ambacho mamlaka na nguvu ya upapa iliruhusiwa kukanyaga na kuponda neno la Mungu" - *Roho ya unabii* Vol . 4 ukr 188

"Miezi Arobaini na mwili, ni sawa na wakati, nyakati mbili na nusu wakati, miaka mitatu na nusu, au siku 1260 za Daniel 7. Ni Kipindi cha muda ambacho mamlaka ya nguvu za upapa zilikandamiza watu wa Mungu. Kipindi hiki kilianza kwa nguvu kuu mno ya upapa mwaka 538 B. K, na kukomea mwaka 1798 katika wakati huo papa alikamatwa mateka na jeshi la Ufaransa, Utawala wa upapa ulitiwa jereha lake la mauti, na unabii uklikuwa umetimia" mtu akichukua mateka atachukuliwa mateka" *[Ufunuo 13.10] Pambano kuu* ukr 439 .

## 4. MATUKIO MATATU YA KIHISTORIA

**a. Kabla ya mwisho wakati wa kipindi cha miaka ya kinaubii 1260 (yaani mateso halisi yalipofupishwa) Ni ishara gani ya asili ilionyesha kuwa kurudi kwa yesu kulikuwa karibu? Math 24:29-30, Marko 13.24 - 26, Uf 6:12- 13.**

---

---

**b. Chunguza unabii huu wa moja kwa moja kutokana na kumbukumbu za mwongozo wa Roho mtakatifu na historia, jambo gani lilitokea hapo kwanza? Ufunuo 6:12**

---

---

"Katika utimilifu wa unabii huu ulitokea mnamo mwaka wa 1755, Tetemeko la kutisha sana ambalo limewahi kuwepo kama kumbukumbu . Ingawa kwa kawaida linafahamika kama tetemeko la Lisbon [Ureno], Lilienea katika sehemu kubwa ulaya, Afrika, na Amerika [Marekani]. Lilifika hadi Greenland, India ya Magharibi, lilienea kwa zaidi ya maili million nne zenye usawa" – Pambano Kuu uk 304.

**c. Unabii wa kuhusiana na jua na mwezi ulitimilika kwa namna gani? Marko 13:24**

---

---

Siku au miaka 1260 zilikoma mwaka 1798 robo ya mwanzoni mwa karne, mateso yalikuwa yamekoma pote . Kufuatia mateso na kulingana na maneno ya kristo, ju lilikuwa limetiwa giza - 1 bid ukr 306

"Tarehe 19 mwezi wa tano mwaka 1780 historia husimama kama siku ya giza duniani"tangu Nyakati za Musa hakuna kipindi cha giza la kiasi hicho. Uwiano, na muda ambao daima [ umesharekodiwa ] [umeshawekwa kumbukumbu] ya maelezo ya tukio hili, kama yalivyotolewa kwa ushahidi wa aliyeona kwa macho, lakini ni kwa mwangwi wa maneno ya Bwana ...Jua litatiwa giza, na mwezi kuwa damu kabla haijaja hiyo siku kuu itishayo ya Bwana" [ Yoel 2.31 ] - Ibid ukr 308 .

**d. Unabii wa Nyota ulitimilika kwa namna gani? Marko 13:15, Ufunuo 6:13.**

---

[Ufunuo 6: 13] imenukuliwa, Unabii huu ulitiwa chapa na utimilifu wa kuvutia katika manyunyu makubwa ya vimondo vya Tarehe 13 Novemba 1833, Hayo yalikuwa maajabu ya kina zaidi kuonekana kuanguka kwa nyota amabazo daima zimekuwa kumbukumbu" Ibid ukr 333.

## *Alhamisi* *Tarehe 06 Julai*

### 5. KUANDALIWA KWA AJILI YA KUPATA NGUVU

**a. Zaidi ya hayo matukio matatu ya asili aliyoyatoa Yesu kama dalili za kurudi kwake upesi, hebu elezea jinsi zinavyotimia kwa upesi zaidi na zaidi . Mathayo 24:6 -12. Marko 13:7 - 9, Luka 21. 9 – 11, 25 – 27.**

---

**b. Katika kuziangalia dalili hizi tungekumbuka jambo gani? Luka 17: 26 Yeremia 8:11 - 12**

---

"Tetemeko la Ardhi, Majanga, Mafuriko, Maafa nchi kavu na baharini yataongezeka . Mungu anatazama katika ulimwengu wa leo kama alivyoangalia juu ya ulimwengu Nyakati za Nuhu. Anatuma ujumbe wake kwa watu wake siku hizi, kama alivyotuma katika siku za Nuhu. Katika kizazi hiki cha ulimwengu kabla ya mafuriko"" *The Advocate,* 01 Desemba 1900.

**c. Kwa nini tunaweza kutiwa moyo na unabii unaokuwa umetumia? 1 Samweli 12:16, 1Petro 2:9.**

---

---

"Wale ambao walikubali kupokea mafundisho ya marejesho waliamushwa katika umuhimu wa toba na unyenyekevu mbele za Mungu. Wengi kwa muda mrefu wamekuwa wakisimama kati ya kristo na ulimwengu, sasa waliona kwamba ulikuwa ni wakati wa kuchukua msimamo. Mambo ya umilele yalisadikiwa nao kuwa ni ukweli usio wa kawaida . Mbingu ililetwa karibu na walijiona wenyewe kuwa wenye hatia mbele za Mungu... Wakristo walifufuliwa katika maisha mapya ya kiroho . Walifanywa waone kwamba mda ulikuwa mfupi na kwamba kile wanachopaswa kufanya kwa ajili ya wanadamu wenzao ni lazima kifanywe haraka" - *Pambano kuu* ukr 340

## *Ijumaa* *Tarehe 07 Julai.*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI

1. **Katika mwaka 70 AD, kwa nini Mungu aliruhusu maangamizi ya hekalu kuu?**
2. **Kwa nini mtu aliyekuwa peke yake alitangaza ole wa Yerusalemu?**
3. **Tuwezaje kujua kwamba siku katika unabii ni sawasawa mwaka?**
4. **Taja tarehe za dalili kuu tatu za kurudi kwa yesu upesi**
5. **Kadri navyoona badili zilitumia, ni nguvu gani ningeiruhusu ije juu yangu?**

# Ujumbe wa Onyo kwa Ajili ya Siku zetu.

**"Kama Bwana wa majeshi asingalituachia mabaki machache sana Tunagalikuwa kama Sodoma, Tungalifanana na Gomora [Isaya 1.9]**

"Sauti ya Mungu inasikika katika ujumbe wa Onyo, anawaagiza watu wake wajitenge wenyewe kwenye wimbi la uovu" - *Wazee na Manabii* uk 166

**Imependekezwa kujifunza :** *Pambano* kuu - 270

*Wazee na manabii* 156- 170.

## *Jumapili* Tarehe 09 Julai

### 1. KATIKA NYAKATI TUNAZOISHI

**a. wakati gani katika histpria ya ulimwengu Yesu aliulinganisha na wakati wetu ? Mthayo 24: 37- 39, Mwanzo 6: 5, 13**

"Dhambi ile iliyopo katika ulimwengu wetu ni ileile ambayo ilileta ghadhabu ya Mungu katika ulimwengu wa Nuhu. Wanaume na wanawake sasa wanaendeleza kula kwao na kunywa kwa ulafi na ulevi . Dhambi hii inaenea, maovu ya kuendekeza na kujiachia juu ya hamu ya chakula potofu, ilichochea Uchu wa watu katika siku za Nuhu na kuwaongoza katika uharibifu mkuu, hadi hapo jeuri yao ilipofika na kurundikana juu mbinguni, na Mungu alisafirisha dunia na mchafuko wake wa maadili kwa mafuriko" - *Shuhuda ya 3* uk 168.

**b. Waumini wafanyeje kuzibariki siku hizi? 2 Petro 3.3 -6**

"Ulimwengu umejaa maandamano, umejaa anasa za Upagani, unalala usingizi katika usalama wa kimwili. Watu wameweka mbali tukio la ujio wa Bwana, wanacheka na kupuuza maonyo -"- *Tumaini la vizazi vyote* ukr 635.

## 2. JIFUNZE KUTOKA KATIKA TUKIO LA KUSHANGAZA

**a. Linganisha tena siku hizi za mwisho na nyakati za Nuhu, kwanini eneo lingine la matukio yaliyotokea Bwana analinganisha na saa ya kurudi kwake? Luka 17: 28**

---

"Hali ya ulimwengu wa leo ni sawa na ule ambao ulikuwepo kipindi cha Lutu, Ambapo maovu ya Sodoma yaliita malaika wageni kwenda katika mji huo muovu, ili kuona kilio kinachoinuka mbele za Mungu wa Mbinguni kilikuwa kama tabia ya wakazi wa Sodoma nzuri - Mji ambao umekuwa ukipendelewa sana na Mungu kwa hali ya juu - ulikuwa umeharibu njia zake mbele za Bwana, ambapo hapakuwepo na tumaini la ukombozi tena. Gadhabu ya Mungu ilikuwa imefunuliwa kwa maana viashiria vya maonyo ya Sodoma yalikuwa yamezidi mno" - *Southern Union workr* 16, October 1913.

**b. Dhambi gani iliyokuwa marufu katika siku za Luthu . Rumi 1:21, 26 - 27**

---

"Watu wa Sodoma walizongazonga nyumba ya Lutu na kadri walivyozidi kusongamana na kuongezeka, maneno ya uovu yalisikika ambayo yalifanya kuifunua hali yao ya uovu iliyokuwepo miongoni mwa watu. Mapendekezo mabaya yalipokelewa na kutendwa . Umati mkubwa ukawa na ghasia na makelele zaidi katika madai yao kwamba Lutu awalete wageni mbele yao kwa hiyo walikuwa wamegeuka kuwa chanzo na chimbuko kupitia kuendekeza mivuto ya uovu, kwamba kila wazo jema lilikuwa linapuuzwa na kung'olewa. Hivyo basi kwa sababu kamili hiyo wangeweza hata kufanya vurugu kwa malaika wa mbinguni" - *Alama za Nyakati*, 09, October s 1893

**c. Kwa nini Hatima ya Sodoma ni Onyo kwa wote? Mwanzo 19 :24 - 26 Luka 17:32 -33.**

---

"Malaika walikuwa wamekuja kunagalia waone kama kuna yeyote katika mji amabaye alikuwa hana uovu na wangemsihi kukimbia maangamizi amabyo yaliitisha sodoma. Kwamba usiku wa watenda maovu uliongeza tone la uovu katika kikombe cha Uovu wao, ambapo ghadhabu ya Mungu isingeweza kuvumilia kuchelewa - Ibid

"Onyo ambalo lilitolewa katika siku za Luthu, Hutuijia tena sisi ambao wanaishi katika kizazi hiki kilichobarikiwa - jiponye nafsi" Sauti ya Adui inasikika ikisema Amani na usalama . Mwovu mmoja ungejisikia kuwa huna woga wowote, na ule, unywe na kuona na uolewa . Hiyo sauti unayoisikia ni sauti ya mbinguni au ni sauti amabyo hukuonga kwenda kwenye uharibifu? - Ibid 16, Octoba 1893

## 3. KUWA MTENDAKAZI BORA WA MAISHA YETU

**a. Onyo gani limetolewa kuhusiana na hali ya kiroho kushuka kiroho kwa Sodoma? Ezekiel 16: 49.**

---

---

"Wengi wa wale ambao kwa mda mrefu wamekataaa uongozi wa kimbingu na Ulinzi, wanaharakisha kwenda katika njia ya msongamano na anasa binafsi, Naam! Zaidi, kwenye fikra potofu na uchafu wa mwili na ujasiri. Kutokana na akili zao kuchafuliwa, dini kwao ni chukizo. Baadhi wamekwenda mbali zaidi katika jambo hili, na kwa bidii kabisa wanafuta njia ya Sodoma ambayo kila siku wanapiga hatua kuifikia laana ambapo sauti ya onyo na karipio inapotea juu yao" - *shuhuda ya 5* ukr 39

**b. Tunakuwa na hali gani kwa hao tuliopewa nuru kuu na kuonywa juu ya uharibifu mkuu hoaswa kuliko ule wa sodoma ? Hosea 4:6 Mithari 1:24-30, 33**

---

---

"Mkombozi wa ulimwengu Rafiki wa watu mwenye huruma, hufichua mbele za macho yetu ukweli kwamba kuna dhambi nyingi kubwa kuliko dhambi za Sodoma. Dhambi ni ile ya kuipinga nuru kuu . Wale ambao wamesikia lakini hawasikii mwaliko wa kutubu wa injili na kuwa na Imani katika kristo, dhambi yao ni kubwa zaidi kuliko iliyokuwa dhambi ya Sodoma. Kwa wale ambao wamekiri jina la Yesu, ambao wameshuhudia kumjua Mungu na kuzitunza amri zake, lakini bado wameshindwa kumwakilisha kristo katika tabia na maisha yao ya kila siku wameonywa na kukemewa, lakini bado wamepuuza mwokozi wao kwa maisha yao yasiyotakasika. Dhambi yao ni kubwa kuliko dhambi ya Sodoma - *Alama za Nyakati* 16 octoba 1893 .

"Wengi ambao wamekili kuamini ukweli na hawamtaki Mungu katika fikra zao wengi wao wanatenda Usodoma. Mmoja mwenye Busara za kutafakari neno la Mungu aamshwe na Roho Mtakatifu na angeteka mipango yake yote. Ubinafsi, ubinafsi, ubinafsi umekuwa miungu yao, mwanzo na mwisho wao Alfa na Omega" - *Mashauri juu ya watendakaz*i ukr 141

"Dhambi ya Sodoma inajirudia tena katika siku zetu, Dunia inaangamia ina haribika na imechafuka chini ya wakaazi wake. Lakini kipengere cha uovu wa leo ni kujifanya wema mfano wa utauwa pasipo kuwa na nguvu zake . Wale wanaojidai kuwa na Nuru kubwa, wamo miongoni mwa wasiojali watu wa tofauti, na wanasababisha kumjeruhi kristo katika nyumba ya kuwashuhudia" - *Alama za Nyakati* 16 Octoba 1893 .

## 4. KUCHAGUA VIPAUMBELE BORA

**a. Kwa kuepuka makosa ya Luthu ambayo yaliiongeza familia yake katika njia ya hali ya chini, Ni jambo gani lazima tulitambue? Mwanzo 13:12-13; 19:30 – 38; 1Wakor 15:33.**

---

---

---

"Uovu wa Sodoma katika kuvunja Amri za Mungu ulidhihirika wazi hasa katika uasherati - *Pambano kuu* ukr 269 .

Wakati Luthu alipoingia Sodoma alidhamiria kujiweka huru dhidi ya uovu na kuamuru familia yake kumfuata yeye . Lakini hakufaulu alishindwa mivuto michafu iliyokuwepo iliathiri mpaka imani yake mwenyewe, muunganiko wa watoto wake na wakaazi wa Sodoma uliwafunga kiasi fulani yeye na wao, Matokeo yake tunayajua .

"Bado wengi wanafanya kosa hilo hilo, katika kuchagua maeneo ya kusihi yanaonekana yana faida ya muda wanayoweza kuipata, kuliko katika eneo lenye mivuto ya maadili mema yatakayo wazunguka wao na familia zao, wanachagua nchi nzuri iliyo na rutuba au kwenda katika miji inayopendeza zaidi kwa kutumaini kupata mafanikio, lakini watoto wao wanazungukwa na majaribu, na mara nyingi hutengeneza muunganiko usiofaa katika kukuza imani na kuendeleza maadili mema. Mazingira yasiyo na Nidhamu ya maadili ya kutoamini, yenye utofauti katika mambo ya dini yenye tabia ya kupingana na wazazi. Vielelezo vya uasi dhidi ya wazazi na mamlaka ya mbingu mara zote ipo kwa vijana, wengi hujiunga na wasioamini na wanakuwa katika upande wa maadui wa Mungu .

"Katika kuchagua mahali pa kuishi, Mungu angependa tufikirie jambo moja muhimu, mivuto ya kiroho na kimaadili itakayo tuzunguka sisi na familia zetu, tunaweza kuwa tumewekwa katika nafasi palipo na majaribu, maana wengi hawawezi kuwa katika mazingira w anayopaswa kuwa . Wakati majukumu yanapokuja kwetu, Mungu atatuwezesha kusimama bila kuchafuliwa, kama tutakesha na kuomba na tukimtegemea yeye katika Rehema za kristo . Lakini hatupaswi kujiweka wenyewe katika mivuto amabayo haifai katika kujenga tabia ya kikirsto. Wakati tunapojiweka wenyewe kwa hiari yetu wenyewe katika mazingira ya kiulimwengu na kutoamini, hatumpendezi Mungu pia tunawafundisha malaika na kuwaongoza watoke katika nyumba zetu" – *Wazee na Manabii* ukr 168, 169

## *Alhamisi* — *Tarehe 13 Julai*

## 5. CHAGUA SEHEMU SALAMA

**a. Mungu husemaje kuhusiana na mahali gani watu wake wanaweza kunufaika? Isaya 32:18-19**

---

"Onyo langu ni hili : Tokeni Mijini, msijenge vituo vya tiba asili mijini, waelimisheni watu wetu watoke mijini katika nchi zao. Mahali ambapo wanaweza kupata kipande kidogo cha ardhi, na kupafanya nyumbani kwao na watoto wao. . .

"Migahawa zetu lazima ziwe Mijini kwa maana tofauti na hapo watendakazi wetu katika migahawa hizi wasingeweza kuwafikia watu na kuwafundisha kanuni za Nuru iliyo hai. Na kwa wakati huo tutatumia nyumba za mjini kufanyia mikutano . Lakini kabla ya kuwafikia kwa mda mrefu kutakuwa na ugomvi, mabishano, vita na machafuko katika miji ambapo wale ambao- watataka kuiacha miji yao hawatakuwa na uwezo" - *The General conference Bulletin* April 16.

"Wazazi waweze kupata nyumba ndogo katika nchi pamoja na Ardhi kwa ajili ya kilimo mahali ambapo wataweza kuwa na bustani na wanaweza kupata mbogamboga na matunda kiasi kwa ajili ya kuchukua nafasi ya nyama ambayo inachafua uhai wa damu unaotiririka katika mishipa kwenye sehemu kama hizo. [vjijini] watoto hawatazungukwa na mivuto miovu ya maisha ya mjini. Mungu saidia watu wako waweze kupata makao nje ya miji" - *Huduma za Utabibu,* uk 310 .

**b. Kwanini ni lazima kujali maombi kwa ajili ya nchi tunamoishi? Mithali 15:31-32.**

---

"Kulikuwepo na hali ya kutoka nje, mtengano wa kujitenga na wimbi la waovu ili kuokoa maisha, Kama vile ilivyokuwa katika siku za Nuhu, Na siku Lutu, hali kadharika katika siku za Mitume na kabla ya angamizo la Yerusalemu ndivyo itakavyokuwa katika siku za mwisho" - *Wazee na Manabi* uk 166.

## *Ijumaa* — *Tarehe 14 Julai.*

## MASWALI BINAFASI YA KUTAFAKARI

1. **Katika kuwakabiri wanaokebehi marejeo ya kristo, jambo gani tunapaswa kulitunza katika akili?**
2. **Kwa nini tunahitaji kuamushwa wote na historia ya Sodoma na Gomora?**
3. **Kwa watu wa Mungu kungekuwa na gatima ya athari gani kung'ang'ania mjini?**
4. **Je, niko katika hatari ya kurudia makosa ya Lutu? kama ni hivyo, je nifanyeje?**
5. **Kuna faida gani ya kuishi ?**

# Imani potofu katik siku za mwisho

**Kwa maana watatokea Makristo wa uongo na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kuu na maajabu, wapate kuwa(danganya) kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. (Mathayo 24:24)**

Kuna uzushi wa uongo wa hatari ambao utawasilishwa kama mafundisho ya Biblia, Tunatakiwa kuwa na ufahamu wa Biblia ili kwamba tuweze kujua jinsi ya kukutana nao, Imani ya kila mmoja itajaribiwa. - *Uinjilisti* uk 590, 591.

**Imependekezwa kujifunza: Manabii na Wafalme uk r 210-212**

## *Jumapili* *Tarehe 16 julai*

### 1. UANGALIFU NA UMAKINI UNAHITAJIKA

**a. Ni mkakati gani wa Adui wa Roho huutumia ili kuzishawishi Roho nyingi za kweli ambazo zinaamini Marejeo ya Yesu kwa upesi ? Mathayo24:11, 24**

---

″Malaika wa shetani wana busara ktk kutenda uovu, Na watafanya kile ambacho baadhi watadai kuwa ni mwendelezo wa Nuru na kuitangaza kuwa ni mpya na ajabu. Na bado ktk kipindi Fulani na maeneo Fulani inaweza kuheshimiwa kuwa ni ujumbe wa kweli. Nuru hii itakuwa imechanganyikana na uvumbuzi wa kibinadamu, Na kufundisha mafundisho yaliyo

Maagizo ya wanadamu. Hakina kama tungalikuwa na wakati wa kuke sha na kuomba siku zote kwa bidii ya kweli, Ni sasa. Mengi yanaonekana kuwa mambo mazuri, itahitajika kuwa na uangalifu pamoja na kuzingatia maombi mengi. Kwa maana wana madanganyo maalum nayapeke yake ya Adui, kuziongoza nafsi ktk njia ambayo uongo umefungwa na kuwekwa Ktk njia ya kweli ambapo ni vigumu kuutofautisha″ - *Uinjilisti* ukr 590.

″Ushuhuda wa Roho wa Mungu, ni ukweli. Imani yako haibadilishwi kwa mafundisho yoyete ya mkupuo, hatakama yanaweza kuonekana ni matamu ya kupendeza, ambayo yataipotosha nafsi.

″Udanganyifu na Madanganyo ya shetani kwa sasa yanakuwa yakizidi, Na kwa wale ambao wameacha na wamejitenga na njia ya kweli watapoteza kinga zao na ulinzi. Hawana kitu chochote kwenye ile Nanga. Watakuwa wamechukuliwa na kupeperushwa kutoka ktk danganyo moja hadi jingine ivume juu upepo wa mafundisho ya ajabu. Shetani amewakandamiza kwa nguvu iliyo kuu.“ Ibid ukr 362.

## 2. MADANGANYO HATARI.

**a. Elezea hila zenye uelevu zinazotumiwa na Adui mdanganyifu wa Mungu kama alivyofanya udanganyifu ktk siku za Musa-Na kujirudia siku hizi. Kutoka 7:10-13**

''Wachawi. . . , walionyesha ishara na maajabu, nao pia hawakutumia nguvu zao peke yao, bali nguvu za miungu yao. Ni shetani aliyekukuwa akiwasaidia kuingiza kwa kuipotosha kazi ya yehova.

''Wachawi hawakugeuza fimbo zao kuwa nyoka kabisa, bali kwa uchawi. Wakisaidiwa na mdanganyifu mkuu ndipo walipoweza kutoa mwonekano huo. Ilikuwa ni zaidi ya nguvu za shetani kubadili fimbo hizo kuwa nyoka walio hai. Mkuu wa uovu ingawa anayo hekma na uwezo wote wa malaika aliyeanguka, lakini hana uwezo wa kuimba, au kutoa uzima, hii ni haki ya miungu pekee lakini yote yalikuwa ktk uwezo na Nguvu za Kutendwa na shetani, aliyatenda na aliendelea kutenda Miujiza. Mbele za wanadamu fimbo zilibadilika na kuwa nyoka. Hivyo wakaamini kuwa ni Nyoka wa Farao na Ikulu yake.“ – *Wazee na manabii* ukr 264.

**b. Kwa nini udanganyifu na uongo ni uadui wa Nafsi unaotumika hivi sasa?Ufunuo 13.13.**

''Watu wanadanganywa kwa miujiza na maajabu ambayo mawakala wa shetani wana uwezo wa kuitenda, wala siyo kwa ile wanayojifanya kuitenda'' *Pambano kuu* ukr 533.

**c. Pamoja na onyo gani kristo alitabiri kutokea?Mathayo 24:25-26**

''Je, Maelfu hawajatoka kwenda jangwani, wakitumaini Kristo kumpata huko? Na kutoka maelfu ya makutano ambapo watu wanatangaza kushikilia muungano pamoja na Roho (Zilizokufa)za wafu, je hatusikii wito sasa ukisikika"Tazameni yumo ndani?Haya ni madai makubwa sana ambayo umizimu huyaweka mbele'' -*Tumaini la vizazi vyote*, 631

**d. Kadri tunavyoona na utabiri dhidi ya hila za mazingaombwe ya Roho ya Umizimu ukitimia ulimwenguni, je ni jambo gani lazima tulitambue? Efeso 6:11-12**

**3. MIUJIZA NA MAAJABU YA KWELI.**

**a. Kadri mwisho ukaribiavyo, Ni onyo gani muhimu limetolewa kwetu linalozuia kuamini ktk ishara na maajabu, Na kwanini? Mathayo 24:4-5 11, 24-25.**

---

″Kadri watu wa Mungu wanapoisogalea hatari ya siku za mwisho, shetani naye hushikilia kwa juhudi mashauriano pamoja na malaika zake kadri wanavyoweza kufanikisha mpango wa kuangamiza imani zao. Huyaangalia makanisa maarufu yale ambayo yamenashwa kwenye usingizi na uwezo wa nguvu za madanganyo yake. Kwa udanganyifu wa kuvutia na miujiza ya uongo ameweza kuwashikilia chini ya uongozi wake. Kwa hiyo anawaagiza malaika zake watandaze mitego yao hasa kwa wale am bao wanatazamia marejeo ya kristo na wanaohitaji kutii amri zote za Mungu.

″Tumeonywa kwamba ktk siku za mwisho shetani atafanya kazi kwa ishara kuu na maajabu. Na ataendeleza maajabu haya na miujiza hadi kufungwa kwa pambano, ili kwamba aweze kuwaonesha yeye ni malaika wa Nuru na siyo malaika wa giza″...

“Baadhi watajaribiwa ili kupokea miujiza na maajabu haya. Wagonjwa watakuwa wakiponywa mbele yetu. Je umejiandaaje kwa ajili ya jaribu linalotusubiri sisi wakati wa miujiza na maajabu ya uongo itakapokuwa imedhihirishwa kikamilifu zaidi? Je si Nafsi nyingi zitakazo naswa na kuchukuliwa? Kwakujitenga na Kanuni zilizo wazi, na Amri za Mungu, na kusikiliza hadithi, na mawazo ya watu wengi, ni Maandalizi ya kupokea miujiza na maajabu ya uongo. Italazimu wote sasa kutafuta silaha yetu wenyewe kwa ajili ya shindano ambalo ni lazima kushiriki. Uaminifu ktk Neno la Mungu, Kusoma sana na kuomba, kufunga kivitendo, hii itakuwa ngao yetu na kimbilio letu dhidi ya mwovu shetani, nguvu itakayo tuletea ushindi kupitia damu ya Kristo″- *Maranatha* ukr 208.

**b. Kwa nini tunahitajika kuitambua moja ya hila za shetani anazotumia? 2Thesalonike 2:9-12 Muhubiri 9:5-6**

---

---

″Shetani anao uwezo wa kuleta mbele ya watu sura na mwonekano wa marafiki zao waliokufa. kwa mfano halisi kabisa sura iliyowazi kabisa, maneno na jinsi alivyokuwa akiongea(Lafudhi yake)vyote vinatolewa kwa uwazi usio na tofauti. Wengi wanafarijika kwa kuwa na uhakika kwamba wapendwa wao wanafurahia raha ya mbinguni na bila kudhania kuwa kuna hatari wanatega sikio″kwa Roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani (1 Thimoth 4:1)″ -*Pambano kuu* ukr 552.

## 4. EPUKA TARATIBU RAHISI, ZA BANDIA

**a. Kwa namna gani mahubiri ya Nuhu yanahusiana Nasi, kadri tunavyo hubiri ukweli wa leo-pamoja na Nuru iliyoaminiwa ya Afya?Luka 17:26-27; 1 Petro 2.11.**

"Nuhu alihubiri kwa watu wa wakati wake kwamba Mungu angetoa kwao miaka mia moja na ishirini ktk hiyo watubu dhambi zao na watafute kimbilio ndani ya safina, Lakini walikataa mwaliko wa thamani……. . . mda mrefu ulikuwa umetolewa kwao ili waonekane na uovu na dhambi zao waachane na mazoea yao mabaya waiendeleze tabia njema ya haki, lakini waliipendelea dhambi. hata hivyo udhaifu wa wengi mwanzoni uliwaongoza kwenye tamaa ya mara kwa mara waliharakisha kwenda kwenye uharibifu usioelezeka" - *Review and Herald,* 20 octoba 1885.

**b. Badala ya kujitoa sisi katika Taratibu na njia Rahisi nyeupe, kwa nini Mungu ametupa tabia ya kujenga ujumbe wa afya ambao hututaka kuufia ubinafsi? Mathayo 7:13-15**

"Shetani atafanya kazi ya miuji za na maajabu. . Atawafanya watu kuwa wagonjwa kisha kwa ghafla anawaondolea ugonjwa kwa nguvu zake za kishetani kwa baadae wanaonekana kana kwamba wamepona. Matendo haya ya kuponywa kwa wazi yataleta jaribu kwa Waadventista wa Sabato." *Maranatha* ukr 209.

"Njia ambayo Yesu aliifanyia kazi, ilikuwa ni kuhubiri Neno, na kukomesha mateso kwa matendo ya miujiza na uponyaji. Lakini nimeelekezwa na Bwana kwamba hatuwezi sasa kufanya kazi ktk njia hii, kwa maana shetani atatumia uwezo wake na kutenda Miujiza. Watumishi wa Mungu siku hizi hawapaswi kufanya kazi kwa njia ya miujiza, kwa sababu uponyaji wa uongo utadai kuwa Uungu ndio utakuwa umeponyesha.

"Kwa sababu hiyo Bwana ametofautisha njia ambayo watu wake waiweke wazi ya uponyaji kimwili pamoja na mafundisho ya neno, vituo vya tiba asilia vianzishwe (sanitariam). Kwa taasisi hizi zitaunganisha watenda kazi ambao watapeleka mbele kazi ya utume wa matibabu ya asili halisi. Hadi hapo linda mvuto kwa bidii pandezote kwao wale

Ambao wamekuja kwa ajili ya matibabu kwenye sanitarium.

"Huu ni utoaji Bwana ameufanya mahali ambapo kazi ya utume wa injili unafanyika kwa ajili ya nafsi nyingi. Taasisi hizi zianzishwe nje na miji, katika kazi ya kuwafahamisha inauweka wazi ufahamu". . . , *Huduma za matibabu* uk 14.

## *Alhamisi* — *Tarehe 20 Julai*

### 5. MWENYE KUONA HAPASWI KUAMINI

**a. Eleza udanganyifu wa mwisho wa shetani atakaoufanya. 2Wakorintho 11:14**

---

"Kadri Uigizaji unavyozidi kuongezeka ktk maigizo makuu ya udanganifu, Shetani mwenyewe ataonekana kama Kristo. Kanisa kwa mda mrefu limetangaza kutazamia tukio la ujio wa mwokozi kama utimilifu wa matumaini ya kanisa. Sasa mdanganyifu mkuu atafanya ionekane kwamba kristo amekuja ktk sehemu tofauti tofauti duniani. Shetani atajidhihirisha mwenyewe miongoni mwa watu kama mwenye utukufu na mng'ao wa kustaajabisha, akifanana na maelezo ya mwana wa Mungu aliyoyatoa kwa Yohana ktk ufunuo. Ufunuo 1.13-15. Utukufu wake uliomzunguka hauna kifani, kitu chochote chenye macho ya kufikwa na mauti, bado hakijawahi kuutazama . \Kelele za ushindi huita juu ya anga "Kristo amekuja, kristo amekuja" watu wanajinyenyekeza na kuabudu mbele zake {Shetani}, wakati huo mikono yake inainuliwa juu na kutangaza baraka juu yao, kama vile kristo alivyowabariki wanafunzi wake wakati alipokuwa hapa duniani. Sauti yake nyororo, tulivu iliyojaa mziki mtamu, kwa upole, anaita kwa huruma kama vile thamani ya Neema ya kimbingu ya kweli ambayo mwokozi alitamka. Aliponya magonjwa ya watu, kisha ktk kuichukua kwake tabia ya kristo, Anadai kuwa na badiliko la sabato kuhamishiwa jumapili na Amri zote zimeruhusu siku ambayo yeye ameibariki. Na anatangaza kuwa wale wote ambao wanaendelea kuitakasa siku ya saba(jumamosi)wanakufuru jina lake kwa kukataa kuwasikiliza malaika aliowatuma kwao pamoja na Nuru na ukweli. Hili ni nguvu kubwa ni zaidi ya udanganyifu wote" *Maranatha* ukr276.

**b. Katika kuitambua hatari kama hiyo, kwa nini lazima kuwa na mtazamo wetu? 2wakorintho 4:8-10, 18.**

## *Ijumaa* — *Tarehe 21 Julai*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAKARI.

**1. Kwa nini ni muhimu zaidi kuwasilisha ukweli wa mafundisho ya Biblia ktk nyakati za mwisho?**

**2. Kwa jinsi gani tunaweza kuelezea kutokea kwa maajabu ya uchawi wa Farao?**

**3. Baadhi ya majina ya hila maalum za mdanganyifu mkuu huwalenga masalio wa Mungu.**

**4. Kama kanuni kwa ujumla kwa nini sisi haturuhusiwi kutarajia uponyaji wa popo hapo siku hizi?**

**5: Kwa namna gani tunaweza kutambua kuja kwa Yesu kristo upesi ambapo ni ujio wa bandia?**

# Hakika Yesu anakuja tena.

**"Nitakuja tena ninawakaribishe kwangu ili pale nilipo mimi nanyi muwepo [Yohana 14: 3]**

"Moja ya ukweli Muhimu sana na wenye utukufu mkuu kabisa ulifunuliwa katika biblia, ni le wa uja kwa kristo mara ya pili kw aajili ya kukamilisha kazi kuu ya ukombozi"oambano kuu ukr 299 .

**Imependekzwa kujifunza . Maandiko ya awali ukr 13-18, 285-286.**

## *Jumapili* *Tarehe 23 Julai*

### 1. TAZAMA, YUAJA!

**a. Kulingana na Biblia kuja kwake Yesu atakuja kwa jinsi gani? Matendo 1.11**

"Ukweli wa thamani zaidi kwa wanafunzi katika kupaa kwa Yesu ulikuwa ni kwamba, aliwaacha kwenda Mbinguni kwa namna iliyowazi tena dhahiri mwalimu wao wa kimbingu. Yesu yule Yule amabye alikuwa akitembea, akiongea na kuomba pamoja nao, amabye aliumega mkate pamoja nao, ambaye alikuwa pamoja nao katika mashie juu ya maji naamabye waliomba pamoja naye mashamba ...alipaa kwenda Mbinguni katika umbo l Kibinadamu. Wajumbe wa kimbingu walikuwa wamewahakikishia kuwa, Yesu yuleyule ambaye walimwona akipaa juu kwenda Mbinguni, wangemuona tena katika namna ileile kama alivyopaa. Uthibitisho na uhakika huu umekuwepo daima, na utakuwapo hadi mwisho wa wakati. Tumaini na furaha la wote wapenda ukweli wa kristo, - *Roho ya unabii* vol 3 ukr 254

**b. Kwa akina nani Yesu atajidhihirisha Kwa uwazi wazi? Ufunuo 1:7 24: 30**

"Wale wote ambao walimdhihaki na kumpiga wakiwepo wale viongozi wa dini na makuhani watalitazama tena mara ya pili eneo la tukio katika kuta za hukumu. Kila jambo litawekwa wazi mbele zao kama limeandikwa kwa herufi za moto, kisha waliomba" damu yake naiwe juu yetu na watoto wetu, watapokea jibu la maombi yao. Ndipo dunia nzima itajua na kufahamu"-*Tumaini la vizazi vyote* uk 739, 740 .

## 2. TUMAINI LA AJABU

**a. Kusudi la kuja kwa Yesu ni lipi kwa namna gani tunapaswa kushangazwa Katika hili, kuzidi tukio linalotuathiri sisi? Yohana 14: 1- 3**

---

---

"Wale amabo hawawezi kumpenda Mwokozi kwa dhati lakini wingi wa furaha na ujumbe uliwekwa juu ya neno la Mungu, yeye Yule ambaye matumaini yao ya uzima wa milele yamewekwa yuaja tena, si kwa kutukanwa, si kwa kudharauliwa, wala kwa kukataliwa kama ilivyokuwa katika ujio w ake wa kwanza, bali sasa anakuja katika nguvu na utukufu ili kuwakomboa watu wake. Tangazo la kurudi kwa Yesu linapaswa kutangazwa kama ililivyofanywa wakati ule na malaika kwa wachungaji wa Kondoo wa Bethelehemu, ni habari njema yenye furaha kuu, Haiwezekani kuwa na ushahidi thabiti zaidi kwamba makanisa yamejitenga na kukengeuka kutoka kwa Mungu kwa uchunguzi kuliko na kujenga msisimuko wa Uadui kwa ujumbe huu uliotumwa kutoka mbinguni.

"Ni kwa wale tu ambao hawana upendo na mwokozi w anaotumaini asirudi akae mbali kwa bidii wanapokea ushuhuda mchafu kama vile mtumwa asiye mwaminifu

"Bwana wangu anakawia kurudi [ Math 24:48 ] wakati wanapokataa kuchunguza na kuyasoma maandiko ili kujifunza, kwamba mambo haya ndiyo yalivyo wao wanafahamu kila simulizi na hadithi za kubuni, ambao zinaliweka pembeni tukio la kuja kwa Yesu katika siku za usoni, kiroho wanafanya utimilifu wa angamizo la Yerusalemu, au kuchukua nafasi katika kifo." *Roho ya unabii* vol 4, ukr 216 - 217

**b. Elezea utamu wa tumaini hili, pamoja na kitu gani kitakuwa uhusiano wa karibu? Filipi 3:20-21.**

---

---

"Kweli za Unabii zimefungwa pamoja na kadri tunavyojifunza kwazo, zinatengeneza nguzo ya uzuri ya matendo ya mkristo. Injili yote tuliyopewa iko wazi kwa ajili ya kufunua kile tunachokingoja, kufanya kazi na kuomba kwa ajili ya ujio wa mwana wa Mungu. Kuja kwake ni tumaini letu. Tumaini hili linakuwa limefungwa pamoja na maneno yetu na matendo yetu, pia pamoja na ushirikiano na mahusiano yetu uinjilisti ukr 220.

"Wale ambao wanampenda na kumgonja yeye kwaajili yake atawavisha taji yenye utukufu, heshima na kutokufa. Wenye haki waliokufa watasimama mbele ya makaburi yao na wale ambao wanaishi kwa pamoja watamlaki Bwana hewani watasikia sauti ya Yesu, ikiwa tamu kuliko sauti ya muziki wowote uliowahi kusikiwa na masikio ya wanaokufa, Akiwaambia, vita vyenu vimekwisha kukamilika". *Matendo ya Mitume* ukr 34.

## 3. UTUKUFU USIOELEZEKA

**a. Ni ishara gani katika mawingu ya Mbinguni itaonyesha kurudi kwa Yesu? Marko 13:26**

---

---

"Mara macho yetu yalikaza kuelekea upande wa mashariki, kulikuwa na wingu dogo jeusi lililoonekana kama Nusu ya kiganja cha mwanadamu ambapo sisi sote tulijua kuwa ile ilikuwa ishara ya wana wa Adamu. Sote tukiwa kimya kabisa tulikaza macho juu ya wingu kadri lilivyozidi kusogea, lilizidi kuwa jeupe, lenye utukufu, na kuendelea kuwa na utukufu zaidi, hadi lilipokuwa wingu kubwa jeupe, kwa chini ya kitako chake lilionekana kama moto ulao na upinde wa mvua ulikiuwa juu yake" - Karama za roho vol. 2 ukr 32

**b. Eleza utukufu wa aina tatu kwenye matejeo ya Yesu - Zingatia pale atakapo kutana na wakombolewa wake. Je, miguu yake itagusa ardhi ajapo mara ya pili? Luka 9:26 [mwishoni] 1Thesolonike 4:16- 17.**

---

"Juu ya wingu ameketi mwana wa Adamu, juu ya kichwa chake alivaa taji za utukufu, nywele zake zilikuwa nyeupe za singa na zilizolala mabegani mwake. Miguu yake ilikuwa na mwonekano kama wa moto, katika mkono wake wa kulia alikuwa na mundu mkali katika mkono wa kushoto alikuwa na Tarumbeta ya rangi ya fedha. Macho yake yalikuwa Kama mwale wa moto ambayo yaliwaangaza watoto wake kila mahali. Ndipo nyuso zote ziling'aa kwa utukufu na wale ambao alimkataa Mungu walifunikwa na giza nene. Kisha tulilia machozi, nani awezaye kusimama? Vazi langu halina Doa? ndipo malaika walikoma kuimba, kukawepo na ukimya wa kutisha . Na kasha Yesu aliposema, ni wale tu ambao ni wasafi wa mikono na mioyo watakaoweza kusimama . Neema yangu inatosha Kwa ajili yao. Wakati huo nyuso zetu zimeelekea juu na kila nafsi ilihisi furaha. Malaika walipiga mziki kwa hali ya juu na kuimba tena wakati wingu likizidi kusogea taratibu duniani . Kisha Tarumbeta la Yesu la rangi ya fedha ilisikika kadri alivyozidi kushuka juu ya wingu akiwa amezingirwa na miale ya moto . Alikaza macho yake juu ya makaburi ya watakatifu waliolala, kisha aliinua macho yake kutazama juu na mikono yae akilia, amkeni, amkeni, amkeni, ninyi mlio lala katika mavumbi ya nchi fufukeni. Kukawepo na tetemeko kubwa. Makauburi yakafunguka wafu wakatoka nje wakiwa wamevikwa kutokufa. wale144, 000 walipiga kelele Haleluya! Kadri walipowatambua marafiki zao walioachanishwa na kifo. Kufumbua na kufumba tulibadilishwa na kwa pamoja tulimlaki Bwana hwani na kuingia ndani ya wingu kwa pamoja" - Ibid uk 32, 33. *Au angalia kitabu cha maandiko ya awali* Uk 17, 18.

**c. Baada ya miaka 1000, kuna utofauti gani wa kuja tena kwa Yesu, ukilinganisha na kuja kwake mara ya pili ? Zakaria 15:4[.**

## 4. YUAJA NA NGUVU NA UWEZA

**a. Nini kitatokea katika asili kwenye tukio la kuja kwa Yesu mara ya pili, na kwa nini? Ufunuo 6:14 Isaya 24:1-6.**

---

---

"Mungu angepata watu wake wenye ufahamu safi ambao watatembea kulingana na utii wao au ukosaji wao. Uovu na magonjwa yanaongezeka kila kizazi mfululizo. Ardhi inatumika chini ya laana ambayo mwanadamu ameileta juu yake kwa sababu ya kuendelea kutotii sheria .

"Mfalme wa wafalme akipaa juu ya mawingu akiwa amezungukwa na kufunikwa katika ndimi za moto ulao. Mbingu zinakunjwa kama ukurasa dunia inatetemeka mbele zake, milima na visiwa vinatoweshwa mahali pake. " - *Pambano kuu* ukr 641, 642.

**b. Kwa namna gani unabii huonyesha hukumu za Uungu ambazo zinaharakisha kuanguka juu ya ulimwengu kwenye ujio wake? Isaya 24:17- 23**

---

"Waovu hulitazama tukio hilo kwa hofu na mshangao, huku wenye haki wakizitazama dalili hizo za kuokolewa kwao kwa furaha kubwa sana. Kila kitu cha asili kinaonekana kuwa kumegeuka kutoka katika hali ya kawaida yake. Mito inakoma kutiririsha maji yake. Mawingu mazito meusi yanatokea na kugongana yenyewe kwa menyewe. Katikati ya mbingu zilizo na hasira kunatokea nafasi na uwazi mmoja wenye utukufu usioelezeka wala kusemeka, ambapo Mungu sauti yake kama maji mengi, inatokea ikisema" *Imekwisha* Uf. 16:17 .

"Sauti hiyo inatetemesha Mbingu na dunia . Linatokea tetemeko la nchi ambalo tangu kuwepo kwa mwanadamu juu ya nchi halijawahi Kutokea kwa namna ile jinsi lilivyo kuwa tetemeko hilo [fungu la 18 ] . Anga linaonekana kufunguka na kujifunga utukufu kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu unaonekana ukimulika ghafla kupitia kwenye uwazi ule. Milima inatetemeka kama tete au nyasi zinazo peperushwa na upeepo, miamba inapasuka pasuka na kutapakaa kila mahalis

Kuna kuwepo na Muungurumu wa ghadhabu ya tufani inayofuatia . Bahari ina chafuka na kusukasuka kwa fujo na ghasia . Kunasikika sauti kali ya msukumo wa kimbuga kama sauti ya mashetani waliotumwa kuangamiza. Dunia yote inavuvuma inatuna na kuvimba kama mawimbi ya bahati . Uso wa Dunia unavunjika vunjika. Misingi yake imara inaonekana kung'olewa . Vilele vya milima vinazama na kutoweshwa. Wakazi wa visiwa wanatoweka. Bandari ambazo zimekuwa kama sodoma kwa uovu zimnamezwa na Hasira ya maji - Ibid ukr 636, 637. *[au Pambano kuu 636, 637 kurasa za ndani].*

## *Alhamisi* *Tarehe 27 Julai*

### 5. UTIMILIFU WA MATUMAINI YALIYODUMU KWA MUDA MREFU

**a. Elezea furaha ya malaika watakatifu pamoja na Yesu kwenye marejeo yake Yuda 1:14**

---

"Nyimbo tamu na mziki mzuri wa malaika watakatifu wengi wasio na idadi, umati mkubwa, wanafuatan na [ Yesu ] katika safari yake . Anga linaonekana limejaa viumbe wenye kung'aa – Elfu kumi mara elfu kumi na maelfu kwa maelfu [ uf 5: 11] . Haipo kalamu ya mwanadamu inayoweza kuandika tukio Hilo, wala haipo akili ya mwanadamu anayekufa inayoweza kufahamu na kutambua mng'aro wa utukufu wake

**b. Ni kazi gani malaika watakatifu wanayofanya [ kulingana na hukumu ya upelelezi ambayo itakuwa imekamilika ] Na hatimaye wakazi wa dunia watatambua nini Mathayo 13:41, 49; 25:32; Rumi 7:12 .**

---

Tarumbeta la malaika mkuu ghafla litawaogofya walio hai na kuwamusha wafu. Katika siku hiyo waovu watatenganisha na wenye haki, kama vile Mchungaji abaguavyo mbuzi kutoka kwenye Kondoo"- *Mwongozo wa watoto* ukr 561 .

"Kristo anayatambua matukio yote ya kutokea tena mara ya pili. Tukio la Hukumu litaonekana kila sayari ilipo na malimwengu yote. Kwa maana katika hukumu hii serikali ya Mungu itakuwa imeithibisha sheria yake kwamba itasimama daima kama Takatifu ya haki na njema [ Rumi 7: 12] . Ndipo kila jambo litakuwa limeamuliwa kauli na usemi utakuwa umepitishwa juu ya kila jambo. Dhambi haitaonekana kupendeza tena, bali itaonekana katika kificho kikubwa, wote wataona uhusiano katika kile walichosimamia kwa Mungu na kwa wengine" - *Review and Herald* 20 septemba, 1898 .

## *Ijumaa* *Tarehe 28 Julai*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKALI

1. **Eleza kundi gani la watu watashuhudia kurudi kwa yesu mara ya pili.**
2. **Kwa nini Yesu, anarudi, kitu gani tunapaswa kuzingatia katika tukio hili?**
3. **Kwa nini tunapaswa ama tusijue, Miguu ya kristo itagusa na kukanyaga ardhi/**
4. **Kutakuwa na mageuzi makubwa kwa jinsi gani katika uumbaji kuhusiana na sheria njema ya Mngu?**
5. **Pamoja na furaha hii bado maasa ya kusifu [ibada] yanendelea, jambo gani tunapaswa kulizingatia kwa undani?.**

**Sadaka ya sabato ya kwanza Ni kwaajili ya shule za utume za miradi ya elimu.**



Kila mwanadamu aliumbwa kwa mfumo wa Mungu amejaliwa Kuwa na nguvu sawa na ile ya muumbaji pekee, nguvu ya Kufikiri na kutenda watu ambao katika nguvu hii anaendelea kuwa mtu aliyebeba majukumu na uwajibikaji, ambao humuongoza katika biashara, na muto wa tabia, ni kazi ya Elimu ya kweli kuendeleza nguvu na uwezo huu, kuwafundisha vijana hadi kuwa wasomi, na siyo kuwa watu wa kuaksi mawazo ya watu wengine……. Badala ya kuwa na Elimu dhaifu isiyofaa, Taasisi za masomo ziweze kuwatuma nje watu wenye nguvu na imara katika kufikiri na kutenda, watu ambao ni waelewa na siyo watumwa wa mazingira na hali ya mambo . Watu wenye upana wa akili, usafi wa mawazo, na ujasiri wa nia zao. - *Elimu* ukr 17, 18 .

Ni kusudi la idara ya Elimu kusaidia kuimalisha taasisi kama hizo. Shule kwa ajili ya Elimu kwa ujumla na shule za utume zinahitajika kwa sasa zaidi kuliko ilivyokuwa zamani kwa ajili ya kuwaelimisha watoto wetu. Zaidi ya karne zilipita mjumbe wa Mungu aliandika, Inaweza kufanyika zaidi kuokoa na kuwaelimisha watoto wa wale ambao kwa sasa hawawezi kutoka mijini. Hili ni jambo la thamani la juhudi zetu bora. Shule za kanisa zianzishwe kwa ajili ya watoto katika miji, Na katika kuhusiana na shule hizi utoaji ufanyike kwa ajili ya mafundisho ya kiwango cha juu, mahali ambao wameenda. *Mwongozo wa watoto* ukr 306.

"Popote halipo na watunza sababto wachache, wazazi w angeungana na kushirikiana kutoa sehemu ya shule ya kutwa mahali ambapo vijana na watoto wao wangeweza kufundishwa na kuelimishwa, wanapaswa kumwajiri malimu mkristo ambaye kadri anavyokuwa mmisionari mwenye wakfu atawaelimisha watoto katika njia ile ipasayo na kuwaongoza kuwa wamishonari [ watume ]. . . ,

"Iwapo wazazi watatambua umuhimu wa vituo hivi vya elimu hizi ndogo, kushiriki kutenda kazi ambayo Bwana hutamani waifanye katika wkaati huu, mipango ya Adamu kwa watoto wetu itakuwa imechanganyikiwa nay a kukatisha tama .

Tunakuomba sabato hii toa Kwa ukarimu ili kusaidia kazi hii

Tunawaomba sabato hii toeni kwa wema na ukarimu kwa ajili ya kusaidia kazi hii katika makanisa yetu yote duniani kote.

*Ni ndugu zenu kutoka Idara ya Elimu [G C] Baraza kuu .*

# Akija Kwa Nguvu nyingi na Utukufu Mkuu

**Katika siku hiyo watasema tazama huyu ndiye Mungu wetu, ndiye tuliyemngoja atusaidie, Huyu ndiye Bwana tuliye mngoja, na tushangilie na kufurahia wokovu wake. [Isaya 29: 9]**

"Mawingu mazito meusi yenye hasira kali yaliyofunika anga yakatengana, na kama alivyyofanya stephano [mtu wa Mungu] wakatazama mbinguni kwa uaminifu na kuona utukufu wa Mungu na mwana wa Adamu ameketi juu ya kiti cha enzi - *Pambano kuu* uk 636 .

**Imependekezwa kujifunza: pambano kuu ukr 479, 484, 641, 645.**

## *Jumapili* *Tarehe 30 Julai*

### 1. HUZUNI, HUZUNI, HUZUNI YA AJABU .

**a. Kipindi Yesu anaporejea mwitikio gani wa Ajabu unakuwepo juu ya wale ambao wamepuuza na kudharau kafara yake ya wokovu? [ Ufunuo 6: 15 -17 Nahum 2.10 .**

---

---

"Wale waiokataa Rehema za Mungu huanguka katika hofu ya kukata tamaa milele" - Pambano kuu ukar 64

"Wakati wenye dhambi wanapolazimika kutazama juu yake Yeye ambaye amevaa Uungu Pamoja na Ubinadamu, ambaye bado anaendelea kuvalia vazi hii kuu, Hofu, fadhaa kuu na wasiwasi wao hauwezi kuelezeka. Kipimo chao kinaangulka mbele za macho yao na wanaona kile ambacho macho yao hayajawahi kukiona hapo kabla . Sasa wanatambua kile ambacho wangekipata ilikuwa wampokee kristo ili awahakikishie fursa iliyotolewa kwao. Wanaiona sheria ile ambayo waliidharau imeinuliwa juu kama kiti cha enzi cha Mungu kilivyo inuka juu. Wanamwona Mungu mwenyewe akitoa heshima juu ya sheria yake mwenyewe" - *SDA Bible commentary* vol 6. Uk 1069.

**b. Hakika litatokea jambo gani kwao. Na Kwa nini? 2 Thesalonike 1.7 -10; 2.8**

---

---

"Nuru ya utukufu wa Mungu ambayo huwapa uzima wenye haki hawaangamiza na kuwauwa waovu" - *Tumaini la vizazi vyote* uk 108 .

## 2. UFUFUO MAALUMU

**a. Kutoka miongoni mwa wote ambao, kupitia historia walilala kwenye makaburi yao wakimwamini watakuwa wamefufuliwa tayari kabla ya kufika kwa Yesu? Ufunuo 14:12- 13, Daniel 12.1-2.**

"Mawingu Meusi mazito yalitokea na kugongana lakini kulikuwepo na sehemu moja wenye uwazi ulijawa na utukufu, ambapo sauti ya Mungu ilitokea kama sauti ya maji mengi, ikitikisa Mbingu na dunia kulikuwepo na tetemeko kuu la nchi. Makaburi yalifunguliwa, na wale waliokufa katika Imani ya ujumbe wa malaika wa Tatu, wakiitunza sabato, walitoka nje kutoka kwenye vitanda vyao vya mavumbi wakiwa na utukufu wapate kulisikia agano la amani ambalo Mungu alilifanya na wale waazishikao amri zake" -*Maandiko ya Awal*i ukr 285 .

**b. Kina Nani kutoka miongoni mwa waovu watafufuliwa punde kabla ya marejeo ya Yesu? Mathayo 26: 62-64: Ufunuo 1.7.**

"Wale ambao walimcheka na kumkejeli [kristo] aliposema kuwa ni mwana wa Mungu, sasa hawana la kuongea. Herode mwenye kiburi na majivuno alikuwepo aliyezomea cheo chake cha kifalme na kumdhihaki, na kuamrisha maaskari wenye dharau kumtawaza kuwa mfalme. Kuna wale watu ambao kwa mikono yao kabisa isiyo na heshima walimvisha vazi la zambarau na taji ya miiba katika paji lake takatifu la kichwa chake na fimbo ya kifalme ya kuigiza katika mkono wake usio na matata, na kuinama kama ishara ya kumwabudu mbele zake kwa kejeli. Wale watu waliompiga na kumtemea mate mfalme wa uzima sasa wanageuka kutoka kwenye macho yake makali yanayo choma, wanatafuta kukimbia kutoka mbele ya utukufu wake mwingi mno iliozidi kiasi . Wale amabo walipigilia na kugongelea misumali katika mikono na miguu yake na Yule askari aliyemchoma ubavu wake, wanaziona alama hizi kwa hofu kuu na majuto kwa uwazi wa kutisha viongozi wakuu na makuhani watakumbuka tukio hilo la kalvari kwa uwazi wa kutisha - *Pambano kuu* ukr 643 .

**c. Kwa namna gani ufufuo huu maalum unatofautiana na ufufuo ambao iutachukua nafasi sauti ya Yesu? Yohana 5: 28 – 29 [Linganisha na Daniel]**

## 3. HOFU ISIYO SEMEKA

**a. Upi utakuwa mwitikio wa mwanzoni kwa wanadamu wote - ukihusisha na waaminifu wachache wa Mungu – Kadri walivyotazama kwa mshangao kuja kwa muumbaji wa Ulimwengu aliyeketi juu ya Kiti cha enzi katika mng'ao wa utukufu? Yeremia 30: 6**

"Wenye haki wanalia na kutetemeka "Nani atakayeweza kusimama"? Wimbo wa malaika unanyamazishwa, na kunakuwepo na kipindi cha ukimya wa kutisha sana". -*Pambano kuu* ukr 641.

**b. Ni uhakika gani wenye kuchangamsha moyo mara moja huwafariji wale wenye shauku ya dhati kwa ajiri ya kuonekana kwa Bwana wao? 2 Wakor 12.9 [mwanzoni]**

"Kisha sauti ya Yesu kristo ikasikika, ikisema : Neema yangu inakutosha [ 2 Wakor 12. 9] Nyuso za wenye haki zinainuliwa juu na kila moyo unajazwa furaha. Na malaika wakapiga vinubi tena na kuimba kwa sauti ya juu kadri walivyoshuka na kuikaribia dunia" Ibid .

**c. Wafuasi wa kristo watasema nini wakati wa kurudi kwake katika wale ambao matumaini yao yamewekwa, na kwa namna gani ingetutia hamasa nasi sasa? Isaya 25 : 9.**

"Kwa wafuasi wake waaminifu, Kristo amekuwa mshiriki na rafiki kipenzi wa kila siku. Wameishi kwa mahusiano ya karibu sana katika ushirika endelevu na Mungu . Juu yao utukufu wa Bwana umeinuliwa . Ndani yao nuru ya ujuzi wa utukufu wa Mungu katika uso wa yesu kristo umekuwa ukiakisiwa, sasa wanafurahia katika miale ya mwangaza usiozimika na katika utukufu wa mfalme katika nguvu zake . Wanatayarishwa kwa ajili ya ushirika wa Mbinguni maana wanayo mbingu mioyoni mwao.

"Kwa vichwa vilivyoinuliwa, kwa mstari wa mwangaza wa jua la haki ukiwaangazia, na kushangilia kuwa ukombozi wao umakaribia, wanaondoka kumlaki Bwana arusi" - Vielelezo vya mafundisho ya kristo UK 421

"Je tunajiandaa kukutana na mwokozi kwa Amani, au tumemezwa na shughuli na mihangaiko ya anasa za ulimwengu ? Je hatutamani kuwa miongoni mwa hesabu ya wale ambao watamkaribisha kristo?" - *Alama za nyakati*, 17/ 4 / 1901.

## 4. WATAKATIFU WATOLEWA DUNIANI

**a. Eleza muujiza na maajabu kutokea kwenye ufufuo wa wenye haki. 1Wakoritho 15: 51-55**

"Mwana wa Mungu... Anayatazama makaburi ya wenye Haki, kisha anainua mikono yake kuelekea mbinguni na kupaza sauti yake akisema

"Amkeni Amkeni, Amkeni ninyi mliolala katika mavumbi, tokeni inukeni. Katika urefu wa Upana wa dunia yote wafu watasikia sauti hiyo na wale watasikia wataishi na kupata uzima" – *Pambano kuu* ukr 644

**b. Kwa jinsi gani hii huendana na Hukumu ya upelelezi ambayo ilikuwa imewahesabu wenye thamani ya umilele, kitu gani tunapaswa kukifanya kituo cha kuzingatia? 1Petro 4: 17. Luka 20: 35 [mwanzoni], 36.**

"Vitabu vya kumbukumbu vinapofunguliwa katika Hukumu, Maisha ya wote ambao wamemwamini Yesu yanachunguzwa mbele za Mungu. Kuanzia kwa wale ambao walikuwa wa kwanza kuishi duaniani, mtetezi wetu anawasilisha kila kesi kwa mfuatano wa vizazi, na kumalizia na walio hai. Kila jina linatajwa, kila kesi inachunguzwa Kwa makini Sana. Majina mengine yanakubaliwa na mengi yanakataliwa ...

"Wote ambao wametubu dhambi zao kikweli kweli, na kuidai damu ya kristo kwa Imani kama dhabihu ya upatanisho wao, walikuwa wamepata msamaha wakati huo majina yao yaliingizwa kwenye kitabu cha Mbinguni wamekuwa washirika wa haki ya kristo, tabia zao zimeonekana kupatana na sheria ya Mungu, dhambi zao zitafutwa, na wao wenyewe watahesabiwa kustahili uzima wa milele" - Ibid ukr 483

**c. Nini kinatokea kwa wenye haki - sehemu zote, wale ambao wanaishi wakati Yesu anaporudi, na wale waliofufuliwa kwa sauti yale? 1Wakoritho 15:49.**

"Kwa sauti ya Mungu [watakatifu walio hai] wanatukuzwa, sasa wanafanywa kuwa wasio na uharibifu kwa pamoja watakatifu waliokufa wakafufuliwa wananyakuliwa na kuinuliwa juu ili kumlaki Bwana wao hewani" - Ibid ukr 645 .

## *Alhamisi* *Tarehe 03 Augost*

### 5. UFUFUO WA KWANZA NA WA PILI

**a. Elezea majira au muda wa ufufuo wa jumla wa wenye haki, na furaha yake elezea. Ufunuo 2 0:1-6 [Linganisha tena na 1Thesalonike 4:16 – 17].**

---

---

"Mpaka ile saaa ya ushindi, wakati wa parapanda ya mwisho itakapolia, jeshi kubwa litainuka kwa ajili ya ushindi wa milele, kila mtakatifu aliyelala atatunza kwa usalama kama jiwe la thamani, ambaye anajulikana mbele za Mungu kwa jina kwa nguvu na uweza wa mwokozi ambao ulikaa ndani yao wakati walipokuwa hai na kwa sababu wanaoshiriki asili ya Uungu, Wanafufuliwa kutoka katika wafu" - Kwa Imani naishi uk 185 .

**b. Tunajifunza jinsi waovu walivyo na hatia ya kmsurubisha kristo na kufufuliwa kwenye ufufuo maalum, lakini pumziko la waovu waliokufa ni lini wanakutana na muumba wao kabla ya Uangamivu wao wa mwisho, je kwa nini hili ni wazo la kutisha? 1Wakorintho 6: 3, [Mwanzoni]. Ufunuo 20:4- 5, 12 –15.**

---

"Mwisho wa miaka elfu moja, kristo anarudi tena duaniani anaambatana na jeshi kubwa la waliokombolewa na kufuatiwa na jeshi kubwa la malaika . Kadri alivyozidi kushuka katika utukufu mkali anawaamru waovu waliokufa wainuke [wafufuke] ili wapokee maangamizo yao …. . Ni ulinganifu ulioje kwa hao ambao walikuwa wamefufuliwa katika ufufuo wa kwanza wenye haki walikuwa wamevikwa ujana na uzuri wa milele usiokufa. Lakini waovu wanakuwa na hali ya asili ya magonjwa na vifo" - Ibid uk, 355. *au Pambano kuu* ukr 662 .

"Siku hadi siku Mungu anawajaribu na kuwathibitisha watu wake. Neno lipo wazi hutangaza kwamba Kwa matendo yetu tunaamua hatima yetu ya milele" - *Manuscript Releases* 1 ukr 278.

## *Ijumaa* *Tarehe 04 August*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI

1. **Akina nani wanauwawa ghafla na ujio wa kristo, na kwa nini?**
2. **Ufufuo maalumu ni kwa akina nani, na kusudi la pili yake ni nini?**
3. **Je nimelenga kwenye kipindi cha Isaya 25:9 au ninatumaini atachelewa?**
4. **Kwa nini hukumu ya upelelezi ije na kuwepo kabla ya kuja a kwa Yesu?**
5. **Kwa nini miaka elfu moja itangulie kabla ya kukabili hukumu Yao?**

# Kukesha na Kungoja.

**(Mwokozi wetu Yesu kristo)alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote na kujisafishia watu wawemilki yake mwenyewe, wale walio na juhudi ktk matendo yao mema. (Tito2.14)**

''Kisha(kristo)alionyesha maana ya kukesha na kuwa tayari kwa ajili ya kuja kwake. Mda haupaswi kutumiwa kwa kungoja kizembe, bali kwa kufanya kazi kwa bidii."- *Vielelezo vya mafundisho ya kristo* uk 325.

**Imependekezwa kujifunza: Vielelezo vya mafundisho ya kristo ukr 353-365.**

## *Jumapili* *Tarehe 12 Augosti*

### 1. KUITWA KWA AJILI YA HUDUMA.

**a. Ni mfano gani yesu aliutoa kwa kuunganisha na marejeo yake mara ya pili? Mathayo 25:13-15**

''Mtu anayetaka kusafiri nchi ya mbali hu mwakilisha kristo ambaye wakati anaongea mfano huu, alikuwa karibu sana kuondoka kutoka duniani kwenda mbinguni."watumishi''(RV) ama watumwa ktk mfano huu huwakilisha wafuasi wa kristo....

Bwana wetu hufundisha kwamba kielelezo cha kweli cha maisha ni huduma. kristo mwenye alikuwa mtenda kazi, na anaweka sheria ya kazi kwa watumishi wake wote –kwa kumtumikia Mungu na wanadamu wenzao"... *Vielelezo vya mafundisho ya kristo*, ukr 325, 326.

**b. Ni vipaji gani vilivyolinganishwa, na kwa namna gani ni muhimu kwao? 1Wakor 12.7-17.**

''Karama zote na vipaji, pengine ni ktk asili au kujipatia, kiasili au kiroho...

Zinawezeshwa ktk huduma ya kristo. Katika kuwa wanafunzi wake, tujisalimishe wenyewe Kwake pamoja na vile vyote tulivyonavyo. Karama hizi huzirudisha kwetu zitutakase na kutusafisha, ili tutumike kwa ajili ya utukufu wake kwa kuwabariki wanadamu wenzetu'' -Ibid ukr 328.

# *Jumatatu*

*Tarehe 07 Augosti*

## 2. KUTUMIA VIZURI KILE CHEMA ULICHOPEWA

**a. Katika kutazama ukweli mzito wa wakati wetu, Nini tunapaswa kujifunza kutoka ktk mfumo wa kristo kuhusu kutumia vipaji tulivyopewa? Mathayo 25:16-18**

"Swali linalotuhusu sana si kwamba nimepokea kiasi gani, bali ninafanyia nini kile nilicho nacho? maendeleo ya nguvu zetu zote ndiyo wajibu wetu wa kwanza tunaodaiwa na Mungu na wanadamu wenzetu. . Hakuna hata mmoja ambae hakui kila siku ktk uwezo na kufaa kwa matumizi yenye kuletea faida anayetimiza malengo ya kuishi. Katika kufanya tangazo la kuwa na imani ktk kristo tumejiwekea agano wenyewe kwa Namna yote inayowezekana kwetu kuwa kama watenda kazi kwa ajili ya Bwana, na sharti tuendeleze kila Nyanja kwa kiwango cha juu sana" -*Vielelezo vya mafundisho ya kristo* uk 329, 330.

**b. Jambo gani linaweza kupatikana kwa kutumia kikamilifu karama zetu? Mathayo 25:19-20, 22.**

"(Bwana)hawezi kutujali kupita kiasi tunapokosa viwango vya sifa, lakini wakati tunapotumia kile ambacho tunacho, yeye atatenda pamoja nasi kwa kutuongeza na kutuongoza kila nguvu ya kuwaza na kutenda. Kwa kila nafsi iliyojitoa kwa moyo wote, kafara au sadaka ya bidii kwa ajili ya Huduma ya Bwana Nguvu zetu zitaongezwa. Wakati tunapozaa wen yewe kama vyombo kwa ajili ya kufanya kazi ya Roho Mtakatifu, Neema ya Mungu hutenda kazi ndani yetu kwa kuikana tamaa na mwelekeo wa zamani, kwa kutiwa nguvu ya kushinda mielekeo na kuumbiwa tabia mpya. Kadri tunavyosamini na kutii uvuvio wa Roho Mtakatifu, mioyo yetu itakuzwa ili kupokea zaidi na zaidi. Nguvu iliyokufa inafufuliwa ipokee maisha mapya na nguvu ya kuwaza kiakili. . .

"Kwa njia ya imani ktk uwezo wa Mungu, Ni maajabu kiasi gani uwezo dhaifu wa mtu huenda unakuwa jinsi alivyoamua, Namna alivyo matokeo ya kuzaa sana. Ambaye huanza na maarifa kidogo sana katika njia ya maarifa ya badae ataipata hazina yote ya kile anachokijua, wakati anapotafuta kwa bidii kwa maarifa ya baadae ataipata hazina yote ya mbinguni inasubiri malipo yake. Zaidi yule atafuatae Nuru ya haki, atapokea nuru zaidi ya hapo . Mmoja anayeweza kujaribu kueleza neno la Mungu kwa wengine, pamoja na upendo kwa ajili ya nafsi, Unyoofu utakuwa wake" - Ibid ukr 353, 354.

## 3. SHUKRANI AU MANUNG'UNIKO?

**a. Ilikuwaje kwa mtumwa asiyemwaminifu aliyelaumiwa kwa kushindwa kuitumia taranta yake, kwa nini ktk mtazamo huo ni onyo kwetu? Mathayo 25:24-8**

---

---

"Kuna wengi ambao ktk mioyo yao wanamshutumu Mungu, kuwa ni Bwana mgumu kwa sababu anadai mali zao na huduma yao. Lakini hatuwezi kumletea Mungu chochote ambacho tayari si mali yake... vitu vyote ni mali ya Mungu, si kwa njia ya uumbaji tu bali pia kwa njia ya ukombozi. Mibaraka yote ya maisha haya na maisha yajayo inayotolewa kwetu, ilitiwa na kuwekwa muhuri wa mateso ya kalvari. Kwa hiyo shutuma juu ya Mungu kwamba ni Bwana mgumu, huvuna asipopanda ni uongo."-*Vielelezo vya mafundisho ya kristo* ukr 362 (coz).

**b. Kwa jinsi gani bidii yetu huonyesha tabia yetu ya malalamiko na kufanya udhuru sisi wenyewe, Na kwa nini tunapaswa kutii tumaini lenye bidii la Bwana k wa ajili ya kila mmoja wetu kabla ya kurudi kwake? Mithali 30:15-16; Isaya 29:24.**

---

---

"Kutoridhika, Kutafuta kasoro na kuweka Misimamo Mikali ni lazima kuiacha. Umekaa mda gani kupata ushindi juu ya Nia yako yenye upoto fu na kasoro ktk Tabia yako? pamoja na mwendelezo unaofanya sasa, mda wako wa majaribio unaweza kufungwa kabla ya kufanya juhudi muhimu zilizo imara ili kukupa wewe ushindi dhidi ya ubinafsi. Taka majaliwa ya Mungu kuwa uwekwe ktk nafsi ya upekee wako kama pa kuishi, utakuwa na bidii na kufunuliwa" - *Shuhuda ya 4* ukr, 341, 342.

"Wengi wanaamua kujitumikia wao wenyewe na shetani kwa kushindwa kufanya juhudi thabiti ili kushinda tabia zao zenye Dosari. Wakati wengi wanagusa mielekeo yenye uovu, Wakati huohuo wanatarajia kuwa washindi, wanakusudia kujiteketeza... kwa jina la Yesu muwe washindi kuanzia sasa,

"Katika hii siku yako"(Luka 19:42)Usipange ama kujielimisha mwenyewe. Huwezi kabisa kutiwa moyo na Bwa na kwa kiwango cha ubinafsi wako. Kama vile upendo mkuu kama mwokozi amekuonyesha ungefunuliwa pamoja na uvumilivu na unyenyekevu, mkuu na kuiendeleza furaha kwa ajili ya kuwa na furaha, lazima kuziongoza fikra na maneno. Itahitajika juhudi ya hali ya juu kwenye sehemu yako, Hata hivyo lazima ikamilike kama wewe ni mtoto wa Mungu. Usichoke ktk juhudi zako. shetani anapambana kwa ajili ya Nafsi yako, Lakini lazima ashindwe na kukata tamaa"- Ibid ukr 344.

## 4. USIFUNIKE UDANGANYIFU NA KUUKIMBIA.

**a. Kwa namna gani kielelezo au mfano wa mwana wa Mungu hukanusha shutuma za uongo za Adui mkuu wa nafsi zetu? mwanzo 3:4-5**

''Shetani huwaongoza watu kumwona Mungu kama mwenye sifa kuu ya ukatili asiye na haki- mmoja ambaye ni jaji mkali, Mwenye kulazimisha, mwonevu alimchukulia muumbaji kama mwenye kuangalia kwa jicho la wivu ili kuona makosa na mapungufu ya watu, ili aweze kushusha ama kuwaletea hukumu wao. Giza hili liliondolewa kwa kufunuliwa ulimwenguni Upendo wa Mungu usiokoma, k wamba Yesu aje kuishi miongoni mwa watu''-*Hatua za kristo* ukr 11.

''Shetani huielezea sheria ya Mungu kama sheria ya ubinafsi, haiwezekani sisi kuyatii maagizo yake''-Tumaini la vizazi vyote uk 24.

''Kama macho yetu yangefumbuliwa, tungewaona malaika waovu wanaotuzunguka, wakibuni njia mpya za kutuudhi na kutuangamiza. Pia tungewaona malaika wa Mungu wakitulinda dhidi ya nguvu za malaika waovu. kwa kuwa jicho la Mungu lisilosinzia liko juu ya Israel daima ili kuwatendea wema, Naye atalinda na kuwaokoa watu iwapo wanamtumaini yeye...

''Malaika alisema''kumbuka huko ktk uwanja wa mapambano''Nalio na kuwa lazima tukeshe na kuwa na silaha zote na kuchukua ngao ya imani, na kisha tutaweza kusimama na mishak ya Adui mwovu iwakayo kama moto haiatatudhuru'' - *Maandiko ya Awali* uk 60

**b. Shauku ya wema wa Mungu huonekanaje kutusaidia sisi kushinda kasoro zetu na udhaifu wetu? Zaburi 20:1-2, 7-9; 94:17-18.**

''Kila msukumo wa Roho mtakatifu unawaongoza watu ktk wema na kwa Mungu unaandikwa ktk vitabu vya mbinguni''-*vielelezo vya mafundisho*, uk361.

''Bwana hutamani watu wake wafikie hatua za ngazi ya juu kabisa ili waweze kumtukuza yeye kwa kuumiliki uwezo yeye anataka kutukuzwa. Kupitia Neema ya Mungu kila mahitaji muhimu yamefanyika kwa ajili yetu kwa kufunua kile tunachotenda juu ya mipango bora kuliko ile ulimwengu unatenda...

''Wale ambao hawana vipaji vikubwa vya karama hawahitaji kukata tama hebu watumie kile walichonacho kwa uaminifu wajilinde na kila udhaifu unaoelezwa ktk Tabia zao, waitafute Neema ya Mungu iwafanye kuwa imara''-Ibd ukr 358

## *Alhamis* — *Tarehe 10 Augost*

## 5. WATENDAKAZI WASHINDI PAMOJA MUNGU

**a. Kadri tunavyojiandaa kwa ajili ya marejeo ya Bwana wetu ktk kujisalimisha kikamilifu ktk huduma zake, shauku yetu kuu ni ipi?na yake ni ipi? Zaburi 145:10-12**

---

---

″Wakati Bwana anapochukua hesabu ya watumishi wake, kurejeshwa kwa kila talanta kutachunguzwa kwa makini. Kazi iliyofanywa hudhihirisha tabia ya mtendakazi.

″Wale waliopokea talanta tano na waliopokea mbili hurudisha kwa Bwana wao amana ya talanta na ongezeko la faida yao. Kwa kufanya hivi huwadai kustahili wao wenyewe.

Talanta zao ni zile walizokuwa wamekabidhiwa wamechuma talanta nyingine, lakini wasingechuma kama wasingeweza. Wanaona kuwa wamefanya wajibu wao tu. Mtaji ulikuwa wa Bwana wao, na faida ilikuwa fukara milele zote.

″Lakini Bwana anapopokea talanta anawasifu na kuwazawadia watendakazi kana kwamba stahili yote ilikuwa mali yao. Uso wake unajaa furaha na kuridhika. Anajawa na furaha kwamba anaweza kuweka Baraka kwao, Siyo kwa sababu ya deni analowadai, bali ni kwa sababu ya moyo wake unafurika upepo wa wema″-*Vielele zo vya mafundisho ya kristo* uk 360, 361.

″Baba yetu wa mbinguni hawezi kudai zaidi ya au chini ya kile alichotupa sisi uwezo wa kutenda. Huwaongoza watumishi wake wasibebe mzigo mzito ambayo hawawezi kuibeba″kwa maana yeye anatujua umbo letu, hutukumbusha kuwa sisi tu mavumbi″(Zaburi 103.14) yote ambayo huyadai kutoka kwetu kwa kupitia Neema ya Mungu tunaweza kutenda″-Ibid ukr 362

## *Ijumaa* — *Tarehe 11 Augosti*

## MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI

1. **Kwa nini mara nyingi halifahamiki kusudi la Mungu ktk kutoa talanta?**
2. **Ingawa unaweza kuwa dhaifu au mkosaji, jempango wa Mungu ni upi kwa ajili ya kukusaidia?**
3. **Hebu linganisha mtumishi mmoja mwenye ile talanta moja na binadamu wa kawaida wa siku hizi.**
4. **Kwan amna gani tunaweza kuikwepa mikakati ya Adui inayozuia utakaso wetu?**
5. **Eleza namna tunavyoweza kupata ushindi kwa kuwa na uhakika, mawakala halisi wa Mungu.**

# Uhusiano wa Pekee pamoja na Kristo.

**"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo Yesu amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, Tazama yamekuwa mapya". (2 Wakorinto 5:17).**

"Wakati tunapogeuka kuelekea kwenye jua la haki, pale tunapokuwa katika mguso na Kristo, nafsi yote inajaa mwangaza wa uwepo wa Mungu" – *Mlima wa Baraka* Ukr. 40.

**Imependekezwa kujifunza:** *Huduma ya uponyaji,* Ukr . 21-85,
*Jjumbe zilizoteuliwa* vol. 1, Ukr. 40-48.

## *Jumapili* Tarehhe 13 Augosti

### 1. NURU HUANGAZA KATIKATI YA GIZA.

**a. Kwa namna gani maandiko huonyesha hali yetu ya kutokuwa na matumaini? Ayubu 14:4; Rumi. 3.23; 8:7.**

---

---

"Haiwezekani kwa sisi wenyewe kujiokoa kutoka kwenye shimo la dhambi ambalo tumezama. Mioyo yetu ya uovu hatuwezi kuibadilisha" – *Hatua za Krisot* uk 118.

"WWengi hawana furaha kwa sababu hawana utakatifu. Utakaso wa moyo, unyoofu wa akili, hizo pekee zaweza kubarikiwa na Mungu. Wakati dhambi inapokuwa jambo jema kabisa, inaweza kuwa ndiyo mwisho wa kufanya chochote bali ni kukosa furaha" – *Shuhuda ya 6,* ukr. 53.

**b. Katika upendo wake Mkuu na Rehema, Mungu amefunua nini kwetu katika siku hizi za mwisho, na kwa namna gani inaathiri maisha yetu katika njia ya vitendo? Rumi. 3:24 – 26, 8:1-4.**

---

---

---

"Bwana na mwokozi wetu ameweka sehemu ya utawala wake utajiri wake na utukufu, alitutafuta sisi ili aweze kutuokoa kutoka kwenye taabu na mateso, na kutufanya kama yeye alivyo. Alijinyenyekeza mwenyewe na kuchukua asili yetu ili kwamba tuwe na uwezo wa kujifunza yake na kuiga maisha yake ya ukarimu na kuufia ubinafsi. Mfuate yeye hatua kwa hatua hadi mbinguni" – Ibid Vol.2 Ukr. 170.

# *Jumatatu* **Tarehe 14 Augosti**

## 2. UPENDO WA MUNGU KWA AJILI YETU

**a. Elezea utimilifu wa mpango wa ukombozi. 1 Wakorintho 1.30, 2 Wakorintho. 5:19-21.**

---

---

"Kristo alijitoa mwenyewe kuwa kafara ya upatanisho, apate kuokoa ulimwengu uliopotea. Alitenda kama tunavyostahili ili kwamba tupate kuchukuliwa kama anavyostahili. Alihukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu, wala yeye hakuwa mshirika wa dhambi ili kwamba tuweze kuhesabiwa haki yake, ambapo sisi hatukuwa washirika wa haki, alihangaika hadi kifo ambacho kilikuwa chetu ili kwamba tuweze kupokea uzima ambao ulikuwa wake."kwa kupigwa kwake sisi tumepona" (Isaya 53.5).

"Kristo alijaribiwa katika mambo yote kama vile tunavyojaribiwa sisi. Naye kwa mara moja alisimama imara katika uaminifu kwa upande wake katika mahala majaribu, katika muda wa udhaifu mkuu (njaa) anakabiliwa na jaribu kali, mwangalie katika miaka yake ya utumishi, alishambuliwa kila mahali kwa ajili ya kuukabili uovu. Hebu mwangalie katika kifo cha uchungu msalabani. Hayo yote yalimpata kwa ajili yetu." – *Shuhuda ya 8* ukr. 208, 209.

**b. Nani anaweza kuwa mzoefu wa Baraka za pendo la Mungu? Mathayo 11.28, Yohana 6:38.**

---

---

"Kuja kwa Yesu hakufanyi kuhitaji jitihada za akili kali na chungu, ni rahisi tu pale unapokubali kupokea sheria na masharti ya wokovu ambao Mungu aliuweka wazi katika Neno lake. Baraka imetolewa bure kwa wote...

"Katika jina lililojuu ya kila jina, jina la pekee kati ya watu ambalo limetolewa kwa watu liwezalo kuokoa, dai ahadi ya Mungu sema"Bwana unisamehe dhambi zangu, Naiweka mikono yangu katika mikono yako kwa msaada, lazima niipate au niangamie, sasa naamini" – *Jumbe zilizoteuliwa* Vol 1, Ukr. 333, 334.

"Hisia ya kina ya mahiitaji yetu na hitaji letu kuu kwa ajili ya mambo tunayoyaomba lazima tuyaelezee katika sara zetu, pengine hayakusikiwa. Lakini haitakiwi kuchoka kwa kusitisha maombi kisa tu maombi hayajibiwi mara moja". Ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu na wenye nguvu wauteka" (Mathayo. 11.12) nguvu hii hapa ina maanisha bidii na juhudi takatifu, kama vile Yakobo alivyoonyesha. Hatupaswi kujitahidi kwa kufanya juhud zetu wenyewe kwa hisia kali, bali kwa utulivu, kwa kudumu katika maombi. Tunapaswa kuelekeza maombi yetu kwenye kiti cha enzi cha Neema" – *That I may know Him*. Ukr 272.

## 3. MAISHA MAPYA NDANI YA KRISTO

**a. Ni mtazamo na tabia gani mpya inakuwa wazi kadri tuna-vyomtumaini Kristo Yesu? 2 Wakorintho. 5:17. Galatia 5:6 Filipo 2.12-13**

---

---

"Imani ifaayo kutuleta katika mawasiliano muhimu pamoja na Kristo hudhihirisha upande wetu upendeleo mkuu, tegemeo kamili, kuwekwa wakfu kikamilifu. Imani hii hufanya kazi kwa upendo na huitakasa nafsi. Hufanya kazi katika maisha ya mfuasi wa Kristo mtii wa kweli wa sheria za Mungu. Kwa kumpenda Mungu na kuwapenda wanadamu yatakuwa matokeo muhimu ya kuunganishwa na Kristo" – *Jumbe zilizotolewa* Vol 1 ukr. 334.

"Ni nguvu tu ya uungu inayoweza kuhuisha moyo wa mwanadamu na kuijaza nafsi pendo la Kristo ambapo daima utadhihirika wenyewe upendo kwa ajili ya wale ambao yeye aliwafia………….. Pale mwana-damu anapobadilishwa na Mungu, hali ya tabia njema inakuja, nguvu ya mvuto mpya inatolewa, na anapenda mambo ya kimbingu ambayo Mungu huyapenda...

"Lakini wale ambao wanasubiri kwa kutazamia muujiza wa badiliko, pasipo kuamua kwa juhudi katika sehemu zao kwa kuishinda dhambi, watakuwa wameshindwa. Hatuna sababu ya kuogopa pale tunapomtaza-mia kristo, haipo sababu ya kuwa na hofu ya mashaka bali yeye ni mwezi wa kuokoa wote ambao humwendea yeye, lakini isije daima siku zote hofu ya asili yetu ya zamani, tutaupata ukuu, ambapo adui atabuni baadhi ya mitego ambapo tutapata kuwa mateka wake." *- Ibid Ukr.* 336, 337.

**b. Kwa nini tumaini la kina daima siku zote linaendelea kuujaza moyo wa kila mshiriki, Na kwa namna gani hili linatuathiri sisi juu ya missing thabiti? Yohana. 15:45, 10, Rumi. 6:6, 10-11.**

---

"Muungano pamoja na Kristo, uundwe mara moja, lazima udumishe... huu siyo mguso wa kawaida, siyo wa kuachwa, kuunganishwa... "

"Kudumu katika Kristo inamaanisha mara kwa mara kumpokea Roho wake maisha ya kujisalimisha chini ya huduma yake".

"Kwa njia ya mazoezi ya mapenzi ya haki, badiliko linaweza kufanya katika maisha yako, kwa kuyatoa mapenzi yako na makusudi yako kwa Kristo, unashiriki mwenyewe nguvu za enzi yote ya mbinguni na mamlaka yote utakuwa na nguvu kutoka juu ya kukushikilia wewe uwe imara, hivyo kwa njia ya kujisalimisha kwa Mungu kwa mara, utakuwa umewezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya Imani" – Hatua za Kristo Ukr, 48.

## 4. KUKUA KATIKA NEEMA.

**a. Wakati moyo unapojisalimisha kwa Kristopamoja na maombi kwa ajili ya hekima zake, ni badiliko gani hutokea katika tabia? Galatia 5:22-23. Zaburi. 119:18.**

"Kwa kumtazama (Kristo) tunabadilishwa na kadri tunavyotafakari juu ya utimilifu wa tabia njema ya uungu, tutabadilishwa kabisa. Na kufanywa upya kwa mfano wa usafi wake. Kwa njia ya Imani kupitia mwana wa Mung badiliko linachukua nafasi katika tabia, mtoto wa uasi anakuwa mwana wa Mungu. Kutoka katika mauti hadi kwenye uzima, anakuwa wa kiroho na kuyabaini mambo ya Kiroho. Hekima za Mungu zinaangazia akili zake, naye anashuhudia mambo ya ajabu ya sheria yake. Kadi mtu anapozidi kubadilishwa na ukweli, kazi ya badiliko la tabia hufuatia, anaongezeko katika kipimo cha ufahamu na uelewa. Katika kumtii Mungu, amekuwa na akili ya Kristo, na mapenzi ya Mungu yanakuwa mapenzi yake." – *Jumbe zilizoteuliwa* Vol. 1.uk 338.

**b. Kwa nini moyo uliowazi kujifunza na kutafakari Biblia na Roho ya unabii ni ufunguo muhimu katika njia hii? Zaburi. 199:24-27.**

"Siyo peke yao tu wale ambao watazikana shuhuda hadharani, au ambao watazitilia mashaka na wasiwasi, hiyo ni hatari ya kihistoria. Kuikataa Nuru na kuipuuza"- *Shuhuda ya 5* Ukr. 680."

"Mtunga zaburi anasema"Neno lako ni taa ya Miguu yangu, na nuru katika njia zangu" (Zaburi. 119:105) wala siyo tatizo iwapo halijafunguliwa au halijasomwa." – *Review and Herald 04*, January 1881.

"Kwa kumtazama mara kwa mara Yesu Kristo katika jicho la Imani, tutaimarishwa. Mungu atafanya ishara za mafunuo ya thamani zaidi kwa wenye njaa na kiu yake. Watampata Kristo ambaye ndiye mwokozi pekee. Kadri wanavyojilisha juu ya Neno lake, watampata Yule Roho wa Uzima. Neno la Mungu huiangamiza ile asili, yaani asili ya kiulimwengu na kukupa maisha mapya katika Kristo Yesu. Roho Mtakatifu huja nafsini kama mfariji. Kwa kufanywa wakala au mshiriki wa Neema yake, sura ya Mungu inazalishwa ndani ya mwanafunzi, na kupokea mfano wa Uungu."Hii kuishi ina maana gani? Kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu" huu ndio ulaji wa mkate ushukao kutoka mbinguni." – *Tumaini la vizazi vyote* Uk. 391.

## *Alhamis* *Tarehe 17 Augosti.*

### 5. KUAKISI NURU

**a. Ulimwengu huu wa giza unahitaji kitu gani muhimu zaidi? Mathayo. 5:14-16.**

---

---

---

"Ni upendeleo wa kila nafsi kwamba iwe na mfereji ulio hai ambao Mungu atautumia kuwasilisha katika ulimwengu hazina za Neema yake utajiri wa Kristo usio na kikomo. Hakuna jambo ambalo Kristo anatamani zaidi kama mawakala ambao watawakilisha katika ulimwengu roho na tabia yake. Hakuna jambo ambalo ulimwengu unahitaji zaidi kama udhihirisho wa upendo wa mwokozi kupitia ubinadamu. Mbingu yote inangojea mifereji inayoweza kumimina mafuta matakatifu yaweze kuwa furaha na Baraka katika mioyo ya wanadamu" – *Vielelezo vya mafundisho ya Kristo* Ukr. 419

**b. Lipi linakuwa lengo la maisha yetu na kupitia hili ni matokeo gani yatakuwa yamepatikana?. Galatia 2.20, Isaya 60: 1 – 3.**

---

---

---

"Kukaa ndani ya Kristo ni kuchagua tu tabia ya Kristo, ili kwamba shauku yake ifungamanishwe naya kwako. Kukaa ndani yake, kwa kufanya tu kile akipendacho yeye. Tabia hizi ni za kitume, kinyume cha hapo huwezi kupata pumziko" – Jumbe zilizoteuliwa Vol. ukr.110.

"kupitia Roho Mtakatifu, Neno la Mungu ni Nuru tena ni mwanga kama lita kuwa nguvu ya badiliko katika maisha ya mpokeaji. Kwa kukuza mioyoni mwao kanuni za Neno lake, Roho Mtakatifu hukaza chembechembe za Mungu ndani ya mwanadamu. Nuru ya Utukufu wake – Tabia yake – itaangaza ndani ya wafuasi wake." – *Vielelezo vya mafundisho ya Kristo* Ukr. 414.

## *Ijumaa* *Tarehe 18 Augosti.*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI.

1. **Elezea hali ngumu ya jamii ya kibinadamu, nani anayeweza kuikamilisha?**
2. **Kwa nini ni kawaida kuunganika vya kutosha pamoja na Kristo?**
3. **Jambo gani ungemwambia mtu aliyekatishwa tamaa na Injili?**
4. **Biblia na Roho ya Unabii inafanya jukumu gani tupate utakaso wetu?**
5. **Elezea jinsi mvuto wako waweza kuwa chanzo cha burudiko kwa wengine.**

# Jiweke Tayari

**"Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utukufu ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao. (Ebrania. 12.14).**

"Je, kwa maisha na kwa mazungumzo yetu matakatifu, yanayoonyesha wale wanaotuzunguka kwamba tunatazamia kufunuliwa kwa utukufu wa Bwana na Mowkozi wetu Yesu kristo?

**Imependekezwa kujifunza: shuhuda ya 5 ukr. 217-228, 743-746.**

## *Jumapili* *Tarehe 20 Augosti.*

### 1. EPUKA MTEGO WA WENGI.

**a. Ni uongo gani wenye hatari unaozidi kufundishwa kwa maneno ya kidini katika dunia ya leo, na kwa jinsi gani maandiko hukanusha? Yakobo. 2.14, 20-22, 24.**

---

---

"Kutoka katika mimbari za Makanisa ya leo maneno yanatamkwa. Amini, wewe ni kuamini tu, uwe na Imani katika Kristo, huna la kufanya kwenye sheria za zamani, we mwamini Yesu pekee. Hili linautofauti kiasi gani kutoka kwenye maneno ya mitume wa Yesu ambao walifundisha na kutangaza kwamba: Imani bila matendo imekufa!" – *Imani na matendo* Ukr. 89.

"Kupenda dini rahisi ambayo haihitaji kung'ang'ania, kujikana nafsi na kuachana na upumbavu wa ulimwengu, kumefanya fundisho la Imani, na Imani peke yake, kuwa fundisho kuu linalopendwa sana na watu wengi, lakini je, Neno la Mungu linasemaje?... (Yakobo. 2.14, 21-22, 24) imenukuliwa.

"Ushahidi wa Neno la Mungu unapingana na fundisho hili lenye hila, la imani bila matendo. Sio Imani ambayo inadai upendelo wa mbinguni pasipo kubaliana na masharti ya kupata rehema na msamaha, huo ni ufedhuli na ubatili. Kwa maana Imani ya kweli ina msingi wake katika Ahadi na katika chakula cha maandiko."

"Hebu waache kujichanganya wenyewe kwa Imani kwamba wanaweza kuwa watakatifu wakati wakivunja kwa hiari moja wapo ya masharti ya Mungu. Utendaji wa dhambi makusudi unanyamazisha sauti ya Roho wa Mungu ya usahidi, na humtenga mtu na Mungu."Dhambi ni uasi wa sheria" na yeyote atendaye dhambi hakumwona yeye, wala (hakumtambua) hakuna yeye." – *Pambano kuu* Ukr. 472.

## 2. KUPOKEA KIUKWELI MPANGO WA UKOMBOZI

**a. Hatua ya kwanza ni ipi kuelekea kwenye wokovu halisi?. Matendo. 2.37-38, Rumi. 5:1.**

"Kadri tunapomtazama mwanakondoo wa Mungu juu ya msalaba wa Kalvari, siri ya ukombozi huanza kufunuliwa katika akili zetu, wema wa Mungu hutuongoza katika toba. Katika kuwafia wenye dhambi Kristo alidhihirisha upande wa hali ya juu usio elezeka wala kutamnbulikana, kadri mwenye dhambi anapolitazama pendo hili, moyo wake hutakasika, moyo wake unavutiwa, na akili pia zinavutiwa, ndipo katika nasi yake majuto yanaamka." – Hatua za Kristo. Ukr. 26, 27

"Toba huhusisha huzuni na masikitiko kwa ajili ya dhambi na kuiacha tusipokuwa dhambi hadi tuone madhara yake ni hatari, hatutakuwa na badiliko katika maisha, hadi tutakaiacha na kuikana ndani ya moyo" – Ibid. Ukr. 23.

**b. Kwa wafuasi wa Kristo, ukweli muhimu ni upi wenye umuhimu mkuu? Ebrania. 12.14, 1 Petro. 1.13 -16.**

"Utakatifu ni makubaliano pamoja na Mungu"*- Shuhuda ya 5* ukr. 743.

"Wakati wa kuongoka mwenye dhambi anapata amnai kwa Mungu kupitia hiyo sasa anapaswa"kusonga mbele katika ukamilifu""kukua na kufikia kipimo cha tabia ya ukamilifu wa Kristo" *– Pambano kuu Ukr.* 470.

"Kupitia tabia njema na wema wa Kristo, kupitia haki yake ambayo kwa njia ya Imani tunahesabiwa haki, nasi tunaufikia ukamilifu wa tabia ya Kristo. Kazi zetu za saa na za kila siku zilizoelezwa katika maneno ya mitume,"Tumwelekee na kumtazama Yesu ndiye mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu." – (Ebrania 12.2)..."

"Kudhihirishwa kwa upendo wa Mungu, wema wake na Rehema zake, na kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya Moyo kuwaangaza na kuufanya upya, umewekwa ndani yetu kwa njia ya Imani, umefungwa kwa karibu sana na mahusiano ya Kristo, anayesafisha mawazo, tunaweza kufahamu siri ya udanganyifu wa shetani..."

"Ndugu na Dada, kwa kumtazama Yule tunabadilishwa. Kwa kukaa ndani ya pendo la Mungu na Mwokozi wetu, kwa kutafakari ukamilifu wa tabia ya Uungu na kuidai haki ya Kristo kama yetu kwa njia ya Imani, tunabadilishwa kwa sura hiyo"*- Shuhuda ya 5,* Ukr. 744.

## 3. KULIFIKIA LENGO

**a. Mpango wa Mungu ni upi kwa ajili yetu katika matayarisho ya kukutana kwetu na Bwana wetu wa Amani? Mathayo. 5:48. Zaburi. 101.2.**

“Wakati Kristo anapolitakasa Hekalu, waumini duniani wangekuwa waangalifu sana kuyatambua maisha yao, walinganishe maisha yao na viwango vya haki. Kadri wanavyoona kasoro zao, wanapaswa kutafuta msaada wa Roho wa Mungu ili awawezeshe kuwa na nguvu ya tabia njema kwa kuyapinga majaribu ya shetani na kufikia kiwango cha ukamilifu. Waweze kuwa washindi juu ya kila jaribu ambalo linaonekana lina nguvu nyingi mwanadamu hawezi kulibeba, nguvu za Uungu zitaunganishwa pamoja na juhudi zao za kibinadamu.” – Refleting Christ Ukr. 296.

“Ishambulie dhambi, lazima upambane na uwe mshindi, kataa sifa za tabia zisizokubalika, pengine ni za urithi au za kulelewa, zingeachwa na kutengana nazo ukilinganisha na iliyo kanuni kuu ya haki. Pia Nuru iangaze kutoka kwenye Neno la Mungu, wanapaswa kuwa imara kuipinga na kuishinda kupitia uwezo wa Yesu.” – Elimu ya Mkristo Ukr. 113.

**b. Kwa nini tunapaswa kujitahidi kwa ajili ya ukamilifu kwa kutembea katika Nuru ya ufunuo wa mpanezi ya Mungu? 2 Wakor. 9:24-25, Filipo. 3.12-14. .**

“Kutembea katika Nuru inamaanisha kuazimia, kukusudia na kuamua pia kuzoeza fikra kwa kutumia nguvu ya utashi katika jitihada ya dhati kwa kumwakilisha Kristo katika uzuri wa tabia. Inamaanisha kuachana na uovu wote. Siyo kutulia tu kwa kuridhika na kujisemea“ Mimi ni mtoto wa Mungu.” Je, unamtazama Yesu, na kwa kumtazama linakuja badiliko la wema wake? Kutembea katika Nuru humaanisha mwendelezo wa kupata mafanikio kiroho”. *Wana na binti za Mungu* ukr. 200

“Kwa namna yoyote makosa au kushindwa kwetu hapo nyuma, kwa msaada wa Mungu tunaweza kuinuliwa juu ya hayo” – Huduma ya uponyaji ukr. 516

**c. Nini kimeahidiwa kwa wale ambao wanatamani maadili halisi ya haki? Efeso. 3.16, Mathayo. 5:6.**

## 5. NGUVU KUBWA KWA MHITAJI YETU YA HARAKA.

**a. Kwa namna gani ya kipekee tunaweza kujitayarisha kusimama katika vita kuu ya mwisho? Yeremia. 15:16.**

---

"Hakuna hata mmoja atakayeweza kusimama katika vita kuu ya mwisho. Isipokuwa tu wale wenye kuimarisha akili zao na kujitoa kwenye ukweli wa Biblia"- *Pambano kuu* Ukr. 593, 594.

**b. Tunaweza kunufaikaje kwa kuanza kujitolea katika tabia zetu za Ibada bora kwa kuyajua mapenzi ya Mungu? 1 Yohana 5:14, , Zaburi 119.129-131.**

---

---

"Shuhuda hazisomwi na hazisaminiwi, Mungu amesema nanyi. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwenye Neno lake na kutoka pia kwenye shuhuda vyote vimeachwa na kupuuzwa kwa kutupiliwa mbali. Matokeo yake ni dhahiri tena wazi katika ukosefu wa usafi wa ibada, na Imani miongoni mwetu."

"Hebu kila mmoja aweke swali moyoni mwake." Tunaanguka kwa namna gani katika hali hii ya unyonge wa kiroho na mafarakano? Je, hatujaleta sisi wenyewe hali ya kumfanya Mungu akunje uso wake kwa sababu matendo yetu hayaendani na Imani yetu?" – *Shuhuda ya 5 ukr.* 217.

"Uwe na tahadhari kwa jinsi gani umepuuza maombi ya sirini na kujifunza neon la Mungu. Hizi ndizo silaha zako dhidi yake ambaye anajitahidi na kutamani kuficha juhudi zako na maendeleo ya kuelekea mbinguni." – *Ujumbe kwa vijana* Ukr. 96

**c. Kwa nini ni muhimu kujitoa kwa moyo wote asilimia 100 kuyatii makusudi ya Mungu kadri yanavyokuwa wazi yaliyoandikwa kutoka kwenye mwongozo? Yakobo. 1:21-25**

---

---

"Shetani anawaongoza watu wengi kuamini kwamba Mungu atasamehe kukosa uaminifu kwao katika mambo madogo madogo ya maisha, lakini Bwana alipokuwa anashughulika na Yakobo anaonyesha kwamba hawezi kuvumilia au kuruhusuuovu kwa namna yoyote. Wote wanaojaribu kutoa udhuru au kuficha dhambi zao na kuziruhusu zidumu katika vitabu vya mbinguni bila kusamehewa na kuungamwa, watashindwa na shetani" -*Pambano kuu Ukr.* 620.

"Mungu hufanya kazi kwa nguvu na uwezo mkuu kwa watu wake waaminifu wa Neno lake pasipo maswali na mashaka" – Shuhuda ya 4 Ukr. 164.

## 7. JIWEKE CHINI YA UTAKASO.

**a. Elezea taratibu za utakaso. 1 Yohana. 3.1-3, ebrania 5:12-14, 6:1.**

"Utii unaweza kuleta ukamilifu kwa njia tu ya haki ya Kristo ambayo hujaza harufu nzuri ya Uungu kila tendo la utii. Mahali pa Mkristo ni kudumu katika ushindi wa kila kosa...

"Siku baada siku Mungu hufanya kazi kwa ajili ya utakaso wa watu, na watu wanashirikiana pamoja naye kwa kuweka mbele juhudi za kudumu katika kuchimba tabia ya haki... mwokozi wetu mara zote huwa tayari kusikia na kujibu maombi ya walio na moyo wa kupondeka, Neema na amani inakuwa nyingi kwa waaminifu wake. Kwa furaha huwabariki na kuwapa Baraka wanaoihitaji katika mapambano na masumbufu yao dhidi ya... Maovu yanayowakabili." – *Matendo ya mitume* Ukr. 532.

**b. Kwa nini ni mhimu kwamba hatuwezi kushupaa na kuipanga njia hii? Efeso. 4:30.**

"Uhasama wa kwanza kwa kiburi cha kiroho huandaa njia ya uadui wa pili, hivyo moyo huwa mgumu, dhamiri isiyo na huruma."

"Kwa upande mwingine, kila nguvu ya majaribu hufanywa nguvu ya majaribu kuwa rahisi kabisa. Kila unapojikana mwenyewe hufanya kujinyima mwenyewe iwe rahisi. Kila ushindi unapopatikana huandaa njia ya ushindi mzuri zaidi kila uadi wa majaribu, kila kujinyima mwenyewe, kila ushindi juu ya dhambi ni mbengu iliyopandwa kwneye maisha milele." – *Ujumbe kwa vijana* Ukr. 96-97.

# *Ijumaa*

*Tarehe 25 Augosti.*

**MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI.**

1. **Wazo gani la uongo huwaongoa Wakristo wengi wenye kujidai kwenye ufedhuli?**
2. **Nawezaje kutambua iwapo kiwango change cha toba ni cha kina?**
3. **Nawezaje kuwa na uhakika kwamba mapenzi ya Mungu halisi ni kunisaidia mimi niweze kushinda makosa yangu?**
4. **Ni mda kiasi nautumia kulinganisha shuhuda na vitabu vingine?**
5. **Elezea mbinu amabyo Mungu huvutia sisi kupanda mbengu kwa ajili ya uzima wa milele.**

## Sadaka ya Sabato ya kwanza Ni kwa ajili ya makao makuu ya Misheni – Fiji.




Jamhuri ya Fiji ni kundi la Visiwa vya Kivolcano katika Kusini mwa Bahari ya Pasfici ni kilomita 4, 450 Kusini Magharibi mwa Honolulu na Kilomita 1, 770 Kaskazini mwa nchi ya Newzland visiwa 332 vinatengeneza Bahari yenye visiwa vidogo vidogo takribani visiwa 106 vina makazi ya kudumu. Fiji hufurahia hali ya hewa ya joto, fukwe zenye mchanga, uoto wa asili wa mimea, matunda tele, mboga za majani na mazao ya mizizi. Fiji inakadiriwa kuwa na wakazi 903, 207, iliyoundwa na wafijiansi asilia (Itaukei) kabila kuu ni Wamelanesiani na wapolinesian ambapo wanatengeneza mchanganyiko wa 56%, wahindu wa fijiani wao wako 45% na jamii nyingine wao wako 7%. Lugha yao Rasmi ni Kiingereza, Kifijiani na Kihindi kinaongewa na wengi. Nyakati zilizopita Fiji ilifahamika kwa ulaji wa nyama za binadamu, wenye kufanya mazoezi kwa kiwango kikubwa kama alama yao kuu ya ubora. Mapema kabisa zama za Mkristo nchini Fiji aliyeacha alama, ni kuwasili kwa dini ya wafuasi wa Weslei wamishionari ambao waliingia mnamo mwaka 1935. Injili ilisambaa kwa upesi na kutokomeza matendo maovu ya ulaji wa nyama za binadamu na uchawi. Siku hizi idadi kubwa ya wananchi ni wafuasi wa dini ya Kikristo, ambapo asilimia 45% ni waprotestant. Asilimia 27.9% ni wahindu. Ambapo asilimia 10.4% ni dini nyingine. Roman Catholic wao ni asilimia 9.1% waislamu wako asilimia 6.3%. Dini ya Wakalasinga wao ni asilimia 9.1% na wasio na dini kabisa (wapagani) wako asilimia 0.8%.

"Ujumbe wa matengenezo uliingia kupitia Pwani za Fiji mnamo mwaka 1974 pale Wamisionari walipotembelea Fiji na walibatiza watu wane (4). Ilipofika mwaka 1997 kazi iliimarika ambapo zaidi ya watu 30 walibatizwa ukuaji umekuwa ukiendelea. Japo umaskini ni jambo la duniani hapa. Waumini wa hapa wanayochangamoto ya kueneza Injili na kuwafikia wanaovutiwa katika visiwa vikuu, nchi kavu, mijini na visiwa vya mbali."

"Tumepata Robo heka tuliyoimiliki mwaka 2015 na kujenga ukumbi mdogo mahali ambapo tulikuwa tukiabudia, zingatia na ukuaji wa washiriki wetu. Hitaji letu kuu kabisa wakati huu tunahitaji nyumba ya kuabudia, ofisi pana kwa ajili ya makao makuu, na kwa ajili ya usambazaji na uzalishaji wa vitabu vya kihistoria. Tunaomba kwa bidii sana Bwana aweze kugusa moyo wako uweze kuitikia mahitaji ya hapa Fiji. Hakika Baraka zitakujia ukitoa kwa ukarimu, kwamba makao makuu yasimame kama kumbukumbu ya utukufu wa Mungu"Toeni nanyi mtapewa, kipimo cha kujaa na kushindilia na kutikisa hata kumwagikia, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu, kwa maana kipimo kile kile mpimacho ndico mtakachopimiwa (Luka. 6:38) tunawashukuruni nyote kwa kuendeleza wema wenu na ukarimu.

*Ni ndugu na dada zenu kutoka Misheni ya Fiji.*

# Kufanya kazi kwa ajili ya Bwana.

**Enendeni ulimwenguni makahubiri injili kwa kila kiumbe. {Marko 16:15}.**

“Wale wanaokesha kwa ajili ya Bwana wanajitakasa nafsi zao kwa kuutii ukweli.Pamoja na bidii.kwa sababu wanafahamu fika kwamba Bwana wao yuko mlangoni.Juhudi zao zitaamushwa ili kushirikiana na mbingu ktk shughuli ya wokovu wa wanadamu′′-*Tumaini la vizazi vyote* ukr 634.

**Imependekezwa kujifunza: shuhuda ya 2 ukr 189-199.**
**Ibid vol 2 ukr 404-410.**

## *Jumapili* *Tarehe 27 Augosti.*

**1. WATENDAKAZI PAMOJA BWANA WA MABWANA.**

**a. Ni juu ya msingi gani k wa kila mkristo mwaminifu- awe mume, mke, aliyeoa au kuolewa, hajaoa, Tajiri, Maskini, wa umri wowote au kabila lolote- wakiamua rasmi kushuhudia kwa ajili ya Bwana na mwalimu wao Yesu kristo? Yohana 15:16, Galatia 3.27-28.**

′′Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe′′(Marko 16:15) ni agizo la Yesu kwa wafuasi wake. Si kwamba wote wameitwa wawe wachungaji au watumwa ktk utaratibu wa Neno bali wote wawe watenda kazi pamoja naye kwa kutoa“Habari njema”

Kwa wanadamu wenzao.kwa wote wakubwa kwa wadogo, wasomi na wasiosoma, wazee kwa vijana, Agizo limetolewa′′-*Elimu* ukr 264.

′′Wakati mwingine naifikiria miji ambayo kazi imefanyika kidogo sana, ambapo kuna maelfu mengi ya maonyo, waonywe kuja kwa mwokozi upesi. Natamani kuwa na nguvu ya kuona wanaume na wanawake wakienda mbele ktk kazi ya Roho mtakatifu wakijaa pendo la kristo kwa ajili ya nafsi zinazo angamia′′-*Uinjiristi* ukr 69.

**b. Kundi gani halisi linahusika pamoja kwenye eneo maalumu la kufunga kazi ya injili? 1Yohana 2.14.(Sehemu ya pili Nusu)**

## 2. KUJIWEKA WAKFU KWA AJILI YA UJUMBE WA LEO.

**a. Umuhimu gani maalumu hufanya injili ya milele iwepo ktk wakati wetu? Muhubiri 12.13-14 Ufunuo 14.6-7.**

″Utangulizi wa hukumu ni tangazo la kurudi kwa Yesu mara ya pili kuwa ku karibu sana. Tangazo hili huitwa injili ya milele, hivyo huhubiri-wa kurudi kwa Yesu mara ya pili tangazo la ukarimu wake limeonyesha ni sehemu muhimu sana ktk ujumbe wa injili;*-Vielelezo vya mafundisho ya kristo ukr* 227, 228.

**b. Jina moja linalohusishwa kwa karibu na ujumbe wa marejeo-na ukweli ni kwamba hutusaidia sisi kufahamu lilivyo bora, Rumi 12.1. 1Thesalonike 5:23.**

″Matengenezo ya afya ni moja ya tawi la kazi kuu ambalo linawafanya watu wa Mungu wafae kwa ujio wa Bwana. Lililofungwa karibu pamoja na ujumbe wa malaika wa tatu kama mkono ulivyo pamoja na mwili′′*-Mashauri juu ya Afya* ukr 20, 21

″Injili na kazi ya umishonari wa dawa asili hutangulizana pamoja.Injili inakwenda pamoja na kanuni za matengenezo ya kweli ya afya………… Tunawasilisha mbele za watu kanuni za kweli za matengenezo ya afya, kwa kufanya yote ktk nguvu zetu ili kuwaongoza watu waume kwa wanawake waone ulazima wa kuwa na kanuni hizi na kuzitenda; *-Mashauri juu ya chakula na kiasi* ukr 442.

**c. Kitu gani humchochea muumini kusambaza ujumbe wa maa-jabu ya wokovu? 2Wakorintho 5:14-15**

“Upendo wa Yesu utadhihirishwa ktk kutamani kufanya kazi kama alivyofanya kazi kwa ajili kuubaliki na kuuinua ubinadamu.Utawaongoza kwenda kwenye upendo, wema, na huruma, kuwaelekea viumbe vyote kwa uangalifu wa Baba yetu wa Mbinguni…………

“Hakuna kwa sasa anayeweza kwenda kristo bila kuzaliwa mara ya pili moyoni mwake, afanye tama ya kuwajua wengine ambao ni marafiki wa thamani aliowapata ndani ya kristo, ukweli unaotakasa na kuokoa ha-uwezi kufungiwa nje ktk mo yo wake.′′*-Hatua za kristo* ukr 77-78.

## 3. KUJAZWA BURE

**a. Ni ushauri gani hubeba nguvu tofauti kwa ajili yetu ambao tunaishi ktk siku za mwisho? 1Thesalonike 5:1-2; 6-8.**

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

″Hebu asipatikane ndani yetu anayelala lindoni, asiwepo anayesema moyoni mwake au kwenye kazi zake″Bwana wangu amekawia kurudi kwake″Hebu ujumbe wa kurudi kwa kristo upesi utangazwe kwa maneno ya sauti ya onyo la bidi. Hebu tuwashawishi manaume na wanawake kila mahali watubu waikimbie ghadhabu inayokuja. Hebu tuwafufue kwa matayarisho ya haraka, kwa maana hatujui hata kile kidogo kilicho mbele yetu. Hebu wachungaji na washiriki wa kawaida waende mbele kwenye mavuno yaliyokomaa;-*Maranatha* ukr 106.

“Upendo ni kiini cha utakatifu.Haijalishi kujidai, hakuna mwanadamu kwa ndugu zake.Lakini kamew hatuwezi kumilikiwa na roho hii kwa kujaribu kuwapenda wengine.Kinacho

Hitajika ni upendo wa kristo moyoni.Wakati nafsi inapounganishwa ndani ya kristo″- *Vielelezo vya mafundisho ya kristo* ukr 384.

**c. Unapaswa kufanya nini iwapo hujisikii Uaminifu au kuhisi Uaminifu, Kama shauku ya ujumbe huu unaijua inavyopaswa kuwa?1 Yohana 4.20-21. Ufunuo 2.2-5, 3.18-19.**

______________________________________________________________

______________________________________________________________

“Tunahitaji ujumbe wa kipindi cha kanisa la Loadikia. Umeacha upendo wako wa kwanza. Kuna ugumu na uvuguvugu omba huruma kwa ajili ya wachache. Kamwe hilo halitakuwa jibu duniani.Tunatafuta na kuokoa kile kilichopotea.Lazima tuwe na Roho ya msaidizi wa kweli, Roho wa kristo″-*Manuscript Releases* vol 9, 61.

“Roho kwenye uzoefu wako wa kwanza, wakati wa Roho yako ilipokuwa imejaa upendo kwa ajili ya mwokozi.Kusanya ndani ya moyo wako utii wa imani ambao hufanya kazi kwa upendo na utakaso wa nafsi utii wa sheria ya Bwana humfanya mtu awe safi, Mtakatifu, asiye na hitaji au kasoro″-*The Review and Harald* 24, feb 1903

“Kuna tumaini kwao wote ambao watausikia na kutubu matendo yao maovu″-*Manuscript(Releases)*Vol, 11 ukr 216.

## 4. UTUKUFU WA MUNGU ULIO WAZI.

**a. Wito gani wa saa, Na tuta uitikia kwa namna gani? Isaya 56:1-8**

″ Bwana sasa anao wito juu ya kanisa lake duniani liamuke kutoka kwenye hali ya kukosa nguvu ambayo shetani ameileta juu yao, nawatimize kazi iliyoteuliwa juu yao ya kuuangazia ulimwengu…………..

″Dunia ya leo inalilia hitaji la ufunuo wa Yesu kristo ndani ya watu wake watakatifu.Mungu anataka kwamba wasimame mbele ya ulimwengu watu watakatifu.Kwa nini?

Ni kwa sababu dunia inaokolewa na Nuru ya injili ya kweli, kadri ujumbe wa kweli, kadri ujumbe wa kweli ambao unawaita watu watoke kwenye giza waingie kwenye Nuru ya maajabu ya Mungu umetolewa pia kwa kanisa na unalifaa kanisa, maisha ya washiriki wake yatakaswe na Roho wa kweli, watoe ushahidi wa kujion ea wenyewe ukweli wa ujumbe uliotangazwa″- *Review and Herald,* 31 machi 1910.

**b. Elezea mbinu za kristo ktk kufanya kazi ya kuokoa Nafsi. Luka 14.23 Yohana 4.27**

“Bwana anatamani kwamba Neno lake la Rehema liende kila nyumba na kila nafsi .

“Sehemu kubwa ya kazi hii itakamilishwa na watu watendakazi. Hii ndiyo kanuni ya Yesu Kazi yake kwa sehemu kubwa ilifanywa kwa mahojiano ya mtu binafsi. Alikuwa mwaminifu kujali usikivu wa mtu mmoja na kupitia kwa mtu huyo ujumbe ulienea kwa watu maelfu ;- *Vielelezo vya mafundisho ya kristo*.uk 229.

**c. Kwa nini Roho anahitajika sana ktk kufanya kazi kwa ajili ya Mungu? 2Wakorintho 12.15**

″Jifunze maana ya Mmishonari wa kristo wa kweli: Mtu yeyote akitaka kunifuata ajikane m wenyewe auchukue msalaba wake, kisha anifuate″Marko 8:34. Mfuate kristo, kama maneno haya, siyo kwa hila au kwa kinyongo.Yesu anataka wanafunzi wake wamfuate kwa ukaribu ktk hatua zake, wadumu kama yeye alivyoshinda. Anasubiri kuona wafuasi wake wakifunua Roho ya kujitoa kafara wenyewe“-*Shuhuda ya 8* ukr 209.

## *Alhamisi* — *Tarehe 31 Augosti*

### 5. UPENDELEO MKUBWA

**a. Kwa namna gani kila mmoja wetu anaweza kushiriki Roho ya kukoa, na jambo gani linapaswa liwe Nia yetu ya dhati na maombi? Rumi 10:13-17 Luka 11.13**

---

---

″Tunahitaji juhudi kubwa zaidi kwa sababu ya kristo.Ujumbe wa dhati wa ukweli mzito ungekuwa umetolewa pomoja na ubora wa hali ya juu ambapo ungewavutia wamisionari kwamba Mungu anafanya kazi kupitia juhudi zetu, ambaye zaidi ya hapo ni chanzo chetu cha nguvu iliyohai″- *Uinjilisti* uk 697.

"Baadhi ya akili zimeongozwa kuacha ukweli wa leo na kutopenda biblia takatifu kwa sababu ya kusoma vitabu vingine vinavyosisimua akili, wengine wamejaa mahangaiko kwa ajili ya vyakula, vinywaji na mavazi. Wengine wanatazamia kuja kwa Bwana kuko mbali mno. Miaka michache iliyodhaniwa imezidi kuwa mingi walivyotarajia wao. Kwa hiyo wanafikiri kwamba itaendelea kukawia zaidi, kwa njia hiyo mioyo yao inautupilia mbali ukweli wa leo, na kufuata mambo ya dunia. Katika mambo hayo naliona hatari kubwa, kwa maana ikiwa akili inafuata mambo mengine, na kuufungia nje ukweli wa leo, haiwezekani kuwekewa muhuri wa Mungu aliye hai juu ya paji za uso wetu. Naliona kuwa wakati wa Yesu kukaa katika chumba cha patakatifu pa patakatifu ulikuwa unakaribia kuisha na kwamba wakati huo ungeendelea kwa mda mfupi tulio nao sisi tunapaswa kuutumia kwa kuichunguza Biblia ambayo ndiyo itakayotumika Ktk Hukumu siku hiyo ya mwisho.

"Ndugu wapendwa na Dada zangu, acheni Amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu kristo vidumu ktk fikra zenu daima na ving`oe mawazo na mifadhaiko ya kidunia ndani yenu.

Yatafakarini hayo daima mlalapo na muamkapo.Muishi na kutenda mkionyesha kabisa marejeo ya mwana wa Adamu.Wakati wa kutiwa muhuri ni mfupi sana kitambo tu kazi hiyo itakwisha″-*Maandiko ya Awali* uk 58.

## *Ijumaa* — *Tarehe 01 Septemba*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI.

**1. Kwa nini hayupo aliye na udhuru wa kuhusu kushiriki ukweli wa leo na wengine?**

**2. Kwa nini sisi tunaifahamu"Injili ya milele?**

**3. Kwa nini ujumbe wa Loadikia unahitajika wakati unasimuliwa kwa uko nje na (Fasheni).wakati.**

**4. Nani ameshasababisha ulimwengu kuwa na mashaka juu ya ujumbe wetu?**

**5: Ni mawazo gani Ninaweza kuyatupa nje kabisa na Akili zangu, kuweka sehemu safi zaidi kwa ajili ya ukweli?**

**Somo la 11** *Sabato ya Tarehe 09 Septemba 2017*

# Busara za Mipango ya Mungu.

**Bwana hakawii kuitimiza ahadi zake kama wenginewanavyokudhania , bali hutuvumilia maana hapendi mtu yeyote apotee, bali afikiri toba (2 petro 3.9)**

Ni ukweli kwamba wakati umeendelea sana kuliko tulivyotarajia ktk siku za mwanzoni wa ujumbe huu.Mwokozi wetu hajaonekana upesi kama tulivyotumaini.Lakini je, Neno la Bwana limeshindwa? Hapana ingekumbukwa kwamba ahadi na wa Mungu ni kama ilivyopang wa''- *Uinjilisti* ukr 695.

**Imependekezwa kujifunza: Jumbe zilizoteuliwa vol, 1. ukr 185-192.**
**Maandiko ya Awali ukr 56-58, 69-73, 111-114**

## *Jumapili* *Tarehe 03 Septemba.*

### 1. HURUMA ZA MUNGU.

**a. Eleza lengo la Mungu kwa ajili ya kila mwanadamu aliye mumba. 1 Timotheo 2.3-6**

''Mungu ni mvumilivu, maana hapendi mtu yeyote apotee, lakini uvumilivu wake unakikomo, Pale uvumilivu unapopita hana muda wa majaribio ya mara ya pili, Ghadhabu yake itakwenda mbele kuangamiza Pasipo dawa'' –*The Youth's Instructor*.28, machi 1905.

**b. Kwa nini Bwana asingewaruhusu watu wa Israel moja kwa moja kwenda kumiliki nchi ya Ahadi? Ebrania 3.7-11**

''Mungu hakutaka watu wa Israel watangetange jangwani kwa mda wa miaka Arobaini, aliwaahidi kuwaongoza moja kwa moja hadi kwenye nchi ya Kanaani, na kuwafanya wawe watakatifu, wenye afya, watu wa furaha; Lakini kwa mara ya kwanza walihubiriwa hawakuingia kwa sababu ''Hawakuamini'' (Ebrania 3.19)''-*Uingilisti* ukr 696.

## 2. SABABU ZA KUCHELEWA ZILIZOWAZI.

**a. Kama waumini, Ni hatari gani inatukabiri siku hizi? Ebrania 3.12-13**

''Kwa muda wa miaka Arobaini hawakuamini, Manung'uniko na Uasi uliifungua Israel wa zamani wasiingie ktk nchi ya Kanaani. Dhambi ileile imewachelewesha Israel wa leo kuingia ktk Kanaani ya Mbinguni. hili lilifanya ahadi ya Mungu waikose.Uasi wa kutoamini, kuupenda ulimwengu, kutojitakasa Ugomvi kati ya watu wanaoshuhudiwa na Bwana ametutunza ktk ulimwengu huu wa dhambi, na masikitiko ya miaka mingi''-*Uingiristi* ukr 696.

**b. Kwa nini inaonekana kwamba Bwana anachelesha ujio wake? 2 Petro3.9**

''Usiku wa huzuni ni mrefu, lakini asubuhi inacheleweshwa ktk rehema kwa sababu kama Bwana angekuja wengi wangekutwa hawajawa tayari. Siyo mapenzi ya Mungu watu wake waangamie, wamesababisha acheleweshe kwa mda mrefu'' -Ibid ukr 694.

''Kwa ajili ya Rehema kwa ulimwengu Yesu amecheleweshа kuja kwake ili wenye dhambi waweze kupata nafasi ya kusikia onyo na kutafuta kimbilio kwake kabla ya kumwagwa kwa Hasira yake kali na Ghadhabu ya Mungu''-*Pambano kuu* ukr 458.

**c. Nani yumo ktk nafsi ya kufarijiwa sana ktk huzuni na gi za la kiroho linaloifunika sayari yetu ? 2 Petro 3.11-12, 1 Wakorintho 15:34.**

''Bwana ktk Huruma anatafuta kuangaza ufahamu wa wale ambao kwa sasa wanajigongagonga kwenye giza la makosa. Amecheleweshа hukumu zake juu ya dunia isiyotubu, ili kwamba nuru yake iweze kuenea na kuokoa kile kilichopotea''- *Review and Herald 31*, machi 1910.

**d. Kwa namna gani tunaweza kuharakisha kuja kwa Yesu? 2 Wakor 5:20 Mathayo 24:14**

''Kwa kuihubiri injili ulimwenguni ni nguvu yetu ya kuharakisha marejeo ya Bwana wetu, siyo kutazama tu bali ni kuiharakisha siku ya Bwana''-*Tumaini la vizazi vyote,* ukr 633.

## 3. NGUVU ZA ZIADA KWA AJILI YA KUONGEZA KASI.

**a Kwa namna gani tutaigawana injili kuifikisha kwenye kilele chake katika siku za mwisho? Zakaria 10:1, Yoeli 2.23.**

''Kazi kuu ya injili haitafungwa kwa udhihirisho hafifu wa uwezo wa Mungu, bali kwa udhihirisho mkuu –kama ilivyobainishwa wakati wa kufunguliwa kwake. Unabii uliotimizwa ktk kumwagwa kwa mvua za vuli wakati wa kufunguliwa kwa injili, zitatimizwa tena kwa kumwagwa mvua za masika kwa kufungwa kwake'-*Pambano kuu* ukr 611, 612.

**c. Nini kinahitajika kuaminiwa na kutolewa kwa mvua ya masika –kumwagwa kwa Roho wa Mungu bila kikomo? –Yoel 2.17, 18. Matendo 3.19-20.**

''Niliona kwamba hayupo atakayepata ''Burudisho''isipokuwa awe amepata ushindi wa kila dhambi imzingayo. Juu ya kiburi, ubinafsi, kuupenda ulimwengu, n a juu ya kila Neno na tendo baya. Kwa hiyo, tunapaswa kumsogelea Bwana zaidi na zaidi na kufanya maandilizi yaliyo muhimu ili kutuwezesha kusimama kwenye vita ktk siku ya Bwana. Hebu sote tuangalie kuwa Mungu ni m takatifu , hayupo awezaye kuishi mbele zake ispokuwa tu walio watakatifu'- *Maandiko ya Awali* ukr 71.

''Moyo lazima usafishwe kwa kujitenga na kila aina ya uchafu, utakaswe kwa ajili ya makazi ya kukaliwa na Roho. Ni kwa kukiri na kuziacha dhambi, kwa maombi ya bidii na kujiweka wakfu wenyewe kwa Mungu, ambapo hata wanafunzi wa hapo awali walijiandaa kwa ajili ya kumwagiwa Roho mtakatifu ktk siku ya Pentekoste. Kwa kiwango hicho hicho tu lazima kifanyike sasa''-Shuhuda za watendakazi ukr 507.

''Kwa ajili ya ubatizo wa Roho wa Roho mtakatifu kila mtendakazi angepaswa kumlilia Mungu.Makundi yangekusanyika pamoja kwa ajili ya kuomba msaada maalumu, na hekma za kimbingu, ambapo waweze kupanga na kutenda kwa Busara.Hasa watu wangemwomba Mungu awabatize watumwa wake kwa ubatizo wa Roho m takatifu.

''Uwepo wa Roho mtakatifu n dani ya watendakazi wa Mungu, watatoa uwasilisho wa kweli, nguvu ambayo watu wote wenye heshima duniani na watukufu hawawezi kuitoa.Roho hutupatia nguvu ambazo hutumika kutuimarisha ktk nafsi ktk kupambana na kila dharura, katikati ya jamaa wasio wema, chuki ya ulimwengu, ili watambue wenyewe makosa yao na kasoro zao''- *Shuhuda ya 8* ukr 22

## 4. FAHAMU KILA JAMBO LILIOBORA.

**a. Hata kama tunaendelea ktk maarifa ya Mungu, Ni habari gani Yeye bado huhifadhi Nuru kwa kuizuilia toka kwetu, na k wa nini? Matendo 1.6-7.**

''Mungu hajatufunulia sisi mda na wakati ambapo ujumbe huu utakuwa umefungwa, au ni lini majaribu yatakuwa yamekoma... sisi hatupaswi kujua kile ambacho kimefanywa siri ktk mashauri ya Mungu mwenyezi''- *Ujumbe ulioteuliwa* vol, 1. ukr191 .(1sm ukr191)

''Hakuna ujumbe tena mara ya pili kwa watu wa Mungu ambao utakuwa wa kulingana na wakati au mda. Hatuna ufahamu wa uhakika wa muda wala wa kumwagwa kwa Roho mtakatif au kule kuja kwa Yesu...

''Bwana alinionyesha kwamba, Ujumbe lazima uhubiriwe na kwamba tusiwe wakutojali wakati, kwa maana wakati hauwezi kuwa jaribu tena. Naliona kwamba baadhi walikuwa wamepata msisimuko wa furaha ya uongo, waliinuka kuhubiri juu ya wakati, kwamba ujumbe wa Malaika wa tatu unaweza kusimama wenyewe juu ya msingi wake wenyewe, Na kwamba hauhitaji muda wa kuuelekeza, Tena utakwenda kwa nguvu kubwa na uwezo na utafanya kazi yake, na utakatishwa kwa ajili ya wenye Haki.''-Ibidi ukr 188.

**b. Kwanini tunapaswa kutosheka na hekma za Mungu ktk tatizo hili? Kumbukumbu 29:29.**

''Kutangaza muda maalumu kwa ajili ya hukumu, ktk kuhubiri ujumbe wa malaika wa kwanza, ulikuwa umeagizwa na Mungu. Mahesabu ya vipindi vya unabii ambavyo ujumbe huo ulilenga, uliwekwa kumalizika kwa siku 2300 ktk majira ya kiangazi mwaka 1884, husimama pasipo kutiliwa shaka. Jitihada za kutafuta kurudia tarehe mpya ya kuanza na kumalizika kwa vipindi vya unabii na sababu zilizoridhisha za kulazimisha kuchukua na kukubaliana na msimamo wa hii, siyo tu kwamba hupotosha akili kutoka kwenye ukweli wa leo, bali pia kubeza na kutweza juhudi zote za kufafanua na kuuelezea unabii. Kuendelea kuweka mda maalumu tena, wa tukio la kurudi kwa Yesu mara ya pili na jinsi inavyozidi kufundishwa tena na tena, kunalifanya litimize makusudi ya shetani kwa ufanisi mkubwa zaidi. Baada ya kupita kwa wakati shetani alichochea dhihaka na dharau kwa watetezi wake, na hivyo ndivyo ilileta lawama na shutuma juu ya harakati kuu za mwaka 1843 na mwaka 1844. Wale wanaoendelea ktk kosa hili hatimaye wataiweka tarehe ya kuja kwa Yesu mbali sana huko mbele. Kwa hiyo wataongozwa kutulia ktk usalama wa uongo (Feki) na wengi wao hawatatambua kabisa hadi hapo watakapokuwa wamechelewa kabisa; - *Pambano kuu* ukr 457.

## *Alhamisi* **_Tarehe 07 Septemba._**

### 5. TANGAZO LISILOCHELEWA.

**a. Tangazo gani linaharakisha upesi kutangaza kutoka mbinguni, Na kwanii hili jambo ni la muhimu kwa kila binadamu? Ufunuo 22.11**

---

---

''Wengi hawatambui utaratibu uwapasao ktk maisha ili waweze kusimama mbele za Mungu bila kuwa na kuhani mkuu ktk hekalu wakati wa Taabu.Wale wanaopekea mhuri wa Mungu aliye hai na kulindwa ktk wakati wa Taabu, Lazima waaksi sura ya Yesu kwa ukamilifu.

''Naliona kwamba wengi walikuwa wanapuuzia maandali muhimu yanayohitajika na huku wakitazama ''wakati wa kurudishwa'' na mvua ya masika ili kuwafanya wafae kusimama ktk siku ya Bwana na kuishi mbele zake.Ooh! Namna gani nilivyowaona wengi

Wakiwa hawana kimbilio wakati wa Taabu! walikuwa wamepuuzia maandalizi muhimu;

Kwa hiyo wasingeweza kupokea Burudiko yaani mvua ya masika amb ayo ingewafanya wafae kuishi mbele za Mungu mtakatifu.Wale wanaokataa kuchongwa na manabii na wale wanaoshindwa kusafisha mioyo yao kwa kutii ukweli wote, na kujidhania kuwa wao ni wema zaidi, kumbe wako kinyume.Wakati wa kipindi cha mapigo ndipo watakapo tambua walistahili kuchongwa na kujengwa ktk unyoofu.Lakini hakutakuwa na wakati au muda wa kufanyiwa jambo hilo, wala mwokozi hatokuwepo wa kuwaombea mbele za Baba''... (Ufunuo 22.11 imenukuliwa) *Maandiko ya Awali* ukr 71

''Wale ambao wanaishi duniani wakati wa upatanisho na maombezi ya kristo yatakapokuwa yamekoma ktk Hema Takatifu ya mbinguni juu yao, sasa watasimama mbele za Mungu mtakatifu pasipo mpatanishi. Mavazi yao lazima yasiwe na doa lolote, Tabia zao lazima zitakaswe ziwe safi kwa damu yake iliyomwagika. Kwa njia ya Neema ya Mungu na juhudi zao wenyewe na bidii, Lazima wawe washindi ktk vita vya uovu; *-Review and Hend. 17*, January 1907.

## *Ijumaa* **_Tarehe 08 Septemba._**

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI

**1. Kwa nini tunapaswa kujifunza ktk kucheleweshwa kwa waisrael kuingia kanaani?**

**2. Nani ambaye ni kinara tena Mharifu wa siku hizi anayechelewesha kuingia ktk kanaani ya Mbinguni?**

**3. Kwa nini mvua ya masika inahusishwa ktk takio hili, Na kitu gani kitaiwezesha kuja?**

**4. Elezea kusudi kuu la mvua ya masika na muda wake.**

**5: Nahitaji nini kwa Mungu aweze kuniamini pamoja na burudiko hili?**

# Kuenea kwa kilio kikuu.

**''Nitamimina maji juu yake aliye na kiu na vijito vya maji juu ya mahali pakavu, Nitamwaga Roho wangu juu ya uzao wako, na Baraka yangu juu yako;-(Isaya 44:3)**

''Kwanini hatua hasira na kiu kwa ajili ya zawadi na karama ya Roho kwa maana hii ndiyo njia ambayo tunapokelea nguvu?kwa nini hatuongei juu yake, hatuombi juu yake, wala hatuhubiri juu yake? *shuhuda ya 8* ukr 22.

**Imependekezwa kujifunza: Shuhuda ya 1 ukr 179-184.**

**: Shuhuda ya 8 ukr 14-23.**

## *Jumapili* *Tarehe 10 Septemba.*

### 1. MAFUNDISHO YA MATENGENEZO YENYE NGUVU.

**a. Ni unabii gani hubeba ishara maalumu ktk kujitayarisha kukutana Bwana? Malaki 4:5.**

''Katika kizazi hiki, kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili ktk mawingu ya mbimguni, Mungu anawaita watu ambao watawaandaa watu kusimama imara ktk siku ya Bwana; - *The SDA Bible commentary* , vol.4 ukr 1184.

**b. Kwa namna gani Yesu aliwaelezea wanafunzi wake ombi la kwanza la unabii huu, na kwa jinsi gani hili husimuliwa na kuhusiana na kazi yetu kwa sasa? Mathayo 17:11-13.**

''Wale ambao wanaandaa njia kwa ajili ya kurudi kwa Yesu mara ya pili, wana mwakilisha Eliya mwaminifu, kama vile Yohana mara ya kwanza. Somo kuu la matengenezo lihamasishwe, na akili za wengi ziamushwe, kuwarudisha watu wa Mungu watoke kwenye Ibada zao za sanamu, somo la kiasi ktk mambo yote limefungwa na kuunganishwa na ujumbe,

Waache ulafi wao, na ushupavu wao ktk mavazi na mambo mengine'- *shuhuda ya 3* ukr, 62.

## 2. KUIANDAA NJIA YA BWANA.

**a. Ni ujumbe gani wenye nguvu Yohana mbatizaji alihubiri, na kwanini inafaa kufanya kama vile? Luka 1.16-17 Mathayo 3.2, 8.**

---

''(Yohana mbatizaji) aliwaona watu wake wakiridhika, na wamelala ktk dhambi zao. Ujumbe aliokuwa wamepewa na Bwana ulipaswa kuwaamusha na kuwafanya wawe na taharuki kwa sababu ya uovu wao mkuu. Kabla mbegu ya Injili haijapandwa kwao, Laizma kwanza mioyo yao ilainishwe, udongo wa moyo uwe laini. Kabla hawajatafuta uponyaji kutoka kwa Yesu, lazima waamushwe kwanza waione hatari inayo wakabiri kutokana na majeraha ya dhambi.

''Mungu hajatuma wajumbe ili kuja kumfurahisha mwenye dhambi, hajatoa ujumbe wa amani ili kuwatuliza eti wakae bila wasiwasi, bali huwa onyesha utisho wa kuzidi juu ya dhamiri ya mkosaji, na kuwafanya watu waone haja ya kutubu na kuepuka mishale ya Hukumu; - *Tumaini la vi zazi vyote* ukr 103, 104.

**b. Toa mfano wa namna Eliya na ujumbe wake ulivyorejeza maisha ya familia –ukilinhganisha na ulivyotolewa ktk kazi ya Yohana mbatizaji. Malaki 2.13-17. 4:6**

---

''Yohana alitambua ukweli kwamba Herode alikuwa karibu amuoe mke wa ndugu yake, wakati alikuwa bado hai. Kwa uaminifu alimwambia Herode kwamba hiyo siyo Haki; - *Maandiko ya Awali* ukr 154.

**c. Ni sifa gani ''za nguvu na Roho wa Eliya''na Ni nani ambaye anahubiri ujumbe huu siku zetu? 1 Wafalme 18:17-18, 21. Ufunuo 12.17.**

---

---

''Wengi hawathubutu ama kujaribu kuukemea uovu, kwa sababu ya sadaka au umaarufu. Inachukuliwa siyo vyema kukemea dhambi. Mtumishi wa Mungu kamwe hawezi kuruhusu Roho yake kujiunga na kemeo ambalo linahitajika kutolewa, lakini akiwa chini ya wajibu muhimu kwa kuwasilisha neno la Mungu pasipo woga wala upendeleo, lazima aitaje dhambi kwa jina (kama ilivyo). Wale ambao kwa uzembe wao au kutojali kwao wameruhusu jina la Mungu kupuuzwa na kudharauliwa kwa ushuhuda wa watu wake, wanahesabika kuwa ni wavunja sheria wahalifuwanaandikwa ktk vitabu vya kumbukumbu vya mbinguni kama washiriki wa matendo yao maovu kabisa;-*Alama za Nyakati* 21 Aprili

## 3. KAZI YA MWISHO

**a. Ni wito gani mfupi wa haraka wa saa? Ufunuo 14;6-13. Ufunuo 18:1-4**

''Katika kufunga kazi ya Mungu duniani kiwango cha sheria yake itatukuzwa. Dini za uongo zitaenea pote, Maovu yanaweza kuenea pote kila mahali, upendo wa wengi utapoa, msalaba wa Kalvari utaweza kukosa thamani ya kutambuliwa giz nene kama nguo nyeusi inayofunika jeneza la maiti itaweza kuenea kila mahali, ulimwenguni na majeshi yake unaweza kuipinga kweli, njama juu ya njama zinaweza kufanywa kwa watu wa Mungu, lakini wakati wa hatari kuu Mungu wa Eliya atainua wanadamu ambao ni vyombo vyake, wauchukue ujumbe ambao hautanyamazishwa na kitu chochote. Ktk miji miovu ya dunia, sauti kali ya karpio itasikika. Watu wa Mungu watakanusha kwa Ujasiri mkuu kabisa wa kanisa kujiunga na kuwa na muungano wa Ulimwengu. Kwa bidii kabisa watawasihi watu waume na wanawake watoke ktk njia ya kutukuza siku iliyowekwa na wanadamu, wa je kumwabudu Mungu ktk sabato ya Kweli; - *Wazee na Manabii* uk 186-187.

**b. Mara zote ni jambo gani lazima liwe dhahiri ktk maisha yetu na kauli zetu? Yohana 1.129, 14:2, 2Wakorintho 4:5-7.**

''Mwangaza wa mwisho wa Nuru yenye Rehema na ujumbe wa mwisho wa Rehema kutolewa duniani, ni kufunuliwa kwa tabia ya upendo. Watoto wa Mungu wanaudhihirisha utukufu wake. Ktk maisha yao na tabia zao wenyewe wanaifafanua Neema ya Mungu ambayo ameifanya kwa ajili yao.

''Nuru ya jua la wenye haki linaangaza mbele kwa wenye matendo mema, katika maneno ya kweli na matendo matakatifu" Vielelezo vya mafundisho ya kristo . uk 415, 416.

**d. Hatimaye kazi ya Mungu itakamilika kwa namna gani? Zakaria 4:6; Isaya 28:21.**

''Bwana atatenda na kufanya kazi hii ya mwisho ktk njia iliyo nje kabisa na kawaida ya utaratibu wa mambo ni ktk njia ambayo itakuwa kinyume kabisa na mipango na mitazamo ya wanadamu; -*Uinjiristi* ukr 118.

## 4 JINSI YA KUPOKEA BURUDISHO.

**a. Lazima tufanye nini siku zote kuhusu kutambua ufunguo muhimu kupitia Roho mtakatifu ktk kujazwa kwa nguvu za mvua ya masika? Isaya 57:15.**

''Kutakuwepo na wale miongoni mwetu ambao mara zote wanataka kuitawala kazi ya Mungu, kwa kulazimisha hata ule mwenendo (Harakati za wanamatengenezo).Watakao fanya kazi iende mbele chini ya uongozi wa malaika yule ambaye anajiunga na yule malaika wa tatu ili ujumbe utolewe duniani.Mungu atatumia njia hiyo na kwa njia ya watu wake itaonekana kwamba amechukua hatua ktk mikono yake mwenyewe'- *Uinjiristi* ukr 118.

''Mtu mwenye talanta moja anaweza kufikia daraja ambalo wenye talanta mbili au tano hawawezi kusogea.Mkubwa na mdogo wamechaguliwa kama chombo cha kubebea maji ya uzima kwa wenye kiu.Hebu wale ambao hawajahubiri neno waweke mikono yao kwa mtenda kazi mnyenyekevu na waseme ''Lazima ufanye kazi ktk mfereji huu, Hebu kila mmoja afanye kazi anga lake wenyewe, pamoja na silaha zake, ufanye chochote unachoweza kufanya ktk njia za unyenyekevu wake.Aiongoze mikono yake ktk kazi.Huu sio wakati wa utawala wa kifarisayo. Hebu Mungu afanye kazi kupitia kwa yule anayetamka na kumuhitaji, ujumbe lazima uende ; -*Shuhuda yas ukr 461.*

**b. Kwanini mvua ya masika inatolewa? Kwanini tunapaswa kutiwa moyo kwa motisha wa mitume wa awali? Matendo 1.8, 4:33. Yeremia 30:5-7.**

''Kumbuka kuwa mitume kuja kwenye utimilifu na umoja, Ni pale walipoacha kugombea ukubwa na madaraka ya juu, ambapo Roho mtakatifu alikuwa amemwagwa walikuwa kitu kimoja, tofauti zao zilikuwa zimezikwa...

''Mitume hawakuomba Kwa ajili ya Baraka zao wenyewe, walibeba mzigo mzito wa nafsi...

''Hebu mkristo aache mizozo, ajitoe mwenyewe kwa Mungu kwa ajili ya kuokoa waliopotea, waombe kwa imani Ahadi ya Baraka iliyoahidiwa kwao, itakuja;- Ibid vol 8, ukr 20, 21.

''Kadri ujumbe wa malaika wa tatu unavyosambaa kwa kilio kikuu, na kadri nguvu kuu na utukufu kuwepo kwa kuifunga kazi, watu wachache waaminifu watashiriki utukufu huo. Ni mvua ya masika itakayofufua na kuwatilia nguvu wapiti kwenye wakati wa majaribu; - Ibid Vol 1, ukr 353.

# *Alhamis* 

*Tarehe 14 Septemba*

## 5. FURAHA ILIYO KUU MNO.

**a. Nafasi gani ipo mbele yetu sasa? Tito 2.13 2Wakor 6:1-2**

''Ndugu zangu na Dada fanya mipango yako ifahamu nafasi ya kuzungumza na majirani zako na ushirikiane nao au usome nao baadhi ya vitabu ambavyo vimebeba ukweli wa leo. Waonyeshe kwamba unaona umuhimu ni umuhimu wa kwanza kwa uovu wa nafsi kwake ambaye Yesu kristo alifanya kafara kuu mno.

''Katika kufanya kazi kwa ajili ya Nafsi zinazoangamia umeshirikishwa pamoja na malaika maelfu kwa maelfu na elfu kumi mara elfu kumi malaika wanatungoja kushirikiana na washiriki wa makanisa yetu ktk kuunganisha Nuru ambayo Mungu kwa ukarimu mkuu aliitoa, ili kwamba watu waweze kuwa tayari kwa ujio wa kristo'-*Shuhuda ya 9*, ukr 129.

**b. Elezea matokeo ya ajabu yatakayotokea pale Roho mtakatifu atakapo mwagwa bila kipimo. Zakaria 8:23, Isaya 44:3-4:61.11.**

''Mbegu imekwishapandwa na sasa itakuwa karibu kutoa matunda, vitabu, makabrasha, vijizuu na machapisho mbalimbali yaliyotawanywa na watenda kazi wamishionari yametumika kama mvuto, hata hivyo bado watu wewngi ambao akili zao zilikuwa zimeshawishiwa, wakiwa wamezuiwa kuufikia ufahamu kamili wa ukwelli au kutoa utii kamili.Sasa miale ya Nuru inapenya kila mahali, ukweli unaonekana ktk usahihi wake na watoto wa Mungu waaminifu wanakata kamba zilizokuwa zimewafunga Miunganiko ya kifamilia na mahisiano ya ki-kanisa sasa hayana nguvu za kuwazuia. Ukweli ni wa thamani kuliko mambo mengine yote; - *Pambano kuu* ukr 612.

# *Ijumaa* 

*Tarehe 15 Septemba*

## MASWALI BINAFSI YA KUTAKAFARI.

**1. Uwiano gani uliopo kati ya kazi yetu na ile ya Eliya na Yohana mbati zaji.**

**2. Kwa namna gani matengenezo yanahitajika siku hizi kulingana na sheria kumi?**

**3. Fafanua kiwango cha ubora wa sifa za hao watakaopokea mvua ya masika.**

**4. Ktk msingi gani naweza kuwa niko kwenye hatari ya kukosa fursa hii ya ajabu?**

**5: Kwanini matokeo ya mvua ya masika n furaha ya ajabu ukiyaona?**

# Usiku wa Manane hadi Mapambazuko.

**“Mungu wetu atakuja, wala hatanyamaza, moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote”. (Zaburi. 50:3).**

Yesu analiendesha (wingu) kama mshindi, siyo kama alivyo. Kwamba ni mtu wa sikitiko, ” kunywea kikombe cha aibu na ole, anakuja akiwa mshindi duniani na mbinguni……………. Hakuna kalamu ya mwanadamu inayoweza kuelezea na kuandika tukio hilo, hakuna akili ya mwanadamu anayekufa inayoweza kufahamu utukufu wake.” – *Pambano kuu* Ukr. 641.

**Imependekezwa kujifunza. Pambano kuu Ukr. 618-622, 638-652.**

## *Jumapili* *Tarehe 17 Septemba.*

### 1. WAKATI WA MATUKIO YA MWISHO.]

**a. Elezea mpango wa Kristo kwa ajili yetu kinyume na washetani. Luka. 22.31 Yohana. 9:4.**

---

---

---

“Shetani... anaelewa kwamba kila anayetegemea akili zake potofu hutengana na Kristo na ukweli wake”.

“Wale ambao watashiriki mibaraka ya Uombezi wa mwokozi hawataruhusu chochote kuingilia wajibu wao wa kukamilisha utukufu katika kumcha Mungu” – *Pambano kuu* Ukr. 488.

“Bidii kwa ajili ya Mungu iliwachochea mitume kubeba ushahidi wa kweli kwa nguvu nyingi, je, hatupaswi kuwa na bidii ndani ya mioyo yetu na kutambua kuielezea habari ya Pendo la Mkombozi na kusurubiwa kwake? Je, Roho wa Mungu hawezi kuja leo?, Jibu ni kuwa na bidii katika maombi na kuwajza watu nguvu kwa ajili ya huduma” – *Shuhuda ya 8* ukr. 22.

“Kila nguvu ya mbinguni tunayoazimiwa, itumike katika kufanya kazi tuliyoelekezwa na Bwana kwa ajili ya wale ambao wanaangamia katika makosa. Onyo la ujumbe lisikike pande zote za ulimwengu, bila kuchelewa ukweli lazima uhubiriwe kila kona ya ulimwengu wenye giza. Vikwazo lazima kukutana navyo lakini lazima ushinde. Kazi kubwa ifanyike na kazi hii imekabidhiwa kwa wale ambao wanaujua ukweli wa wakati huu”- *Review and Herald*, 23, November 1905.

## 2. KIWANGO HUONGEZEKA.

**a. Ni lazima tutambue jambo gani kuhusu shirikisho la Roho tatu za uchafu zenye lengo la kubomoa sheria ya Mungu katika kiwango cha kimataifa? Ufunuo. 16:13-14. 1 The Salonike 5:3-4.**

"Kadri pambano linapozidi kuenea sana katika maeneo mapya, na akili za watu kurejeshwa kwenye sheria ya Mungu ilivyovunjwa, shetani alianza kufurukuta. Nguvu iliyokuwepo kwenye ujumbe itawaita wazimu wenye kuipinga. Mapadri, makasisi na wachungaji wa Makanisa watatumia nguvu zote kupita uwezo wa binadamu kuzuia Nuru ile isije ikaangaza juu ya makundi yao. Kwa amri zao watajaribu kila njia kuzuia majadiliano ya maswala hayo muhimu. Kanisa litaomba mamlaka ya serikali mkono wa Dola, na katika kazi hii, wakatholiki na waprotestanti wanaungana"- *Maranatha* ukr. 172.

"Kupitia makosa makuu mawili la Roho haifi na utakatifu wa Jumapili shetani atawaweka watu chini ya udanganyifu wake mkuu. Wakati waanzilishi wameweka msingi wa umizimu, mwishowe wanajenga dhamana ya huruma ya Roma. Waprotestanti wa Marekani watakuwa wa kwanza kunyoosha mikono yao kuvuka shimo la kuzimu kwa mikono pamoja na nguvu ya Rumi, na chini ya mvuto wa muungano huu, nchi hii (Marekani) itakuwa imefuata nyayo za Rumi kwa kugandamiza haki ya dhamiri...

"Upapa, Uprotestanti na watu wa ulimwengu watalipokea taratibu kwa wema pasipo nguvu ya kualzimisha, na wataona waugeuze ulimwengu katika muungano huu muhimu sana watumike katika matarajio ya Milleniamu ndefu." – Ibid Ukr. 190.

**b. Ni mawazo gani ya mtunga zaburi yanweza kutuhakikishia kuwa ni mwangwi wa siku zetu? Zaburi 119:126.**

"Wakati tunaoishi ni wakati unaojulikana kuwa ni mchafu. Hofu ya dini imetupwa mbali, watu wameikataa sheria ya Mungu kama isiyofaa kwa tahadhari yao. Dharau iliyozaidi ya kawaida imewekwa juu ya sheria...

"Wakati kwa sasa wanavuka msitari wa mpaka, na Bwana ameruhusu adui kufanya atakavyo...., ngurumo na kishindo cha Bwana kitasikika juu ya nchi kavu na baharini, kwa ajili ya utukufu wake mwenyewe Mungu akiadhibu uovu. Anakuja haraka, tena upesi kuja kuthibitisha madai ya sheria yake" – *The Review and Herald,* 23 November 1905.

## 3. MLANGO WA MWISHO.

**a. Onyo la jina moja Kristo alilitoa ambalo lina maombi tofauti tofauti katika siku zetu – kadri dalili za mwisho ambazo utume unakamilika. Mathayo. 24:15-19. Je, mambo gani tunapaswa kuzingatia katika saa hizi za mwisho? Ufunuo. 3.11.**

---

---

"Wakati haupo sasa kwa watu wa Mungu kutoa upendo wao au kuweka hazina zao duniani. Wakati hauko mbali, ni lini? Ni kama mitume wa hapo awali, tutalazimika kukimbilia maeneo ya ukiwa na upweke. Kama ilivyozingirwa Yerusalemu na majeshi ya kirumi ilikuwa ishara kwa makundi ya wakristo wa Yudea, hivyo tetesi za nguvu ya madaraka kwa upande wa Taifa letu (Marekani) katika utekelezaji wa kulazimisha sabato ya kipapa litakuwa onyo kwetu. Hivyo basi utakuwa ni wakati wa kuhama katika miji mikubwa maandalizi ya kuondoka kidogo kidogo kwa ajili ya kwenda kuishi katika nyumba za faragha katikati ya milima. Na sasa badala ya kutafuta makazi ya gharama za hali ya juu hapa, tunapaswa kujiandaa kuingia katika nchi iliyobora kuliko ni mbinguni kwa baba. Badala ya kutumia njia zetu wenyewe kwa kujinufaisha wenyewe, tungejifunza namna ya kubana matumizi. Kila kipaji kilichotolewa na Mungu kingetumika kwa ajili ya utukufu wake katika kutoa onyo ulimwenguni. Mungu anayokazi ya kufanya kwa watendakazi wake katika miji. Utume wetu lazima uwe endelevu. Misheni mpaya lazima zifunguliwe. Kuipeleka mbele kazi hii ifanikiwe haitahitaji gharama kidogo, nyumba za ibada zinahitajika mahali ambapo watu wanaweza kukaribishwa kusikia ukweli kwa ajili ya wakati huu. Kwa ajili ya lengo hili jema, Mungu amekabidhi mtaji kwa mawakili wake. Hebu mali yako isiwe kifungo au isikufanye katika makapmuni ya kiulimwengu, kiasi cha kukabana. Tafuta njia ambayo itakuwezesha kuitawala kwa manufaa ya kazi ya mungu wekeza hazina yako mbinguni kabla yaw ewe hujaingia mbinguni" – *Shuhuda ya 5* Ukr. 464, 465.

**b. Katikati ya ole ulio karibu sana, Mungu hutaka tuzingatie mahali gani? Isaya 26:3-4.**

---

---

"Hebu waza juu ya Yesu, yupo mahali patakatifu siyo katika hali ya upweke, bali amezungukwa na elfu kumi mara elfu kumi za malaika watakatifu wa mbinguni wanasubiri wafanye mwitikio wake. Wanamwitikia wanaenda kufanya kazi kwa watakatifu walio dhaifu ambao wameweka matumaini yao kwa Mungu. Wajuu na wa chini, matajiri na masikini, msaada wao ni ule ule unaotolewa." – *Kwa imani naishi* Ukr. 205.

## 4. TUNZA NA KUULINDA MTAZAMO WETU.

**a. Elezea swala halisi la kufa na kupona katika jaribu la mwisho, habari gani kuhusiana na mtume Petro, je, tunajiandaa kila siku kukutana nalo? Ufunuo. 13.11, 15-17, Matendo. 5:29.**

---

---

"Wakati unakuja ambapo watu hawaturuhusiwa kabisa kufanya kazi siku ya Jumapili, bali watajaribu kuwalazimisha watu wafanye kazi siku ya sabato, kujisajiri kwa utunzaji wa Jumapili au kutozwa faini uhuru wao na maisha yao." – Review and Herald 06/04/1911.

**b. Ni ahadi gani ya thamani hufunua wema wa ulinzi wa Baba yetu wa mbinguni katika saa ya kujaraibiwa? Zaburi. 31.19-20, 91.5-7, Isaya.26:20-21.**

---

---

"(Isaya. 26:20 imenukuliwa) ni vyumba gani ambavyo inawapasa wajifiche (watu wa Mungu)? Ni ulinzi wa Kristo na Malaika watakatifu. Watu wa Mungu kwa wakati huu hawako sehemu moja. Wapo katika makundi na sehemu mbalimbali za ulimwengu"

"Niliwoana watakatifu wakiiacha Miji na Vijiji, wakishirikiana pamoja katika makundi wakiishi mahali pa upweke. Malaika waliwapa chakula na maji, wakati waovu wakihangaika kwa njaa na kiu."

"Wakati wa usiku mwonekano wenye mguso wa pekee ulipita mbele zaungu. Ilionekana kuwa kulikuwa na machafuko makubwa na ugomvi wa majeshi. Mjumbe wa Bwana alisimama mbele yangu, akasema"waite watu wa nyumbani wako, nitakuongoza, nifuate" Aliniongoza hadi kwenye kinjia chenye giza tukapita kwenye msitu, harafu kwenye mianya na uwazi wa milima akasema"hapa uko salama" wapo wengine ambao wlaikuwa wameongozwa kuja kwenye kimbilio hili. Mjumbe wa mbinguni akasema, wakati wa taabu umekuja kama mwivu wakati wa usiku, kama Bwana alivyowaonya namna utakavyokuja".

"Katika wakti wa taabu, mara baada ya ujio wa Kristo, wenye haki watakuwa wametunzwa kwa njia ya Huduma ya Malaika wa mbinguni, Lakini usalama hautakuwepo kwa wale walioivunja sheria ya Mungu. Malaika hawa atawalinda wale watakaokuwa wakiidharau hata kanuni moja tu ya mbinguni."

"Katika kipindi cha mwisho cha historia ya dunia Bwana atatenda kazi kwa nguvu zaidi kwa niaba ya wale wanaodumu kusimama kwa ajili ya haki" – *Maranatha* Ukr. 270.

## *Alhamis* *Tarehe 21 Septemba.*

## 5. UKOMBOZI WA UTUKUFU.

**a. Ni pamoja na mawazo wenye busara kiasi gani tunapaswa kuimarisha akili zetu sasa hivi? Marko. 8:38. Ufunuo. 22.7, 12.**

---

"Tunasubiri kwa hamu kurudi kwa Bwana, tunahitaji kuweka silaha zetu tayari. Tunahitaji jina lote liashirie Ukristo. Tuna hitaji kuishi katika mazoea ya ushirikiano pamoja na Mungu na Mwokozi wetu, tufungwe ndani yake."

"Kristo hajatoa uhakika kwetu kwamba kupata utimilifu wa tabia ni jambo la kawaida au rahisi... je, tuwe waoga wenye kuona haya kwa sababu ya majaribu tunayokutana nayo kadri tunavyozidi kwenda? Je, tusikutane nayo pasipo malalamiko?" – *Manuscript Releases* Vol. 10. Ukr 167.

**b. Nini kitatokea wakati Yesu anaporudi? Zaburi. 50:3-6. 1Thesalonike 4:16-18.**

---

"Ghafla likaonekana wingu kubwa jeupe. Juu yake ameketi mwana wa Adamu... Hakuna lugha ya mwanadamu inayoweza kuelezea utukufu wa tukio hilo. Wingu lililohai lenye utukufu usio na kifani linaendelea kushuka karibu. Tusingeweza kuutazama bila shida upendo wa utu wa Yesu. Hakuvalia tena taji ya miiba, bali taji ya utukufu...

"Gari lile la wingu lilikuwa na mabawa kila upande, na chini yake kulikuwa na magurudumu yaliyo na uhai, kadri gari lile lilivyokuwa likipanda juu, yale magurudmu yalipaza sauti" Mtakatifu" nay ale mabawa yalipokuwa yakienda yalipaza sauti yakiseama"Mtakatifu" nalo kundi la Malaika wlaiolizunguka wingu walipaza sauti wakisema"Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi". Na watakatifu waliokuwa kwenye lile wingu walipaza sauti zao wakisema."Utukufu Haleluya. Ndipo gari hilo likapanda juu kwenye mji Mtakatifu." – *Karama za Roho* Vol. 1 Ukr. 206, 208.

## *Ijumaa* *Tarehe 22 Septemba*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAFAKARI

1. **Siku hizi, kwa vile kila mmoja anashughuli nyingi, njama gani shetani huitumia kupata watu?**
2. **Elezea ushirikiano wa jumbe tatu za ufunuo 16.**
3. **Ujumbe gani hasa kwa nchi unayoishi umefundishwa tangia miaka ya 1880, na unaelekeza nini ikiwa haubadiliki kwa ajili ya waumini?**
4. **Mtihani gani unatujia juu ya upepo wetu kuhusu kupumzika siku ya Jumapili?**
5. **Jambo gani lingekuwa la kwanza katika akili zetu tunayosubiri marejeo ya Bwana wetu Yesu kristo?**

# Matokeo ya Mwisho

**"Jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo amabyo Mungu aliwaandalia wampendao. [1Wakorintho 2. 9]**

"Hebu piga picha kimawazo nyumbani kwa wakombolewa , na ukumbuke kuwa utukufu utakuwa zaidi ya hapo kuliko mawazo [ fikira zake] ziko safi unazoweza kuona" - Hatua za kristo ukr 86.

**Imependekezwa kujifunza:** *Pambano kuu* ukr 658 - 678
*Elimu* ukr 301 - 309

## *Jumapili* *Tarehe 24 Septemba*

### 1. KUSHUKA KWA GHADHABU DUNIANI.

**a. Linatokea jambo gani juu sayari ya dunia wakati wa kurudi kwake muumba? Isaya 24: 1, 3, 5 Yeremia 4: 23 - 26.**

"Wakati wakuja kristo waovu wanatoweshwa katika uso wa dunia yote- wana teketezwa na pumuzi ya kinywa chake na kuangamizwa kwa mng'ao wa utukufu wake. Krsto anawachukua watu w ake na hadi kwenye jiji la Mungu na dunia inaachwa ukiwa , utupu bula wakaaji wake ……

Dunia yote inaonekana kama jangwa la ukiwa magofu ya nyumba ya mji na vijiji yameharibiwa na tetemeko kubwa la nchi, miti inayong'olewa, miamba iliyopasuka imerusshwa nje na bahari au iliyopasuliwa na dunia yenyewe, yote yanatapakaa na kusambaa juu ya uso wa Dunia." -*Pambano kuu* uk 657

**b. Kinatokea nini Kwa Yule aliyeichafua sayari ya dunia? Ufunuo 20:1 - 2**

"[Imenukuliwa katika Yeremia 4 :23- 26 ] Hapa ndipo patakuwa nyumbani na makao ya shetani pamoja na malaika zake waovu kwa muda wa miaka elfu moja" - Ibid ukr 659. *Au pambano kuu* ukr 659.

## 2. MIAKA ELFU MOJA

**a. Elezea maana katika kile ambacho shetani atafungwa minyororo miaka elfu moja. Ufunuo 20:3.**

---

"Akiwa na ukomo wa mipaka [ shetani] wa kusalia katika dunia tu, hataruhusiwa kwenda katika sayri nyingine kwamwe .Anafungwa katika hii, hayupo mwanda atakaye salia ambaye shetani atatumia nguvu zake kumdanganya tena. Amekatwa kabisa katika kazi yake ya udanganyifu na maangamizi ambayo kwa karne nyingi imekuwa ndiyo kazi yake pekee tena ya kupendeza kwake sana...

"Hata waovu sasa wamewekwa mbali na mamlaka ya shetani , na ni yeye yu pamoja na malaika zake waovu , amebakia ili atambue athari ya laana iliyo letwa na dhambi ...

"Kwa muda wa miaka elfu moja , shetani atatangatanga huku na huko katika dunia yenye ukiwa ili kutazama matokeo ya uasiwake juu ya sheria ya mungu. Katika wakati huu mateso yake yanakuwa makali zaidi." *-pambano kuu* ukr 659 , 660 .

**b. Kazi gani inakamilishwa mbinguni kwa wakombolewa tokea vizazi vyote , ambao wata paa kumlaki kristo hewani? Ufunuo 20: 4, 6 1 wakor 6:2- 3**

---

"Wakishirikiana pampja na Yesu kristo [ Watakatifu ] wanawahukumu waovu wakilinganisha matendo yao na kitabu cha sheria Biblia , na kuamua kila kesi sawasawa na matendo yaliyofanywa katika mwili .

Shetani pia na malaika zake waovu , wanahukumiwa - Kristo akiwa na watu wake . 1 bid uk 661.

**c. Ni mahali gani duniani krsto na Yerusalemu mpya utashuka toka Mbinguni mwishoni mwa miaka elfumoja? Zakaria 14:4 , 9 ufunuo 21. 1 – 12**

---

"Yerusalemu mpya unaposhuka chini kutoka Mbinguni katika mng'ao wake wa utukufuu unatua juu ya mahali palipotakaswa na kuandaliwa kumpokea kristo pamoja na watu wake na malaika , wanaingia katika mji mtakatifu." - 1 bid ukr 663 .

**d. Ni mtazamo gani wa watu waliofufuka katika ufufuo ambapo hufuatiwa na miaka elfu?**

---

**e. Watu waliofufuka katika ufufuo ambao hufuatiwa na miaka elfu wanakuwa na mtizamo wa aina gani? Ufunuo 20: 5 [mwanzoni] 7-8**

---

## 3. MADANGANYO KATIKA UHARIBIFU

**a. Elezea njama za udanganyifu wa mwisho wa shetani, na jinsi anavyo adhibiwa. Ufunuo 20: 9- 15 Malaki 4:1**

---

“Kadri waovu wanapofufuliwa [ shetani naye akiona umati mkubwa sana ukiwa upande wake , matumaini yake yanaamuka , wala hadhamini kuachana na pambano kuu ataimarisha majeshi yake yote ya waliopotea ambao wako chin ya bendera yake na katika kupitia hao anajaribu kutekeleza mipango yake. Waovu ni mateka wa shetani, kwa kumkataa kristo wamekubali kupokea kanuni za kiongozi mwasi. Wako tayari kupokea na kukubali mashauri yake na kutenda maagizo yake . Akiwa bado anaamini katika werevu wake wa hapo awali. Hataki kujikubali mwenyewe kwamba yeye ndiye shetani. Anadai kuwa ndiye mfalme halali mwenye haki ya kumiliki ulimwengus, na anadai kwamba alinyang’anywa urithi wake kidharimu . Anajiwakilisha mwenyewe Kama mkombozi Kwa Rais wake aliowadanganya na kudanganyika. akiwahakikishia kwamba yuko karibu sana kuwakomboa kutoka kwenye utawala wa mabavu kandamizi wenye ukatilii mkuu. Kwa kuwa nguvu ya uwepo wa kristo itakuwa haipo shetani anatenda miujiza ili kuunga mkono madai yake . Anawafanya waliodhaifu kuwa na nguvu na kuwavuvia wote kwa Roho na nguvu zake mwenyewe . Anapendekeza na kuwashauri wapambane na kambi ya watakatifu na kuumili mji wa Mungu...

“Kwa utaratibu wa kijeshi misafara ya maaskari inasonga mbele juu ya uso wa dunia iliyovunjika vunjika na kupasuka na kubomoka bomoka kuelekea kwenye mji wa Mungu kwa amri ya Yesu malango ya Yerusalemu mpya yanafungwa , na majeshi ya shetani linauzingira mji na kujitayarisha tayari kwa ajiliya kuanza mashambulizi - pambano kuu ukr , 664 .

“Moto unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu , ardhi ya dunia inavunjika vunjika silaha zinafichwa kwenye mashimoyake na kufukiwa kabisa. Ndimi za moto ulao na kuteketeza zinafumuka kutoka kila upande wa shimo. Kila mwamba unaanza kuwaka moto …. Waovu wanapokea malipo Yao duniani ….. Wengine wlaiangamia Kwa mda mfupi, wakati wengine waliangamia Kwa mda mrefu wa siku. Wote wanaadhibiwa kulingana na matendo yao [ sab 28: 4 ] Dhambi za wenye Haki zinahamishwa kwa shetani , zinamfanya ateseke siyo tu kwaajili ya uasi wake mwenyewe , bali pia kwaajili ya dhambi zote ambazo amewasababishia watu wa mungu kuzitenda . Adhabu yake itakuwa kubwa zaidi kuliko wale aliowadanganya .Baada ya wote ambao walianguka kutokana na madanganyoi yake kuw a tayari wameangamizwa , ataendelea bado kuishi na kuhangaika ndani ya moto. Hatima waovu na uovu utasafishwa kwa ndimi za moto usafisha shina na Tawi , shetani ndiye shina , na wafuasi wake ni matawi . Adhabu kamili ya shetani imaptilizwa , madai ya haki yametimia , Mbingu na nchi zinatangaza haki ya Yehova” - Ibid ukr 672 , 773 *au pambano kuu* ukr 672 , 673.

## 4. KULINDWA MILELE.

**a. Kristo anawakinga wenye haki kwa namna gani na moto usiozimika? Zaburi 84:11**

''Wakati dunia ilipofunikwa ktk moto wa maangamizi wenye Haki walikuwa salama salimini ndani ya mji mtakatifu;- Pambano kuu ukr 673.

**b. Ni tukio gani lenye utukufu wa matokeo ya utakaso wa dunia?**

''Moto unaowatekeleza waovu huitakasa pia dunia.Kila alama ya laana inaondolewa na kufunguliwa mbali.Hakuna moto wa jehanamu ya milele, ambao ni ukumbusho wa kutisha wa matokeo ya dhambi; - *Pambano kuu* 674. Ibid 674.

**c. Kwa ajili yetu siku hizi, Bado tunakaa kwenye sayari iliyopandwa mahangaiko na masumbufu(matatizo) mahali gani utnapaswa kutazama kwa ajili ya makao yetu ya milele? 2 Petro 3.13 1Wakorintho 2.9.**

''Lugha iliyobora zaidi haiwezi kuusimulia utukufu wa mbinguni au kina cha upendo wa mwokozi usiopimika;- Maandiko ya awali ukr 289.

Hofu, woga unaowafanya watakatifu wenye urithi waonekane malighafi hasa umewaongoza wengi kwenye njia ya kweli ya kiroho ukweli halisi ambao unatuongoza sisi kuitazama mbingu mpya kama nyumbani. Kristo aliwahakikishia wanafunzi wake kwamba anaenda kuandaa makao kwa ajili yao.Wale wanaopokea mafundisho ya Neno la Mungu, kwa ujumla hawatapuuza makao ya mbinguni; -*Histiria ya Ukombozi* ukr430.

**d. Ni maelezo gani makuu Yohana hutupatia sisi ya mbingu mpya?Uf 21.3-4:22.1-5.**

''Pale chemi chemi hububujika daima, maji angavu kama kioo, na (pembeni)yake kuna miti inayopepea ikitupa kivuli chake kwenye njia iliyoandaliwa kwa ajili ya wakombolewa wa Bwana.Kuna Tambarare pan asana zinazopandia kwenye vilima vya uzuri, na milima ya Mungu iliyosimamisha vilele vyake vya kupendeza sana.Ktk hizo tambarare tulivu, kando ya chemichemi zilizo hai, Hapo ndipo watu wa Mungu ambao kwa mda mrefu sana wamekuwa wasafiri wenye kutangatanga, watapata makao; - *Pambano kuu* ukr 675.

## *Alhamis* — *Tarehe 28 septemba*

### 5. FURAHA YA MILELE.

**a. Ni hali gani katika ulimwengu mpya inakuwa kumbukumbu? Isaya. 35:5-10, 65:25. Taswila ya maisha ya kimbingu ni ya namna gani?**

---

"Tena naliona shamba lenye majani marefu, mazuri sana kwa kutazama. Lilikuwa na rangi ya kijani kibichi, lilikuwa likiakisi Nuru ya rangi ya fedha na dhahabu, likipepea kwa fahari ya utukufu wa Yesu mfalme. Baadaye tuliingia kwenye uwanda mmoja uliojaa wnayama wa kila aina – Simba, Chui, Mwanakondoo na Mbwa mwitu, wote kwa pamoja katika umoja mkamilifu." - *Maandiko ya Awali* ukr. 18.

"mkali atakuwa mpole, na mwenye woga na aibu atakuwa mwneye *kujiamini Elimu* Ukr. 304.

**b. Nani ambaye atakuwa kituo cha kila kitu kwa ajili ya umilele wote, na kwa namna gani hili litajulikana? Zakaria. 13.6, ufunuo. 7:15-17, 5:13.**

---

"Hakuna Jehenamu ya moto wa milele itakayowekwa mbele kama fidia ya kutisha matokeo ya dhambi. Kumbukumbu moja pekee inabakia. Mwokozi wetu pekee daima atabakia na Alama za kusurubiwa kwake." – *Roho ya Unabii* Vol. 4 Ukr. 489.

"Kadri miaka ya umilele inavyoendelea, ndivyo itakataa mafunuo ya utajiri na utukufu wa Mungu na wa Kristo zaidi na zaidi. Na kadri maarifa yanavyozidi kuongezeka, ndiyo pia upendo, kicho, na furaha vinavyoongezeka. Kwa kadri watu wanavyozidi kujifunza kuhusu Mungu zaidi, ndivyo kupendezwa kwao na tabia yake kutakavyozidi kuongezeka...

Pambano kuu limekoma. Dhambi na wenye dhambi hawapo tena katika viumbe vyote. Kutoka kwake yeye aliyeviumba vitu vyote, hububujika uzima na Nuru na furaha katika ufalme wote usio na ukomo. Kutoka kwenye sehemu ndogo kabisa hadi kwenye ulimwengu mkubwa kabisa. Vitu vyote, vilivyohai na visivyo hai, aktika uzuri wake halisi na kwa furaha kamili hutangaza kuwa Munguni upendo (pendo)" *-pambano kuu*. 678.

## *Ijumaa* — *Tarehe 29 september*

### MASWALI BINAFSI YA KUTAKARI.

1. **Kwa nini muhimu sana kujiandaa kwa ajili ya marejeo ya Yesu?**
2. **Fafanua kushindwa mara kwa mara kufahamu malengo ya Milleniumu.**
3. **Eleza njama ya mwisho ya shetani, kwa nini watu watadanganyika ...?**
4. **Tunahitajika kutambua nini kuhusu maisha katika ulimwengu mpya unaofanywa?**
5. **Uzuri wa umilele ni upi, kwa nini tunapaswa kuufahamu na kuuthamini?**

## TUMAINI LENYE BARAKA

Wakati mwokozi alipo kuwa karibu kujitenga kutoka kwa wanafunzi wake aliwafariji kutoka katika huzuni yao kwa kuwahakikishia kwamba angekuja tena "Msifadhaike mioyoni mwenu ….. Nyumbani mwa baba yangu mna makao mengi …. Naenda kuwaandalia mahali.Basi Mimi nikienda kuwaandalia mahali nitakuja tena niwakalibishe kwangu , ili nilipo mimis nanyi muwepo [Yohana 14: 1 -3 ] mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wake na malaika watakatifu pamoja naye , ndipo atakapoketi , katika kiti cha utukufu wake na mataifa yote yatakusanyika mbele zake [ mathayo 25: 31- 32]

"Malaika waliozungukazunguka juu ya mlima wa mizeituni baada ya kupaa kwa kristo walirudia ahadi ya kurudi kwake kwa wanafunzi .Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni atakuja jinsi hiyo hiyo mliyomwona akienda zake Mbinguni [matendo 1:11]. Na mtume Paul akiongea kwa uvuvio wa Roho alithibitisha " Kwa sababu Bwana mwenyewe parapanda ya Mungu [ 1 thesalonike 4: 16 ] Nabii yohana wa Patimo anasema tazama yuaja na mawingu , na kila jicho litamwona [ ufunuo 1: 7 ]

"Utukufu wa kundi la karibu na kuja kwake ambalo ilimpasa kupokewa mbinguni hata zile zamani za kufanywa upya vitu vyote , zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea zamani mwanzo wa ulimwengu [ matendo 3:21 ] Ndipo kanuni ya uouvu ya kuendelea kwa muda mrefu mrefu itavunjwa

Falme za ulimwengu huu , zitakuwa falme za Bwana wetu zake kristo , naye atamiliki hata milele na milele [ufunuo 11:15 ] Utukufu wa Bwana wetu utafunuliwa wote wenye mwili watauona pamoja , "Bwana Mungu ataonyesha haki na sifa mbele za mataifa yote. Atakuwa ni taji ya fahari na kilemba cha uzuri kwa mabaki ya watu wake [Isaya 40: 5 , 61: 11 , 28: 5]

Kisha itakuwa kwamba ufalme wa Amani wa masihi uliotaamaniwa kwa muda mrefu utaanzishwa chini ya Mbingu yote.

"Kuja kwa bwana limekuwa tumaini la vizazi vyote kwa wafuasi wake na kweli. Ahadi ya mwokozi alipoachana nao juu ya mlima wa Mieitunianglekuja tena , iliangaza kipindi cha mbele cha wanafunzi wake ikiijaza miuoyo yao kwa furaha na tumainiambapo huzuni au giza la taabu , visingeweza kuizimisha . Katikati ya taabu na mateso, kuonekana kwa mungu mkuu na mwokozi wetu Yesu kristo , lilikuwa Tumaini lenye Baraka wkaati wakristo wa pale thesalonike walipojawa na huzuni walipokuwa wakizika wapendwa wao.Ambao walitumaini kwamba wangeishi na kushuhudia kuja kwa Bwana , Mwalimu wao Paulo aliwatazamisha kwenye ufufuo utakaofanyika wkaati wa marejesho ya mwokozi kisha waliokufa katika kristo waamuka pamoja na walio hai watanyakuliwa juu kumlaki Bwana hewani . Alisema hapo ndipo tutakuwa na Bwana milele na milele , Basi farijianeni kwa maneno hayo [ 1 Thesalonike 4: 16 – 18 ] . „*The great controversy* ukr 301, 302."

# Note

# Note

# Sadaka za sabato ya kwanza




**01 JULAI, 2017.**
Ni kwa ajili ya Kanisa dogo lililoko Washington DC nchini Marekani.

**Angalia p. 4**

**05, AUGUST**
Ni kwaajili ya shule za utume za miradi ya elimu.

**Angalia p. 30**







**02 SEPTEMBA 2017.**
Ni kwa ajili ya makao makuu ya Misheni – Fiji.

**Angalia p. 51**